- SAFARI -

# SAFARI KIJIJINI

Jifunze namna ya kushuhudia upendo na ujumbe wa Yesu

DIGNITY

www.dignityonline.org.uk

**Safari**

Kozi ya masomo ya Dignity

**Safari Kijijini**

Toleo la pili, 2024

Kiswahili

**Ilani ya Hakimiliki na Sheria (Toleo la pili, Desemba 2024)**
Kazi hii kwa ujumla ni Hakimiliki © Dignity 2020, 2024 isipokuwa maeneo yaliyowekwa chini ya maandishi.

Mwandishi anazuia haki ya kudai bila kutuliza hakimiliki hii juu ya kazi zote za asili zilizomo ndani ya chapisho hili. Kazi hii inaweza kuzalishwa kwa ukamilifu na kusambazwa na Dignity (Ulimwenguni), Kampuni Iliyodhaminiwa kwa Dhamana. Imesajiliwa Uingereza na Wales No. 6394480. Chama cha Kusaidia No. 1122656.

Watu binafsi wanaruhusiwa kutoa nakala moja ya kazi hii kamili kwa matumizi yao binafsi. Maandishi ya kazi hii siku zote ni lazima kuchapisha kitabu kamili na haikubaliki kubadilishwa kwa namna yeyote. Hairuhusiwi kuchapishwa nakala nyingi.

Kama wewe ama shirika lako lingependa kuchapisha nakala nyingi kwa lengo la kusambaza, tafadhali wasiliana na Dignity uweze kupewa idhini. Gharama inaweza kuhitajika.

Kwa namna yeyote kazi hii hairuhusiwi kuchapisha nakala kwa lengo la kuuza na taasisi yeyote zaidi ya Dignity (Worldwide) Ltd.

Dignity
6 Barlow Moor Road
Didsbury
Manchester
M20 6TR
United Kingdom

Tovuti: hello@dignityonline.org.uk
No ya simu: +44 (0)7340 573 937

**Kikundi Kinachohusika na Safari**
Waandishi na Wahariri: Jon Paul Witt, Rebecca Burr, Ethan Witt na Jo Kimball
Msanii-Mchoraji na Mpangilio: Akash Sunny na Jo Kimball
Kusahihisha: Elisabeth Cartwright
Somo la 8: Kuomba kwa Pamoja ikijumuisha sehemu za asili iliyoandikwa na Sarah Small na Tobbias Ngala

**Vifungu vya Biblia**
Biblia Takatifu kwa Kiswahili, Muunganiko wa Vifungu, iliyochapishwa kama Biblia. Ilichapishwa kwa pamoja na Chama cha Biblia Tanzania, S.L.P. 175, DODOMA, Tanzania na Chama cha Biblia cha Kenya, P.O. Box 72983-00200, NAIROBI, Kenya.

**Taswira za Alama Zinazoongoza**
Taswira za Alama Zinazoongoza zimechorwa na Studio ya Metro Icon 5 iliyochapishwa na SyncFusion. Alama zimetumika kwa ruhusa.

# Yaliyomo

Kuhusu *Safari* ... 1
Marafiki Safarini ... 5
Kulinda watoto wetu tunapokuwa katika Vikundi vya Uzima ... 7
1: Miti Mikubwa ya Haki ... 8
2: Safari ya Dignity ... 20
Chombo Cha Kazi: Tembea na Yesu ... 30
3: Injili ni Nini? ... 32
4: Uzima ni Kupitia Familia ... 43
Chombo Cha Kazi: Kuwatayarisha Watu wa Mungu ... 52
5: Kila mmoja anayo Mahali ... 55
6: Kuendesha Vikundi Vikunda vya Uzima ... 67
Chombo Cha Kazi: Kuwa Mchungaji ... 78
7: Shuhudia Upendo na Ujumbe wa Yesu ... 81
8: Waombee Watu ... 92
Chombo Cha Kazi: Kujifunza Kuto Kukubaliana ... 103
9: Uwe na Imani ... 106
10: Muktasari – Nimejifunza Nini? ... 116
Orodha za Picha ... 127

# Kuhusu *Safari*

Mitume ni 'wale waliotumwa' wa kanisa la kwanza. Paulo na mitume wengine walichukua safari kubwa ya imani. Walipata njia ya kuwaeleza watu habari za ujumbe wa Yesu na kuchukua muda kuonyesha upendo na nguvu za Yesu kwenye jumuia na vijiji vingi. Hapo mwanzo waliwafundisha watu kuishi kwa kweli ya Yesu, wakisambaza ujumbe na matendo ya upendo wa Yesu kwao wenyewe. Haikuwahusu mitume wenyewe, iliwahusu watu wote.

Hapa ndipo unapohusika. Dignity imeanzisha ***Safari***, kozi ya kukusaidia kufuata hatua za wafuasi wa kwanza wa Yesu. Tunataka wewe ujifunze namna ya kuchukua hatua hizo wewe mwenyewe.

Kujifunza ***Safari*** itakupa wewe nafasi ya kujifunza kufanya kazi na Mungu, kuanzia kwenye kijiji chako au jumuia. Huhitaji kuhudhuria shule. Utajifunza mafundisho mahali pale pale ulipo, hata na marafiki wanaokuzunguka. Wakati kozi inapoendelea utawashirikisha watu ujumbe na upendo wa Yesu kila siku kwa wanakijiji na jumuia inayokuzunguka.

***Safari*** ni mtiririko wa vitabu vinne. Katika kila kitabu utajifunza namna ya kushiriki upendo na ujumbe wa Yesu kwa kuanzisha Vikundi vya Uzima au kuwasaidia wengine kufanya hivyo. Ni jambo la muhimu kufanya kazi kwa vitendo. Hii itakuwezesha wewe kuanzisha kazi ya Mungu kwa vitendo badala tu ya kujifunza. Utaendelea na kitabu kinachofuata wakati kazi ya vitendo imekamilika.

***Safari Kijijini*** inawasaidia watu binafsi kutambua hali iliopo sasa kwenye vijiji vyao na namna Kikundi cha Uzima inavyokuleta upendo wa Yesu na kujenga umoja. Watu binafsi watakuwa wameanzisha Kikundi cha Uzima mwisho wa kitabu hiki.

***Safari ya Eneo*** inawasaidia watu binafsi kukua na kupanua kazi ya Vikundi vya Uzima kwa kuwahusisha wengine, hata kuanzisha Vikundi vya Uzima vingine. Watu binafsi watakuwa wamesaidia Kikundi cha Uzima kuanzisha kikundi kingine mwisho wa kitabu hiki.

***Kuelekeza Safari*** hupeleleza namna ya kuanzisha Vikundi vya Uzima vipya kwenye maeneo mapya na watu wapya. Watu binafsi watakuwa wamewasaidia wengine kuanzisha Vikundi vya Uzima kwenye maeneo mapya mwisho wa kitabu hiki.

***Kuongoza Safari*** husaidia watu binafsi kupata maono ya kwa ajili ya Vikundi vya Uzima kuanzishwa nchini kote. Watu binafsi watakuwa wamewasidia kuanzisha Vikundi vya Uzima kwenye maeneo mapya mwisho wa kitabu hiki.

# Namna ya kutumia Kitabu Hiki

## Nini kimo ndani ya kitabu hiki

Ndani ya kitabu hiki utajifunza namna ya kushirikisha upendo na ujumbe wa Yesu kwa kuanzisha Vikundi vya Uzima au kuwasaidia wengine kufanya hivyo. Utafanya hivyo kupitia masomo 10 ndani ya kitabu hiki, hivi ni vipindi pekee vilivyomo. Kila somo litachukua masaa 1.5 – 2. Inashauriwa ukamilishe wiki moja.

Kila mmoja wetu anapenda kufanya kazi na Mungu vizuri. Ndani ya kitabu hiki, kuna 'Chombo cha Kazi' vinne makala ya kukusaidia kufikiri namna ya kufanya kazi (kutumika) na Mungu, kuyajenga uzima yako au kukupa taarifa. Kila makala itakuchukua kama dakika 30 kusoma na kufikiri. Inayo maswali ya kukusaidia kufikiri kuhusu taarifa, mbinu au mwongozo kwa yale uliyoyasoma.

**Vitu unavyovihitaji kwa kila Somo**

Masomo yameandaliwa kuwa marahisi na hayahitaji vyanzo vingi. Utahitaji kuwa na:

- Nakala ya kitabu hiki, ***Safari Kijijini***
- Kijitabu cha kumbukumbu au daftari ya shule
- Biblia
- Kalamu

Zipo vyanzo vingine ambavyo Dignity imeandika, utapata vingi zaidi juu ya hivi unaposoma kupitia somo na makala.


***Kitabu chako cha kumbukumbu***

Ikiwa kuna swali au shughuli ndani ya kitabu hiki unaweza kuandika majibu yako ndani ya kitabu chako cha kumbukumbu.

Kuandika kumbukumbu na kujibu maswali kwenye kitabu chako cha kumbukumbu ni namna ya kupanua uelewa wako na kukumbuka kile ulichojifunza. Kuwa na muda wa kuandika chini majibu yako, na kuyafikiria kwa makini juu yake na hata kurudia kusoma tena itakusaidia kusikia yale Mungu anayokuambia wewe wakati unajifunza ***Safari Kijijini.***

**Alama za kukusaidia**

Kukusaidia kufanyia kazi somo tumeweka alama kukujulisha kila sehemu inasema nini. Alama zimeorodheshwa hapo chini na maana zake. Chukua muda sasa kujua kila alama ina maana gani na tazama masomo machache na ujifunze jinsi alama zinavyotumika. Hii itakupa urahisi wakati unapojifunza.



**Lengo**

Kila somo ina malengo 2 au 3. Hizi ni ishara za kukuongoza kukuelekeza kule somo linakoelekea.



**Tazama Nyuma**

Kila mwanzo wa kila somo tunataka kukutia moyo utazame nyuma kwenye somo lililopita na ufikiri yale uliyoyafanya na yale ambayo Mungu amekufundisha. Utaulizwa kufikiri yale uliyoyajifunza wiki iliyopita, jinsi unavyoyaingiza kwenye matendo na umemshirikisha nani.

**Hadithi**
Hadithi ni njia nzuri ya kujifunza kitu kinachojulikana. Mahali popote utakapoona alama hii ni muhimu sana kusoma kusoma hadithi yote kufikiri somo linatufundisha nini. Ikiwa unajifunza na kikundi soma hadithi kwa sauti na kwa kiasi kikubwa, ili kikundi chote kiweze kuelewa.

**Mafundisho**
Utakapoona alama hii kiki ni kiini cha mafundisho ya somo, kwa hiyo soma sehemu hizi pole pole na kwa uangalifu. Ikiwa unajifunza na kikundi soma mafundisho kwa sauti ili kikundi chote kiweze kusikia, soma pole pole ili kila mtu aweze kuelewa. Uliza kikundi kama kuna maneno yeyote au sentensi ambazo hawazielewi, ili uweze kurudia hayo tena na kuwaeleza kwa maneno yako mwenyewe.

**Vifungu vya Biblia**
Unapoona alama hii hakikisha unasoma vifungu vya Biblia pole pole, unaweza hata kusoma mara mbili na utafute ndani ya Biblia pia. Ikiwa unajifunza na kikundi na watu kwenye kikundi chako wanajisikia vizuri kusoma, unaweza kubadili na kusoma vifungu vya Biblia. Pengine unaweza kurudia kusoma mara mbili kuhakikisha kila mtu amesikia na kuyaelewa.

**Maswali**
Maswali ni njia kubwa ya kukusaidia kujifunza na kufikiri. Jibu maswali ndani ya kitabu chako cha kumbukumbu, kwa njia hiyo unaweza kuwarudia tena. Ikiwa unajifunza na kikundi tumia maswali kwenye somo hili ili kuwepo na majadiliano, ili kila moja aweze kushiriki kutoa majibu yao. Kujadili maswali kwa pamoja itamsaidia kila moja kuyakumbuka.

**Shughuli**
Alama ya shughuli inamaanisha unahitajika kufanya jambo kukusaidia kujifunza, unaweza kutumia kitabu chako cha kumbukumbu kwenye maeneo haya. Ikiwa unajifunza na kikundi mnaweza kufanya shughuli pamoja. Unaweza kutumia majadiliano kuwasaidia watu kujifunza.

**Hadithi ya Kikundi cha Uzima**
Hizi ni hadithi za kweli za watu wanaojihusisha na Dignity. Tunataka hadithi hizi zikuhamasishe kufanya kitu kama hicho kijijini kwako. Ikiwa unajifunza na kikundi unaweza kuchagua kufanya igizo za hadithi hizi pamoja. Hii itawasaidia wao kukumbuka!

**Omba**
Tunataka kusisitiza maombi kila inapowezekana. Unapoona alama hii chukua muda kuomba kwa yale uliyoyakamilisha kwenye somo, labda Mungu ameleta kwenye mawazo watu maalum au hali Fulani ya kuombea. Ikiwa unajifunza pamoja na kikundi mwombe kwa pamoja au kwenye vikundi vidogo. Mpe kila moja nafasi kuomba kwa sauti na ushirikishe chochote unachohisi Mungu anasema.

**Kufanya Wiki Hii**
Unapo fanyia kazi sehemu 'Kufanya Wiki Hii' utakuwa unachukua hatua inayohitajika kuanzisha Kikundi cha Uzima. Utakapomaliza kitabu hiki utakuwa umekusanya Kikundi na mtakuwa mmeanza kukutana na kutafuta njia ya kushiriki upendo na ujumbe wa Yesu.

**Mpigie simu mtu wako wa mawasiliano**
Kila mtu anayejifunza Safari ni muhimu kuwa na 'mtu wa kuwasiliana naye' – huyu ni mtu ambaye ni rafiki kwenye safari, anayekutia moyo na kukusaidia. Alama hii ni ya kukumbusha kuwasiliana na mtu wako wa mawasiliano.

**Andika Chini**
Baada ya kufanya shughuli ya matendo, itakuwa vizuri kuandika baadhi ya kumbukumbu kwa ajili ya kujikumbusha mwenyewe. Kila somo inajumlisha kumbukumbu ya kuyafanya haya, pamoja na baadhi ya maswali ya kukusaidia wewe.

**Kutumia kitabu hiki na kikundi**
Kitabu hiki kimeandaliwa kwa mtu binafsi kujifunza, hata ingawa inaweza kutumika na wengine kwa kujifunza katka kikundi. Kutmia kozi na wengine itawasaidia wao kueneza upendo na ujumbe wa Yesu kwenye vijiji vyao pia.

Ikiwa utatumia kitabu hiki na wengine, ni muhimu kumuusisha kila mtu kwenye somo. Siyo kitu tu rahisi ya kusoma somo na kuwaambia watu kile cha kufanya. Tunaamini kuwa kila mtu ana kitu cha kipekee cha kushirikisha na Mungu anatufundisha kupitia hao wanaotuzunguka. Kama kiongozi wa kikundi unapaswa kushika usukani wa majadiliano na kuisaidia iende kwenye lengo sawa, lakini hupaswi kufanya kila kitu mwenyewe. Unatakiwa kuwatia moyo watu wenye aibu na wakimya kujaribu kuongea pale wanapoweza. Unapaswa pia kuwata moyo wale wenye sauti kubwa na wazungumzaji kuwapa watu wengine nafasi kushirikisha mawazo yao pia.

# Marafiki Safarini

Ni vizuri mara zote kutembea na marafiki. Marafiki wanaweza kushiriki mambo mazuri na wakati mwingine mambo magumu kwenye uzima pamoja nasi. Yanaweza kutupa changamoto, kututia moyo na kuwa washindi.

Yesu alituonyesha umuhimuwa urafiki. Alishiriki uzima yake na wale wanafunzi wake 12. Katika kitabu cha Luka 24 tunaona hadithi ya Cleopas na rafiki yake wakisafiri kuelekea Emmaus. Walipokuwa wakitembea walikuwa wakijadiliana matukio yaliotokea hivi karibu ya Yesu kufa na maneno yamesikika kuwa 'amefufuka' tena. *"Walipokuwa wakiendelea kujadili juu ya jambo hilo, Yesu mwenyewe alijiunga nao na kutembea nao"* (Luka 24:15-16).

Wakati unajifunza kozi ya ***Safari***, ni muhimu sana kufanya hivyo na marafiki.

**Mtu wa Kuwasiliana Naye**
Unapofanya kazi na ***Safari*** na kuanzisha Kikundi cha Uzima kuna kupanda na kushuka. Kuna mambo mengi ya kujifunza na maswali ambayo ungependa kuuliza. Pengine ungemwitaji mtu wa kuzungumza naye juu ya mambo makubwa yanayotokea na changamoto unazokabiliana nazo. Rafiki wa muhimu katika safari ni yule aliyekualika kujifunza kozi hii. Inaonekana wao tayari wanao ujuzi wa kuanzisha Vikundi vya Uzima na wanafahamu kupanda na kushuka kwa kazi hii. Itawatia wote moyo mnapowasiliana.

Na ikiwa huna mtu wa kuwasiliana naye, basi wasiliana na Dignity kwa **hello@dignityonline.org.uk** au tumia WhatsApp kwa no **+447340 573 937**. Tutakuunganisha na mtu ambaye yuko maeneo yako anayeshughulika na Vikundi vya Uzima.

**Agnes, Mutambo & Asisi**
Unapojifunza ***Safari Kijijini*** utakuwa unafuatilia tabia za watu watatu ambao wako kwenye hatua tofauti ya ***Safari***. Utasikia tabia zao kwenye vipindi, hivyo zifuatilie! Zitakusaidia kufikiri juu ya kijiji chako mwenyewe na jambo la kufanya baada ya hapo.



**Agnes**
Agnes anaishi Kalambwa. Alijulishwa masomo ya Dignity na Fred binamu yake umbali wa km 500. Alijiunga na kozi ya ***Safari*** na kwa majuma amekuwa akijifunza Kikundi cha Uzima ni nini na kwa nini ni jambo jema kulianza. Ametamani sana kuanzisha kikundi na amezungumza na watu wengi. Amekuwa akiwasiliana na Julius anayeendesha kozi Zambia, na amekuwa akimtia moyo. Agnes na baadhi ya marafiki zake wako karibu kuanzisha Kikundi cha Uzima kwa wiki chache zijazo.



**Mutambo**
Mutambo ni kiongozi wa kanisa la High Faith nje ya Johannesburg, Africa ya Kusini. Anayo moyo wa kushawishi kanisa kuja pamoja na kufikia jumuia inayowazunguka. Amefanya ushirika na Dignity na amekuwa mtu wa kuunganisha huduma hii kwenye maeneo mengine. Amekuwa akiwasaidia kufanya kazi kupitia *Safari Kijijini* na *Safari ya Eneo*. Mutambo alijifunza vitabu hivi mwenyewe mwaka uliopita na alipozijifunza na kuingiza kwenye matendo alihamasika kuwasaidia wengine kufanya hivyo.



**Asisi**
Asisi anaishi Kenya na akaona kwenye mtandao matangazo ya Dignity. Kwa vile kozi ni bure alijisajili, akajifunza namna ya kuanzisha Kikundi cha Uzima akaenda kuvianzisha. Asisi amekuwa akijifunza namna na kuwatia moyo wengine kuanzisha vikundi pia. Wanapeleleza jinsi Kikundi cha

Uzima vilivyopo vinaweza kuanzisha vingine na kuunda umoja. Anayo shauku kubwa kuona nini kitakachotokea.

# Kulinda watoto wetu tunapokuwa katika Vikundi vya Uzima

Pamoja tunaweza kutengeneza masharti ili watoto wetu wawe salama wanapokuwa nyumbani au katika Kikundi cha Uzima pamoja nasi. Masharti au sheria hizi zinafaa kufanyia kazi katika sehemu tofauti katika uzima yetu. Ikiwa tunafanya kazi katika mitaa, kanisani au pamoja na marafiki, Mungu anataka watoto wetu wawe salama.

Kila mmoja anayehudhuria Kikundi cha Uzima lazima ahakikishe kuwa watoto wake wako salama nyumbani na wanaangaliwa na mtu mzima au wanaweza kuja na watoto wao.

Viongozi wa vikundi lazima wawakumbushe washirika kuhakikisha kuwa watoto wao wako salama nyumbani na wanaangaliwa na watu wazima au wawakaribishe katika kikundi.

Yeyote anayewashughulikia watoto katika kikundi asifanye kazi peke yake bali asaidiwe na mtu mmoja au wawili. Ikiwa ni watu wawili, hawapaswi kutoka katika familia moja. (Lazima watoke katika familia tofauti.)

Wale wanaoshughulikia watoto katika kikundi lazima wawe wamehudhuria vikao vya kikundi angalau kwa kipindi cha miezi mitatu mfululizo.

Viongozi wa kikundi na na washirika hawapaswi kupiga watoto picha wanapojishughulisha na Kikundi cha Uzima.

Ikiwa watoto wanakula kwa pamoja katika Kikundi cha Uzima, hakikisha chakula wanachokula ni salama na hakina madhara yoyote kwao.

Wanavikundi wanapotembelea familia katika vijiji lazima wawe katika makundi ya wawili wawili, kwa mfano wanaume wawili wamtembelee mwanamume au wanawake wawili wamtembelee mwanamke.

# 1



# Miti Mikubwa ya Haki

Wapate kuitwa miti ya haki,
iliyopandwa na Bwana,
ili atukuzwe.

Isaya 61:3

**Lengo**

Wewe na wengine wanaomfuata Yesu wanayo nafasi ya muhimu ndani ya kijiji chako. Somo hili litakusaidia kujua yale ambayo Mungu anasema na wewe kuhusu kijiji chako kwa kutazama kitabu cha Isaya 61:1-4.

**Mwisho wa somo hili utakuwa na:**

- Umefahamu mti mkubwa wa Mungu ni nini
- Umefahamu kuwa unayo nafasi ya muhimu kwa yale ambayo Mungu anafanya
- Hata hivyo waza juu ya hali ndani ya kijiji chako au jumuia

**Hadithi: Pilius Anachukua Hatua**

Pilius aliishi katika kijiji cha ndani ya vijiji vya Zambia. Mama yake na na baba wanafanya kazi kwa bidii kwa ajili ya familia yao. Walilima kwa vizazi na kila wakati wa mvua walipanda na kupalilia mazao ili waweze kutunza familia yao. Hayo ndiyo yamekuwa uzima yao mwaka kwa mwaka. Pilius alipofikisha umri wa miaka kumi, hayo ndiyo uzima aliyoyafahamu.

Familia yake ilikuwa maskini, maskini sana kiasi cha kwamba wakati mwingine walikosa chakula na hawakuweza kuwapeleka watoto wao shule. Gharama za vitabu, mavazi na mitihani yalikuwa makubwa sana kwao. Uzima ya mbele hayakuonyesha mwanga wowote kwa Pilius na familia yao.

Siku moja Pilius aliukuta mti wa mopani. Miti ya mopani ni miti imara na hata ingawa huchukua muda mrefu kukua, inazalisha zao linalogarimu pesa nyingi. Siyo hivyo tu, kivuli chake kinaleta tulizo kwa kazi ngumu ya wanakijiji wanapopumzika chini ya kivuli chake. Mbegu nyingi za mti wa Mopani zilizagaa kuuzunguka mti. Pilius alizikusanya na kuzipeleka nyumbani. Kabla ya giza kuingia alizotesha akatumia mbolea kidogo iliyokuwepo kuzikuza nayo.

Miaka iliendelea na Pilius akakuwa, na miti pia. Baada ya miaka 10 alianza kuwa mtu mzima na miti nayo ikaendelea kukua. Mbegu nyingi ilizalishwa na miti mingi ikaoteshwa. Baada ya miaka 20, Pilius ameshakuwa mtu mzima, wa miaka 30. Alizunguka kutazama miti mingi aliyootesha iliyozunguka kijiji chake. Ilikuwa ni sehemu ya kivuli, mahali ambapo watu waliweza kufanya kazi bila kuunguzwa na jua kali. Pilius akakumbuka jinsi mbao zilivyokuwa na dhamani, hivyo siku moja waliuangusha mmoja na kuuza mbao. Mwaka huo wakawa na chakula zaidi ambayo wasingaliweza kusahau.

Wana kijiji wengine wakaangalia kilichotokea, nao pia wakaotesha miti na kwa wakati wengi wakavuna faida ya kivuli, pesa na mabadiliko yaliyoletwa na miti katika kijiji.

Haya yote yalianzishwa na kijana mdogo tu, kupanda mbegu. Aliitunza, akaijali akahakikisha inakua na kukua. Kitendo cha Pilius ilibadilisha kijiji chake milele.

**Maswali**

(Kumbuka kuandika majibu yako kwenye kitabu chako cha kumbukumbu)

- Pilius alichua hatua gani?
- Kitendo cha Pilius ilileta athari gani kwa familia yake na kijiji chote?
- Ni nini kingetokea kama Pilius asingechukua hatua?
- Unafikiri hadithi ya Pilius inatufundisha nini?

**Mafundisho: Miti Mikubwa**
Mti wa mopani ni mfano wa mti mkubwa. Miti hutupatia kivuli kutokana na joto la jua wakati wa mchana na hutukinga kutokana na giza wakati wa usiku. Wakati mti mmoja mkubwa umeoteshwa, ni rahisi kutengeneza msitu mkubwa wa miti ndani ya kijiji ambayo italeta kivuli na kinga kwa kila mmoja.

Biblia mara nyingi huzungumzia watu wa Mungu kuwa miti mikubwa. Watu hawa huleta kivuli na kinga kutokana na shida ya mambo yanayoibuka ndani ya kijiji. Labda mtu wa Mungu anaweza kumsaidia mtu wakati wa giza ambaye hana chakula, kuleta msaada kijijini kwa kuwasaidia wajane, au watoto yatima ukiwajumlisha wale ambao mara nyingi hawajumlishwi. Kikundi chote cha watu ambao ni miti mikubwa wanaweza kuleta mabadiliko makubwa ndani ya vijiji vyao, kwa kuleta kivuli, ukombozi na upendo kwa kila mtu!

Biblia inaenda mbali zaidi na kusema watu wake ni miti mikubwa ya haki. Haki siyo mtu kuonekana kuwa mtu mzuri; inamaanisha kuwa na uhusiano na Mungu na kati ya watu, ukiwahudumia wengine kwa heshima na upendo. Tunaweza kufanya haya kwa sababu tumepokea upendo kwa Mungu na tumepatanishwa naye. Kwa hiyo haki kwa urahisi ni ‘kuwa sawa na Mungu na sawa na watu’.

***Safari*** ni kufanya tofauti ndani ya uzima yako mwenyewe na uzima yaw engine. Dignity ni watu wanaotembea wanaofanya tofauti ndani ya jumuia zao, mahali popote walipo. Tunaamini kuwa watu bora wanaoweza kuleta mabadiliko ndani ya jumuia yako ni WEWE na WATU WALIOKUZUNGUKA.

**Hadithi: Kanisa la Kijiji**
Hadithi hii itakusaidia kufahamu baadhi ya mambo yaliyotokea ndani ya kijiji chako na kwa nini yanatokea. Inatazama jinsi Kanisa lilivyo na jinsi inavyoweza kusaidia au kutosaidia.

**Ikiwa unajifunza pomoja na kikundi:**
Unapo hadithia hadithi hii unaweza kuwachukua watu wa kujitolea kuigiza tabia tofauti. Unaposoma hadithi wanatakiwa kuigiza maeneo tofauti ukiwatia moyo. Wanapoigiza itawasaidia watu kuelewa kinachoendelea na itafurahisha. Fuata hadithi, ukimsisitiza kila mmoja kuigiza sehemu ya mchezo mnapoendelea.

Utawahitaji watu wa kujitolea wenye tabia hizi tofauti:

- Wachungaji Watatu
    - Mchungaji Daka
    - Mchungaji Kenneth
    - Mchungaji Lungu
- Wanakijiji
    - Grace
    - Mutepa na Hope
    - Bright na Masiye
    - John na Bernard
- Mfanyakazi/chama kisicho cha serikali – Rebecca
- Wapandaji wa Makanisa – Mabo na Cheswa
- Mashahidi wa Yehova

Hii ni hadithi ya kijiji, labda kijiji kama chako! Ni kijiji kidogo Kusini Mangaribi mwa Zambia. Watu walifanya kazi kwa bidii na kujaribu kwa kadri walivyoweza lakini kijiji bado kilibaki na matatizo. Yapo makanisa matatu kwenye kijiji.

Kanisa la Anglikana liliongozwa na Mchungaji Daka. Alimaanisha kweli na akajaribu kwa kadri ya alivyoweza. Alifikiri aliitaji watu wengi ndani ya kanisa lake ili aweze kuwa na mafanikio. Alifikiri kanisa ni LAKE na siyo kanisa la Mungu. Anafundisha jumbe zenye kutia moyo na mara nyingine anasema vitu kuwafurahisha watu ili waendelee kubaki hapo kanisani. Katika kila kusanyiko huhesabu watu ni wangapi waliohudhuria!

Kanisa la Babtisti ni sehemu ya dini kubwa, lakini kanisa linapata shida kwa sababu dini inatoa msaada mdogo vijijini. Hii ina maana kuwa Mchungaji Kenneth na kanisa hawana msaada mkubwa. Hakuna mafundisho hakuna Biblia. Mkusanyiko unapata shida kuelewa na hawajui maana ya kuwa Mkristo.

Kanisa la Pentekoste lilongozwa na Mchungaji Lungu, ni muhubiri mzuri na baadhi ya watu wakawa Wakristo ndani ya kanisa. Hawa watu walivutiwa kumfuata Yesu na wakachagua kujiunga na kanisa la Anglicana au Babtisti kwa sababu marafiki wao wlihudhuria huko. Mchungaji Lungu akaumizwa na jambo hilo akakasirika na kutuhumu makanisa mengine kwa kuwaiba watu toka kanisani kwake!

Wako watu wengi, wengi sana ndani ya kijiji wanaopambana! Wengi wana njaa, wanateseka na ukimwi na kupambana na kileo. Grace ni mama mzee kutoka kanisa la Anglikana na Mungu akaugusa moyo wake awafikie watu hao. Akaenda na kuzungumza nao akawa rafiki yao akafahamu shida zao. Kwa uvumilivu mwingi na upendo, baadhi yao walifikia kumfahamu Yesu wakaenda kanisani pamoja naye – jambo la kushangaza! Lakini watu wa makanisa mengine wakaona wivu, maana walihitaji watu wapya ndani ya makanisa pia! Wakaenda kuwasaidia watu wanaoteseka, lakini walikuwa wabinafsi hawakusikiliza shida za hao watu wanaoteseka. Jambo hili likamfanya Grace na Mungu wakagadhibika. Hata viongozi wa kanisa nao wakaingilia na kushindana juu ya kanisa lipi hao watu wataenda!

Kuna watu wengi kijijini wanowapenda wengine, lakini wakati mwingine hawafahamu kamili maana ya kuwa Mkristo. Wanafikiri kwenda kwenye mikutano ya kanisa ndilo jambo la muhimu. Hii ina maana kuwa kuwasaidia watu wenye mahitaji kijijini haina umuhimu, kwa kweli watu hawafikiri kama jambo lenye maana hata kidogo. Kwa mfano, Mupeta anawapuuza watu wenye njaa kwa sababu anawahi kanisani. Hope anajifanya hamwoni mjane mpweke kwa sababu anataka kwenda kwenye mkutano. Inahuzunisha! Hakuna hata mtu mmoja katika hawa anayefahamu au kuwa na ujuzi wa kweli wa kumfahamu Yesu.

Watu wanafikiri kuwa msaada utatoka nje ya kijiji, hivyo siku moja Rebecca, mfanyakazi wa shirika lisilo la kiserikali akfika kijijini akiahidi uzima bora mbeleni! Akaanza mradi na kuanza kuwapa watu vitu bure, vifurushi vya nguo na mikopo. Watu wengi walipendezwa na jambo hilo! Wamama wapya, Bright na Masiye toka kanisa la Babtisti walichukua nguo kwa ajili ya watoto wao, lakini wakachukua nguo na kuuza. Vijana wachache, John na Bernard, toka kanisa la Anglikana na Pentekoste wakachukua mikopo na hawakuwa na uangalifu wakaishia kupoteza fedha zote! Hii iliumiza moyo wa kila mmoja maana walikuwa wanatumaini kuwa msaada kutoka nje ungefanya kijiji sehemu bora lakini ilifanya kuwa mbaya zaidi.

Mabo na Cheswa ni watu wenye shauku wa kuanzisha makanisa wakatoka mjini kwenda kijini. Tena, watu wakafurahia wakidhani pengine mabadiliko yangeweza kutokea wakaenda kuona kinachoendelea. Mabo na Cheswa ni watu wema na wanampenda Yesu lakini ukweli hawajui shida iliyoko kijijini maana wanatoka mjini. Watu wachache walimwamini Yesu wakajiunga na kanisa. Viongozi wengine wa makanisa wakaogopeshwa na kanisa jipya linalokua na hawakupenda jambo hili hata kidogo, walipiga kete na kulalamika na hata siku moja wakaenda kuwakabili!

Kanisa la Mashahidi wa Yehova likaja kijijini. Hakuna mtu aliyetambua mwanzoni; viongozi wa makanisa walijishughulisha na mashindano, wanakijiji wakahuzunika na hali iliyokuwapo kijijini wakapiga kete wao kwa wao. Bado watu wachache wakaanza kujiunga na kanisa la Mashahidi wa Yehova, baadaye wakaongezeka na kuongezeka zaidi! Viongozi wa makanisa na wanakijiji baadaye wakatambua na kugundua kuwa walikuwa kwenye malumbano na kupiga kete badala ya kuwajali watu waliokuwa karibu nao.

?

**Maswali: Kanisa la Kijiji**

- Ndani ya kijiji hiki, unafikiri kweli watu walimfahamu Yesu? Kwa nini?
- Watu wenye njaa na walioadhirika na kileo waliona nini? Unadhani hii Iliwadhuru namna gani?
- Unadhani watu waliotoka nje na kijiji (mfanya kazi wa chama kisicho cha Serikali na Waanzilishi wa Makanisa) walidumu kwa muda mrefu ndani ya kijiji au kufahamu changamoto zilizowakabili watu hapo?
- Kama viongozi wa makanisa wasingejishugulisha na mashindano, wakafanya kazi kwa pamoja, nini kingeweza kutokea badala yake?

Kama viongozi wa makanisa na washirika wangefanya kazi kwa pamoja, watu waliokuwa na njaa wangelishwa, na wale walioadhirika na kileo wangewekwa huru na watu wangeunganika! Hii ingekuwa na nguvu mfano wa upendo wa Yesu na wengi wangekuja kumjua yeye.

Sasa fikiri juu ya kijiji chako mwenyewe:

- Je kuna watu wanaoteseka na njaa kuadhirika na kileo?
- Ni nani anayewaangalia?
- Je watu toka nje wanakuja kwenye kijiji chako kusaidia? Nini hutokea?
- Je makanisa ndani ya kijiji chako hushindana na kutokukubaliana?
- Hii ina adhari gani kwa kijiji chote?



*"Nilipoanza kuongea na watu ndani ya kijiji nilitambua kuwa kweli tunamhitaji Mungu kusaidia kijiji chetu. Wanakijiji waliniambia mabishano waliokuwa nayo, juu ya watu waliotengwa ndani ya jumuia zao nikatambua kuwa kulikuwa na watu wengi hawakuwa na chakula cha kutosha! Sikufahamu jambo hili! Nilidhani kijiji ilikuwa ni sehemu nzuri ya kuishi lakini Mungu alinionyesha kuwa tunaweza kufanya bora zaidi na ametaka kubadilisha mambo!" **- Agnes***



*"Nimegundua kuwa watu wengi kutoka mashirika ya nje yanayokuja kijijini kwetu kusaidia, lakini mara nyingi ilifanya mambo kuwa mabaya zaidi. Watu wanakuwa walafi na kuchukua*

*vitu na kuwa wabinafsi. Nilidhani Dignity ni shirika linalofanana na hayo lakini kwa ukweli walinionyesha kuwa wana kijiji wanaweza kufanya mabadiliko wenyewe. Watu wengi ndani ya kijiji chetu wanafikiri kuwa hawawezi kufanya tofauti yeyote, lakini kwa msaada wa Mungu wanaweza kujisaidia wenyewe na kuwasaidia wengine!" - **Asisi***

**Mafundisho: Nini kinachoweza kutokea badala yake?**

Kuanzisha kanisa lingine ndani ya kijiji katika hadithi yetu haiwezi kutatua matatizo. Jinsi tulivyoona, kanisa lingine linaweza kuanzisha mashindano na haiwezi kabisa kusaidia kuunganisha watu ndani ya kijiji. Waza kama kitu cha tofauti kikitokea hii ikamaanisha makanisa kuwa pamoja, inamaanisha kanisa linahusika katika jumuia na kuwaruhusu watu kumjua Yesu, kuwasaidia watu kwa matendo.

**Itakuwaje jambo hili likitokea kijijini kwako?**

Itakuwaje ukikusanya kikundi kidogo kutoka kwenye kijiji pamoja? Unaweza kuwakaribisha watu toka makanisa tofauti, kuwa mwangalifu kukutana muda ambo haitawazuia kuhudhuria ibada zao za kawaida. Mnaweza kuanza kukutana na kujifunza pamoja, kuomba pamoja na kuonyesha kuwa kila mtu anakaribishwa. Unaweza kuwakaribisha watu wenye upungufu wa chakula, wenye huzuni na hao walioadhiriwa na kileo wawe sehemu ya kikundi. Kwa pamoja mnaweza kuanza kutoa sadaka kusaidia watu ndani ya kijiji. Hii ni hali nzuri kwa sababu kila mmoja ameanza kushiriki upendo wa Yesu!

Kwa kuanza, baadhi ya viongozi wa kanisa wanaweza kupinga, lakini kila mara mkikutana baadaye wataelewa kuwa kikundi hiki si cha mfumo wa kanisa la kawaida, lakini inamaanisha kusaidia kanisa kwa mapana na kusaidia kijiji. Muda utakavyoendelea kanisa litatiwa moyo na kuimarishwa watakapoona upendo wa Yesu ukishirikishwa kupitia kikundi.

Badala ya kuchanganyikiwa tunakuwa na umoja, badala ya kubishana tunafanya kazi kwa pamoja. Huo ndio mwanzo wa kubadilisha kijiji. Pamoja na Yesu tunafanya kazi pamoja na WEWE unaweza kuwa sehemu ya kazi yenyewe!

Huo ndiyo mwanzo wa kuwa **Miti Mikubwa ndani ya Kijiji chako!**

"*Watu wengi ndani ya kijiji chetu hawadhani kuwa kijiji kinaweza kubadilika. Wafanyakazi wa misaada na waanzilishi wa makanisa watajaribu kuleta mabadiliko ndani ya kijiji lakini hawatujui na hawajui shida zetu na hawakai muda mrefu wa kutosha kutambua mahitaji yetu. Wanakijiji wanapaswa kuamini kuwa wanaweza kufanya mabadiliko kwa familia zao, jumuia na vijijini na kufanya kazi pamoja na kusaidiana. Haya yanaweza kutokea ikiwa watu wataishi uzima yao kwa ajili ya Yesu. Hapo wanakijiji watabadilika kwa ubora!" **– Agnes***

**Vifungu vya Biblia**


Sura mbili za Biblia zinazofuata inazungumzia kweli ya Mungu na jinsi inavyofanya kazi ndani ya kijiji chetu na kuleta uzima kwa kila mmoja. Mstari wa kwanza inatoka katika barua ambayo Mtume Paulo aliwaandikia waumini waliokuwa Roma. Ya pili ni mkusanyiko wa mistari inatoka kwa mtu mkongwe wa Mungu Isaya.

*Kwa maana siionei haya Injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza, na kwa Myunani pia.*

*Warumi 1:16*

*[1]Roho ya Bwana MUNGU i juu yangu;*
*kwa sababu BWANA amenitia mafuta*
*niwahubiri wanyenyekevu habari njema;*
*amenituma ili kuwaganga waliovunjika moyo,*
*kuwatangazia mateka uhuru wao,*
*na hao waliofungwa habari za kufunguliwa kwao.*
*[2]Kutangaza mwaka wa BWANA uliokubaliwa,*
*na siku ya kisasi cha Mungu wetu;*
*kuwafariji wote waliao;*
*[3]kuwaagizia hao waliao katika Sayuni,*
*wapewe taji ya maua badala ya majivu,*
*mafuta ya furaha badala ya maombolezo,*
*vazi la sifa badala ya roho nzito;*
*wapate kuitwa miti ya haki,*
*iliyopandwa na BWANA, ili atukuzwe.*
*[4]Nao watajenga mahali pa kale palipoharibiwa,*
*watapainua mahali palipokuwa ukiwa zamani,*
*watatengeneza miji iliyoharibiwa,*
*mahali palipoachwa kizazi baada ya kizazi.*

*Isaya 61:1-4*



**Shughuli: Isaya 61:1-4**
Mistari katika kitabu cha Warumi inatuambia kuwa injili, kweli ya Yesu Kristo, ni nguvu ya Mungu ya wokovu kwa kila mtu. Mistari kwenye kitabu cha Isaya inatuambia kuwa injili siyo kwa watu binafsi tu bali inarejeza vitu vyote. Isaya anatuonyesha kuwa Mungu anataka kujenga miji ya kale iliyoharibiwa, hii ina maana anataka kutujenga sisi, vijiji vyetu na dunia. Anafanya hivyo kwa kupanda miti mikubwa (watu wake) ili atukuzwe na kutoa kivuli, usalama na msaada kwa kila mtu aliyewazunguka.

Mistari kwenye kitabu cha Isaya itatusaidia kufahamu haya. Yesu mwenyewe alizitumia katika kitabu cha Luka 4 alipozungumzia yale ambayo Masihi (Hili ni neno la Kiebrania kwa Mwokozi) alikuja kufanya. Alikuwa anajizungumzia! Kwa hiyo maandiko haya yanasema nini? (Kumbuka kuandika majibu yako kwenye kitabu chako cha kumbukumbu)

- Angalia kitabu cha Isaya 61:1-4 na uandike chini matendo yote yanayoweka watu huru kiroho (kwa mfano, watapewa roho ya sifa)
- Andika chini mambo yanayowaweka watu huru kihisia na kimwili (kwa mfano, kuwafariji wenye huzuni)

Mara nyingi tunafikiri kuwa kuna kitu kimepungua kwenye uzima yetu, kijijini au kwenye jumuia. Kwa sehemu inaonekana kuwa kweli, lakini kuna kitu kimepungua. Tunaweza kusema kuwa uzima yetu au kijiji chetu siyo 'yote' – ujuzi wa kujua kuwa kuna kitu kimepungua. Angalia tena Isaya 61:1-4.

- Katika kifungu hiki ni tendo gani inayojali mtu mzima?
- Katika kifungu hiki ni tendo gani linaloonyesha jumuia nzima?

Kusudi la Mungu ni kurejesha vitu vyote. Mahali dhambi (watu wanaoishi mbali na Mungu na njia zake) imeharibu dunia yetu na uzima yetu, anataka kutufanya sisi na dunia wakamilifu tena, kutuwezesha kuishi uzima ya umilele (milele mbinguni pamoja naye). Mungu anatutaka sisi kujenga yale yaliyobomolewa ya kale na kufanya upya miji iliyobomoka. Tukifanya haya kwenye vijiji vyetu, anataka kuvifanya vijiji vyetu kuwa kamili na katika hali nzuri. Hilo ndilo kusudi! Injili itafanya miji yetu kuwa kamili.

Mungu anafanyaje mambo haya? Anafanya haya kupitia 'miti ya Haki' (tazama mstari wa 3). Miti ya Haki ni miti mikubwa. Katika kifungu hiki ni picha ya watu wanaofananishwa na miti mikubwa kwa ajili ya Mungu katika kijiji. Hawa ni watu wanaotoa hifadhi, matunda na kivuli kwa kila mtu. Ndani ya maneno ya kifungu, sifa za Mungu huonekana ndani yao, hili ni pando la Mungu mwenyewe. Tunaweza kuwa kama miti mikubwa ndani ya kijiji chetu na tunaweza kuwasaidia wengine kuwa miti mikubwa katika vijiji vyao.

Injili, kweli ya Mungu na Mungu kuingia ndani ya vijiiji vyetu hutegemea miti mikubwa ya haki. Inawategemea watu wake na kukubali kwao kuwa pando la Bwana.

**Ikiwa unajifunza pomoja na kikundi**
Mwambie kila mtu aandike chini majibu ya maswali kwenye shughuli hii, halafu kila mtu ashirikishe majibu yao na wenzao ili watu waweze kusikia majibu kwa yale ambayo waliokosea.

Watu wengine watahitaji msaada wa ziada au muda zaidi kwa mazoezi haya.
Kama watashindana kupata majibu, watie moyo kusoma kifungu kwa uangalifu tena na usikilize majibu ya watu wengine.

**Mafundisho: Mti wa Banyani na Ndizi – Sisi tu miti ya aina gani?**
Mti wa banyani huzingira eneo lote. Inazungusha mizizi yake kwenye mti uliopo na kukua kuuzunguka na 'kuunyonga' mti wa asili uliokuwepo. Mti wa banyani huweka mizizi imara na kumiliki eneo. Kuna msemo "hakuna kitu kinachoweza kukua chini ya mti wa banyani". Hakuna kabisa! Lo! Kila kitu kinakufa kwa sababu mti wa banyani humiliki. Hapa kuna picha ya mmoja, unaweza kuona mizizi mingi iliyounguka mti wa asili.



**Maswali: Mti wa Banyani na Ndizi – Sisi tu miti ya aina gani?**

- Je unafahamu mche wa Ndizi unavyokuwa?
- Ina tofauti gani na mti wa Banyani?

Mche wa ndizi ni tofauti. Wakati mche unapokuwa na kuzaa matunda, pia inazalisha mbegu ya ‘miche midogo’ pembeni ya mche mkubwa. Baadaye, mche mkubwa unapozalisha ndizi hufa na kwa kufanya hivyo, inatoa nafasi kwa mbegu ya ‘miche midogo’ inayozunguka. Kinachoanza kama mche mmoja wa ndizi haraka miche mingine huzalishwa na kila mche huzalisha ndizi na kuhamisha uhai kwa miche midogo inayokuwa kuuzunguka. Kila mche wa ndizi unaendelea kujifia wenyewe.



Hivyo hii miti ni ya aina gani? Miti wa aina yeyote unaoufanania huonyesha kama utamtumikia Mungu ndani ya kijiji chako.

Watu wengi wanafanana na mti wa banyani, wakijikuza kuwa wakubwa na wenye nguvu. Hii ina maana watu wengine hawawezi kuwa na harufu nzuri wanapowazunguka. Watu wengine wanafanana na miche ya ndizi. Wanatumia uzima yao, muda wao na mali zao kuwapa wengine na kuwapa uhai hao wanao wazunguka.

Lengo la uzima ya Kikristo siyo kujitajirisha mwenyewe, ni kumwabudu Mungu na kuwatumikia wengine. Tunapofanya hivi tunapata kusudi la Mungu uzimani mwetu. Tukirudi nyuma kutazama kifungu katika kitabu cha Isaya 61:1-4, kila kilichokuweko kwenye mistari miwili ya kwanza ni kufanya kama Mwokozi, Yesu, angefanya na kuleta mabadiliko. Kwenye mstari 3 ghafla inasema 'wao' ambao watakuwa pando la Bwana, siyo sisi. Lengo letu ni kuwafanya wengine kukua. Tumeitwa kuwa kama mche wa ndizi, kutoa uzima kwa wengine na kuwafanya kukua kuwa miti mikubwa.

**Mafundisho: Vikundi vya Uzima – Hii Inafanyaje Kazi kwenye Kijiji**
Unakumbuka hadithi ya kijiji?

Watu, ambao ni kama miti mikubwa ya haki, wakisimama imara kwa pamoja, wanaweza kuleta tofauti kubwa katika kijiji kama hicho. Wanaweza kufanya tofauti katika kijiji chako pia!

Kila mtu kwenye kijiji anaweza kuwa bora kuwepo kwenye kikundi cha Kikristo wanaojifunza juu ya Yesu,  wenye hisia waliojitoa kwenye kijiji chao, kuwa kama miti mikubwa ya haki.

Dignity inaiita vikundi hivi vya watu Vikundi vya Uzima. Ni vyombo imara yenye nguvu ambayo Mungu atavitumia kufanya kazi ndani ya kijiji chako. Kuna vitu ambavyo ni vya muhimu juu ya vikundi hivi:

- Hawafungamani na dini yeyote.
- Hawako mahali mchungaji anapohubiri, wako mahali ambapo watu wanajifunza kwa pamoja.
- Wako kwa ajili ya jumuia yote, kila mtu anakaribishwa.
- Haikumaanishwa kuwa ni kwa kanisa letu tu (ingawa wakati mwingine mafundisho hutumika makanisani).
- Wananajitoa wenyewe kumpenda Mungu na kupenda majirani.
- Wanatafuta njia ya kuwatumikia na kuwapenda hao wenye mahitaji ndani ya jumuia yao.
- Wanamwonyesha Yesu kwa kila mtu.

**Kikundi cha Uzima Hadithi**
Vikundi vya Uzima Vingi vimeanzishwa Tanzania. Changamoto kubwa inayokabiliana nayo ndani ya jumuia zao ni kwamba watu wengi ni watu wa dini, lakini siyo wakiroho. Hii ina maana watu wanahudhuria kanisani na kujaribu kufuata taratibu, lakini mara zote hushindana. Mara zote imani yao siyo ya matendo chanya au upendo wenye mguso kwa watu wanaowazunguka.

Wakati Kikundi cha Uzima vilipoanza, wanachama wengi kwenye jumuia walikuwa na mashaka wakidhani kuwa walikuwa wanaanzisha makanisa mapya au dini mpya hivyo hawakutaka kujihusisha. Muda ulipoendelea, watu walikuja kutambua kuwa waliweka mizizi yao kwa Yesu na

kuchukua muda kuzidi kumjua Yesu. Mashaka yalianza kwisha na wanajumuia wakawakubali kuwepo. Hii ilitokea kwenye jumuia nyingi.

Misozi* amekuwa akihudhuria Kikundi cha Uzima kwa miezi 3 tu na tayari amekwisha ona badiliko kwenye uzima yake mwenywe:

> *"Kuna mabadiliko mengi ndani yangu tokea nijiunge kwenye Kikundi cha Uzima. Najisikia kama vile nimewekwa huru maana vitu vingi ambavyo ilkuwa sivielewi, sasa navielwa!"*

Viongozi wa Vikundi vya Uzima wanatumaini kuwa neno la Mungu litaenea mbali na kwa mapana. Wanatumaini kuwa kwa muunganiko wa vikundi vyao mwishowe itaidhibitishia jumuia yao kuwa hawajaribu kuanzisha dini mpya au kutafuta pesa kwao, lakini ni kuwapenda wao kwa jina la Yesu. Wanatumaini kuwa Vikundi vya Uzima vitakuwa na adhari kubwa na kuweza kumsaidia kila mmoja kujitolea zaidi kwenye jumia zao, kuleta kwa pamoja dini tofauti na umoja kwenye makanisa.

Huu ni mfano wa Kikundi cha Uzima ikitenda kazi kama miti mikubwa kwenye kijiji, mtu kuwa kama mti mkubwa na kikundi kuwa na adhari ndani ya jumuia nzima!

**Jina limebadilishwa kutunza siri za ndani*

**Omba**
Waombee watu wanaoteseka ndani ya kijiji chako (labda wanaoteseka kwa njaa au kudhurika na kileo) ili wawe na matumaini kuwa Mungu anaweza kubadilisha mtiririko wa tabia ambayo imewafunga wao na wengine gerezani kwa vizazi.

Waombee Wkristo ndani ya kijiji chako ili Roho Mtakatifu awape maono kwa kijiji chao na kwa uvumilivu watamani kufanya kazi ya Mungu. Mwombe Mungu awasaidie kukua na kuwa miti mikubwa ya haki, ndani ya kijiji chako.

**Kufanya Wiki Hii: Anza kwa kuifahamu kijiji chako**
La kwanza, chukua muda kufikiri na kuyaombea maswali haya, ukiandika chini mawazo yako kwenye kitabu chako cha kumbukumbu:

- Mungu anakuita kufanya nini?
- Unafikiri Mungu anakuuliza kuwa mti mkubwa na kusaidia wengine wawe miti mikubwa pia?
- Umekuwa kama mti wa mche wa ndizi au mti wa banyani mpaka sasa?
- Uko tayari kuwa mti wa mche wa ndizi unaotoa uhai wake kusaidia wengine kukua?
- Je Mungu anakuambia uanzishe Kikundi cha Uzima? Je ungependa kuitikia wito wake?

Kazi ya wiki hii ni kuanza kufikiri hali iliyoko ndani ya kijiji chako. Hii ina maana kuwa uzungumze na baadhi ya wanakijiji juu ya ujuzi wao wa kuishi ndani ya kijiji, wanaona nini rahisi au kigumu kuishi kijijini, wameona kanisa likisaidia kijiji namna gani. Washirikishe vifungu vya Biblia kutoka katika somo na waulize wanafikiri nini juu ya Mungu akitumia watu wake kama miti mikubwa ndani ya kijiji chako.

Tembea ukiomba ukizungukia kijiji chako. Maombi ya kutembea ni pale tunapokusudia kutembea kuongea na Mungu na kuombea watu na maeneo unayoyapitia. Unapotembea ndani kijiji chako

mwombe Mungu akuonyeshe watu anaotaka kuwakuza kuwa miti mikubwa, watu wasiokuwa na mahusiano mazuri na kwa nini, na watu wanaoteseka. Kama ukigundua hali, mtu au kikundi cha watu wakati unapotembea inawezekana Mungu anazungumza na wewe kwa yale anayoyaona. Muulize Mungu namna anavyotaka usaidie.

**Andika Chini**

- Wanakijiji walisema nini juu ya ujuzi wao wa kuishi kijijini?
- Walipokeaje ulipowashirikisha vifungu vya Biblia na jinsi Mungu anavyo tumia watu wake kama miti mikubwa? Je walikubali? Je walikataa? Walitiwa moyo? Je wao nao walitaka kuwa miti mikubwa ya Mungu?
- Uligundua nini juu ya maombi ya kutembea ukiomba ukizunguka? Labda umekutana na mtu hukuwa unamfahamu kabla au kuona wanakijiji wakisaidiana.
- Unafikiri Mungu anakutaka vipi uwasaidie watu hawa na hali ndani ya kijiji?

**Shughuli ya ziada**

Shughuli hizi za ziada zitakusaidia wewe kufikiri yale uliyojifunza, na kayaingiza kwenye mazoezi na kupanua uwelewa wako. Hupaswi kufanya shughuli zote za ziada lakini tunakutia moyo ufanye moja au mbili. Unaweza kuchagua moja unayoona itakusaidia au unayofurahia zaidi!

**Uchaguzi 1:** Nenda tafuta mti wa mche wa ndizi, je unaweza kuona miche midogo ikiota au mgomba ukifa. Andika ama chora unachokiona hapa chini. Andika au chora unachoona kwenye daftari yako.

**Uchaguzi 2:** Panda mti wa mche wa ndizi ili uweze kuona ukikua kwa miezi inayokuja. Andika chini yale utakayoyaona baada ya miezi kadhaa.

**Uchaguzi 3:** Kutana na baadhi ya marafiki toka makanisa tofauti. Unaweza ukawauliza:

- Nini ngumu au rahisi unapokuwa ndani ya kanisa?
- Waeleze hadithi ya makanisa yakipigana na waulize kama kanisa kwenye jumuia yako linafanania?
- Wamelionaje kanisa likisaidia jumuia pana?
- Nini inarudisha kanisa nyuma kwenye jumuia?
- Je kanisa linakuwa? Kwa nini wanafikiri hili linatokea?
- Shiriki vifungu vya Biblia pamoja nao kutoka kwenye somo na waulize wanafikiri nini na unawezaje kuwa mti mkubwa wa Mungu.

Andaa kumbukumbu toka kwenye majadiliano yako ndani ya kitabu chako cha kumbukumbu.

**Uchaguzi 4:** Tafuta mti mkubwa kwenye kijiji chako na ukae chini yake kwa dakika 20. Fikiri jinsi mti ulivyo mkubwa, jinsi inavyokupa hifadhi kutokana na jua au mvua. Angalia uone kama kuna ndege ama mnyama yeyote aliyeufanya mti nyumba yao ya salama. Mwombe Mungu azungumze na wewe na kukusaidia uwaze wewe, na wengine ndani ya jumuia yako, tunaweza kuwa miti mikubwa kuleta usalama na uzima kwenye jumuia pana. Andika kumbukumbu ya mawazo yako na yale ambayo Mungu anazungumza na wewe hapo chini. Andaa na kuandika mawazo yako na yale ambayo Mungu anasema kwenye daftari yako.

# 2



# Safari ya Dignity

‘Tazama, naweka katika Sayuni
jiwe kuu la pembeni, teule,
lenye heshima, na kila
amwaminiye hatatahayarika.’
1 Petro 2:6

**Lengo**
Unaweza kuwa sehemu ya safari Dignity! Somo hili litakusaidia kufahamu yale ambayo Mungu anakuambia nini kuhusu kijiji chako kwa kutumia Waefeso 2:19-22.

**Mwisho wa somo hili utakuwa na:**

- Fahamu jinsi Dignity ilivyoanza na namna gani unaweza kuwa sehemu ya safari ya Dignity
- Upate hamasa ya kuanzisha jambo jipya kijijini kwako
- Fahamu umuhimu wa kila mtu katika kijiji chako na umuhimu wa kufanya kazi kwa pamoja

**Tazama Nyuma**
Kila mwanzo wa kila somo tunataka kukutia moyo utazame nyuma kwenye somo lililopita na ufikiri yale uliyoyafanya na yale ambayo Mungu amekufundisha.

- Ulijifunza nini kwenye somo lililopita kuhusu miti mikubwa ya Mungu?
- Je ulifanya maombi ya kutembea ukiomba ukizunguka wiki hii? Umeona nini? Mungu alisema nini?
- Je umemshuhudia mtu yeyote yale uliyoyajifunza wiki hii?

**Hadithi: Safari ya Dignity**
Kukusaidia wewe kufahamu namna miti mikubwa ya Mungu inavyoweza kufanya tofauti kwenye kijiji chako, tunataka kukujulisha juu ya safari ya Dignity.

Jon, mtu kutoka Uingereza, amekuwa akifanya kazi na Wakristo Uingereza na Africa kwa miaka mingi. Mwaka 2004, alianza kuona kuwa jinsi kanisa linavyofanya kazi haileti tofauti yeyote. Alichanganyikiwa kuona viongozi wa makanisa wakifundishwa na kuwa na mawazo mazuri, lakini bado ambacho kingetokea. Jon aliomba kwamba Mungu amwonyeshe njia nyingine ya kufanya mambo, na Mungu akampa Jon kifungu hiki:

*Wapate kuitwa miti ya haki,*
*iliyopandwa na BWANA,*
*ili atukuzwe.*
*Isaya 61:3b*

Je unakumbuka kifungu hiki toka somo la mwisho?

Swali ambalo Jon alimwuliza Mungu ni: *'Unamfanyaje kila mtu mti mkubwa wenye wenye kutangaza sifa za Bwana?'*

Jon alielewa kuwa Mungu amewaweka watu kila mahali na kila kijiji tayari na walihitaji msaada ili waweze kukua, kumfuata Mungu na kuchukua yale ambayo Mungu anayo kwa ajili yao. Wanaume na wanawake wangeweza kubadilisha dunia yao na zaidi. Badala ya kuanza na viongozi, hii ina maana kuanza na watu **wa kawaida**, kama mimi na wewe!

Mwaka 2007, Jon alitembelea sehemu ya vijiji vya Zambia na kusikiliza hadithi za watu pale. Walikuwa na hadithi za kustaajabisha! Watu walifufuliwa, waliponywa na watu wengi wakawa Wakristo. Walisafiri kwenye maeneo ya vijiji vya Africa na kumwona Mungu akifanya mambo

makubwa. Lakini bado wanajiona kuvunjika moyo na kukata tama. Sababu ni kwamba hakuna walichokifanya kikadumu.

Kwa hiyo mwaka 2008 Jon alikusanya watu wachache kuomba na kufikiri juu ya swali, *'Tutamfanyaje kila mtu mti mkubwa wenye kutangaza sifa za Bwana utakaodumu?'* Walikutana na baadhi watu maeneo ya Ukanda wa Shaba Nyekundu ya Zambia na kwa pamoja wakajadiliana namna ya kuanzisha Vikundi vitano vya Uzima ndani ya vijiji vyao. Vikundi hivi vilikutana ndani ya makanisa ya matope, mashuleni na hata chini ya miti!

Baada ya mwaka 1 tayari kulikuwa na Vikundi 10 vya Uzima yenye watu 200 walioshiriki.
Baada ya miaka 10 kulikuwa na Vikundi 700 yenye watu 14,000 walioshiriki!

Vikundi hivvi vya Uzima vinaendelea kuongezeka na mpya zingine zimeendelea kuanzishwa.
Hebu waza zitakuwepo vingapi baada ya miaka 10 zingine?

Waza kama kulikuwepo na Kikundi cha Uzima inayofanya tofauti ndani ya kijiji chako? Na baadaye Vikundi vya Uzima vingi vikawepo ndani ya kijiji chako? Halafu Vikundi vya Uzima vikaanzishwa kwenye vijiji jirani kwa sababu tayari wamesikia yale yanayotendeka.

Jon amekuwepo kwenye safari ya kuona Vikundi vya Uzima vingi vikianzishwa, lakini sababu ya kweli haya yamefanyika ni kwa sababu ya Mungu na sababu ya nguvu ya watu wa kawaida wakifanya vitu vya ziada kwa ajili ya Yesu. Hawa watu wa kawaida ndani ya vijiji kuzunguka jangwa-Sahara Africa ni **miti mikubwa ya Mungu!**

Safari ya Dignity bado inaandikwa na unaweza kuwa sehemu yake. Je ungependa kuwa sehemu ya yale Mungu anayoyafanya kwenye kijiji chako na zaidi? Unaweza kufanyika mti mkubwa na kuwasaidia wengine kukua na kufikia miti mikubwa pia.

Jon alikuwa mti mkubwa aliyejaribu kufanya yale ambayo Mungu alimwambia kufanya. Ikatokea watu aliokutana nao wakawa kama yeye, walijaribu kufanya yale ambayo Mungu aliwaambia. Historia ya Dignity bado inaendelea kuandikwa na watu zaidi na zaidi wakifanya yale ambayo Mungu anayowaagiza kufanya.

Huhitaji kuwa kiongozi. Wala huhitaji mafundisho mengi. Wala kuwa na fedha nyingi. Mungu anaweza kumtumia kila mtu na mtu yeyote – hata wewe anaweza kukutumia!

**Kikundi cha Uzima Hadithi**
Soma yale ambayo Precious, Esther na John walichosema kuhusu Vikundi vya Uzima ndani ya vijiji vyao.

**Precious**: *"Nilizaliwa nikawa mtu mbaya. Nilifanya vitu vibaya nikafikiri labda sitaweza kuwepo kwenye mipango ya Dignity. Lakini sasa namwomba Mungu na amekwisha kunibadilisha. Sasa, mimi ni mwalimu na nawafundisha watu wengine. Naona kuwa watu wanafurahia Vikundi vya Uzima kwa sababu wanajisikia kuaminiwa na kazi na kupewa wajibu. Wako kama wanajeshi wanaosubiri."*

**Esther**: *"Dignity imeleta upendo ndani ya vijiji na watu waliozunguka. Inawafundisha watu kupendana, na kusaidiana."*

**John**: *"Ujumbe wa Dignity ulinishawishi nikawa sehemu ya kutatua matatizo ndani ya vijiji. Inayo nguvu ya kubadilisha watu."*

**Vifungu vya Biblia: Mawe Yaliyo Hai**

Tunapozungumza juu ya miti mikubwa ya Mungu itasaidia kumzungumzia mtu anapokuwa mzuri, mti wenye afya unaozaa matunda mengi. Inato kivuli kwa wengine (wanawapenda wengine ma kuwasaidia kwenye imani yao) na wanazaa matunda (ni wakarimu, wenye furaha na kuishi kwa amani na watu wote). Hata hivyo, mara zingine miti husimama zenyewe. Hatutaki mti mmoja mkubwa kusimama peke yake ndani ya kijiji, tunataka kila mmoja ampende Yesu, kupenda wengine na kuleta tofauti!

Kwa hiyo kwenye somo hili tutaenda kutumia picha tofauti kutusaidia. Tutamzungumzia mtu moja moja ndani ya kijiji chako kama jiwe. Kuna mawe mengi ndani n kuzunguka kijiji. Kuna watu wengi ndani ya kijiji chako.

Waza kama kila mtu kijijini kwako ni jiwe. Kila jiwe Kila jiwe lina shepu tofauti, saizi tofauti na rangi tofauti. Jiwe moja linaonekana kuwa haliwezi kuleta badiliko lenyewe, linaweza tu kwa wepesi kutupwa. Lakini Mungu amekuambia ukusanye hayo mawe yote ya dhamani na uyaweke pamoja. Ukiyaweka mawe pamoja yanaweza kujenga ukuta imara, yanaweza kuungwa kamili na kujenga kitu ambacho ni kizuri na imara zaidi ya jiwe moja linalosimama lenyewe.

> 4*Mmwendee yeye, jiwe lililo hai, lililokataliwa na wanadamu, bali kwa Mungu ni teule, lenye*
> *heshima.* 5*Ninyi nanyi, kama mawe yaliyo hai, mmejengwa mwe nyumba ya Roho, ukuhani*
> *mtakatifu, mtoe dhabihu za roho, zinazokubaliwa na Mungu, kwa njia ya Yesu Kristo.* 6*Kwa*
> *kuwa imeandikwa katika maandiko*
>
> *Tazama, naweka katika Sayuni jiwe kuu la pembeni, teule, lenye heshima,*
> *Na kila amwaminiye hatatahayarika.*
> 7*Basi, heshima hii ni kwenu ninyi mnaoamini. Bali kwao wasioamini,*
>
> *Jiwe walilolikataa waashi,*
> *Limekuwa jiwe kuu la pembeni.*
>
> 8*Tena, jiwe la kujikwaza mguu, na mwamba wa kuangusha.*
>
> *Kwa maana hujikwaza kwa neno lile, wasiliamini, nao waliwekwa kusudi wapate hayo.* 9*Bali*
> *ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate*
> *kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu;*
> 10*ninyi mliokuwa kwanza si taifa, bali sasa ni taifa la Mungu; mliokuwa hamkupata rehema,*
> *bali sasa mmepata rehema.*
>
> *1 Petro 2:4-10*

> 19*Basi tangu sasa ninyi si wageni wala wapitaji, bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu,*
> *watu wa nyumbani mwake Mungu.* 20*Mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii,*
> *naye Kristo Yesu mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni.* 21*Katika yeye jengo lote*
> *linaungamanishwa vema na kukua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana.* 22*Katika yeye*
> *ninyi nanyi mnajengwa pamoja kuwa maskani ya Mungu katika Roho.*
>
> *Waefeso 2:19-22*

**Mafundisho: Mawe Yaliyo Hai**
Uliwahi kujenga ukuta au nyumba? Mawe ya kwanza yanayoanza kuwekwa chini yanakuwa ni ya muhimu sana kwa sababu jingo lote linasimama juu yake. Ni lazima yawe imara na salama.

Katika kitabu cha 1 Petro 2:4-10 kinasema Yesu ni 'jiwe lililo hai' na kila mmoja wetu kuwa 'mawe yaliyo hai.' Yesu ndiye msingi wa jengo la Mungu nasi ni mawe yaliyo hai tunaoweka imani yetu kwake na kuweka uzima yetu msingi wa Yesu.

Katika kitabu cha Waefeso 2:19-22 inamtaja Yesu kuwa ni jiwe kuu la pembeni. Ni jiwe lililo imara na tunajenga uzima yetu juu yake, ni msingi usiyotingishika.

Baadhi ya watu watamkataa Yesu kama jiwe lililo hai na kujenga uzima yao kwa njia zao wenyewe. Bado tunawapenda watu hao na kuwasaidia kufahamu kuwa kujenga uzima yao juu ya Yesu ni njia bora ya kufuata!

Kwetu sisi tunaoamini, sisi kama mawe yaliyo hai tunaweza kujenga kitu kizuri na Yesu! Kifungu toka katika kitabu cha Petro 1 inamzungumzia Mungu kuwa mjenzi mkuu, tukijengwa katika nyumba ya kiroho yenye kumpendeza Mungu. Mungu anatuunganisha pamoja kuwa watu wake, amelichagua kila jiwe kwa makini (huyo ni wewe na watu ndani ya kijiji chako) na kuwaunganisha kwa pamoja kamili. Jengo hili linakuwa mahali Roho Mtakatifu anakaa; Mungu anaishi ndani na kupitia watu wake. Mungu analiona kila jiwe kuwa la dhamani, na anatutaka sote tuunganike na kufanya kazi pamoja kuwa imara na kujenga kitu cha ajabu! Hii ndiyo sababu Mungu anasema ni muhimu sana kuungana na kufanya kazi kwa pamoja ndani ya makanisa yetu, ndani ya vijiji vyetu, ndani ya jumuia zetu na katika nchi yetu.

**Maswali: Mawe Yaliyo Hai**
- Uliwahi kujenga kitu chochote au kuangalia kitu kikijengwa? Ikiwa ni, ni nini?
- Ulijisikiaje ulipokuwa ukijenga na ulipomaliza kujenga?
- Vifaa gani vilitumika kujenga?
- Kuna vifaa vyovyote vilivyotumika vilivyokuwa bora zaidi au vyote vilihitajika kukamilisha chombo?

**Mafundisho: Dhamani za Dignity**
Dignity inadumu kuwaleta watu kwa Yesu kupitia jumuia na kwa kufanya hivyo inaondoa umasikini wa aina zote. Hii ni pamoja na umaskini wa kiroho, kiafya, kifedha na wa mazingira.

Vitu vitatu ambavyo ni vya muhimu kwa kazi hii ni:
1. Kupeleleza
2. Watu
3. Kufanya kazi kwa pamoja

**1. Kuchunguza**
Dignity inalenga kusaidia maeneo ambayo kanisa liko katika udhaifu. Tunataka kujenga na kuwapa watu nguvu mijini, maeneo ya vijijini kuanzisha kitu fulani kipya ndani ya jumuia zao na kufanya tofauti kubwa!

Tunaamini kuwa unacho kila unachokihitaji kuanzisha Kikundi cha Uzima na kufanya adhari kwenye kijiji chako. Tayari unayo mahusiano na mawasiliano ndani ya kijiji chako.  Tunajua una

moyo wa kumfuata Mungu na kupenda wengine kwa sababu unasoma kozi hii. Unayo Mungu upande wako ambaye atakusaidia!

Tunafikiri umetumia akili njema kuchukua hatua hii ya imani kujifunza kitabu hiki, na unataka kujifunza na una moyo wa kufanya mabadiliko kwenye jumuia yako. Unacho kila unachokihitaji, tunataka tu kukusaidia, siyo kukufanyia kazi yote, bali kukusaidia kwa kukufundisha ili ufanye mwenyewe na kuwafundisha wengine. Zaidi ya yote, unakifahamu kijiji chako zaidi! Unaenda kuanzisha kitu chenye uwezo wa kukua na kudumu kwa muda mrefu sana, sana ikigusa kijiji chako chote na zaidi.

**Kikundi cha Uzima Hadithi**
Samwel* anaishi Ganze, Kenya. Alianzisha vitu vingi vizuri ndani ya kijiji chake na kwa vijiji vya karibu, Ameanzisha Vikundi vya Uzima, tukamuuliza ni kwa nini na anafanyaje!

Samwel akaeleza kuwa katika eneo la Ganze misikiti mingi ilijengwa na idadi ya watu walianza kuhudhuria msikitini badala ya kanisani. Jambo hili lilimtatiza Samwel. Anaamini kuwa kuna nafasi ya dirisha kutenda kabla Uislamu kuenea eneo kubwa la jumuia.

Samwel alianzisha Kikundi cha Uzima karibu na nyumbani kwake mwaka 2018 na alitiwa moyo kuona kuwa rafiki ambaye tayari hivi karibu alianza kuhudhuria msikitini alifika kutaka kufahamu yale ambayo Biblia inasema. Mtu huyo kuanzia hapo alianza kumfuata Yesu na amerudi kanisani, na kuhudhuria Kikundi cha Uzima. Jambo hili lilimwonyesha Samwel kuwa Vikundi vya Uzima zana nzuri kutumika kusaidia watu kuelewa na kufahamu maana ya kumfuata Yesu na anafikiri hii inahitajika sana ndani ya jumuia.

Kuanzia hapo Samwel alianzisha mbinu yake ya kuanzisha Vikundi vya Uzima. Kikundi chake cha kwanza kilipoanza na kuimarika alihakikisha kuwa mtu mwingine kwenye kikundi angeendelea kuongoza. Yeye na kikundi cha watu wengine toka kwenye kikundi chake waliongea na marafiki toka jumuia ya jirani na wakakubali kwenda kuwasaidia kuanzisha Kikundi cha Uzima. Kwa pamoja walienda kila wiki kukutana na kikundi hicho kipya mpaka walipokuwa na uhakika kuwa kikundi hicho kingeweza kujiendesha chenyewe.

Samwel na marafiki zake wakaenda kwenye jumuia nyingine na kufanya utaratibu tena! Anayo idadi ya jumuia anazotaka kuanzisha vikundi humo na, kwa kutazama rekodi yake ya nyuma, tunatarajia atavifanikisha!

**Jina limebadilishwa kutunza siri za ndani*

**Maswali: Hadithi ya Samwel**

- Samwel alifanya nini ambayo ilikuwa mpya?
- Ni adhari gani Samwel alikuwa nayo kwa kijiji chake na vijiji vya jirani?
- Unafikiri Samwel alikuwa na fedha nyingi, nyumba kubwa au elimu Kubwa kuanzisha Kikundi cha Uzima? Alitumia nini kuanzisha vikundi?
- Unayo nini tayari cha kukusaidia kuanzisha Kikundi cha Uzima?

*"Nimekuwa nikifikiri kuwa nilihitaji mali au vitu vingi ili kuweza kufanya mabadiliko kwenye kijiji changu. Nilidhani sikuwa na chochote cha dhamani ambacho kingefanya tofauti. Nilipowaza kuanzisha Kikundi cha Uzima niltambua kuwa vitu vya dhamani ni marafiki pamoja na watu na kuifahamu hali ndani ya jumuia yangu. Tayari ninavyo hivyo vtu viwili!"* ***– Mutambo***

**2. Watu**
Watu ni wa muhimu sana. Watu wa kawaida wanafanya mambo makubwa kwa ajili ya Yesu!

Tunaamini kuwa kuna watu katika kila jumuia ambao Mungu amewaweka hapo na anataka kufanya kazi nao. WEWE ndiye mtu huyo! Je unfahamu kuwa Mungu amekuweka kwenye kijiji chako kwa sababu anataka kukutumia kuwa jiwe lililo hai na kukusanya mawe mengine yaliyo hai? Hii inastaajabisha namna gani?

Watu ndiyo hazina ya muhimu ndani ya kijiji chako. Ni mawe yaliyo hai maalum ya kipekee ambayo Mungu anataka kuyatumia.

**Shughuli: Mawe Yaliyo Hai**
Tumezungumzia juu ya kila mtu kuwa jiwe lililo hai. Kila mtu yuko tofauti, na mawe yanaweza kuwa mengi yenye sura tofauti, vipimo na rangi. Chora ukuta wa mawe ndani ya kitabu chako cha kumbukumbu. Waza juu ya watu ndani ya kijiji chako na namna wanavyoweza kuwa mawe yaliyo hai. Andika majina yao chini juu ya kila jiwe ndani ya kitabu chako cha kumbukumbu. Kumbuka kuandika majina ya watu hao ambao watu hawana shughuli nao, Mungu anataka kuwatumia pia!

**Ikiwa unajifunza pomoja na kikundi**
Tafuta mchoro wa ukuta wa mawe kwenye kitabu chako cha kumbukumbu na uwaonyeshe wana kikundi. Wafanye wafikiri juu ya watu ndani ya kijiji na namna yanavyoweza kuwa mawe yaliyo hai. Andika chini majina ya wato hao juu ya kila jiwe juu ya ukuta. Kumbuka kuandika majina ya watu hao ambao hata watu hawana shughuli nao, Mungu anataka kuwatumia pia!

**3. Kufanya kazi kwa Pamoja**
Tunaamini kuwa kuwaleta watu wengi tofauti pamoja kwa njia ya Yesu ndani ya jumuia zao ni msukumo wenye nguvu wa kufanya mabadiliko!

Tunaamini kuwa kinakuwa na nguvu watu wanapofanya kazi pamoja. Hii ina maana kuwa watu walioko makanisani wafanye kazi pamoja. Hii ina maana watu wa makanisa tofauti wafanye kazi pamoja. Hii ina maana watu wasiyoenda kanisani kufanya kazi pamoja na watu wanaoenda kanisani. Hii ina maana hata kuwa vijiji tofauti kufanya kazi pamoja na kusaidiana!

Vikundi vya Uzima ni njia yenye nguvu ya kuleta vijiji pamoja na kufanya kazi pamoja kutajirisha jumuia zao.

Festus amesaidia Vikundi vya Uzima kuanza kwenye vijiji vingi kwenye eneo lao. Alisema, *"Tokea tuanzishe Dignity kwenye maeneo yetu, watu toka makanisa tofauti wameanza kufanya kazi pamoja, kushirikiana. Tulipoanza kushirikiana, watu ambao ilikuwa hawaji kanisani,*

*wasiomfahamu Kristo, sasa wanakuja kumfahamu Kristo kwa sababu ya ushirika ambao wameona kati yetu."*

**Shughuli: Kufanya kazi kwa Pamoja**
Tafuta mchoro wa ukuta wa mawe kwenye kitabu chako cha kumbukumbu na uwaonyeshe wana kikundi. Kuzunguka mawe andika chini maneno yote yanayokuja ndani ya mawazo yako unapofikiri juu ya kufanya kazi pamoja na nini kinatokea wakati watu wanapofanya kazi pamoja. Hizi ni mifano michache:

- Umoja
- Urafiki
- Mabadiliko

**Ikiwa unajifunza pomoja na kikundi**
Tafuta mstari wa mawe juu ya ukuta wa mawe ndani ya kitabu chako cha kumbukumbu na waambie wana kikundi kusema kwa sauti maneno yanayokuja kwenye mawazo yao wanapofikiri juu ya kufanya kazi kwa pamoja na nini kinatokea wakati watu wanafanya kazi pamoja. Andika maneno hayo juu yam awe. Hapa kuna mifano michache:

- Umoja
- Urafiki
- Mabadiliko

**Kikundi cha Uzima Hadithi**
Nkandu* alisikia habari za Dignity toka kwa rafiki aliyemkaribisha kwenye mkutano Kikundi cha Uzima. Nkandu alienda kwenye mkutano na alishangazwa nay ale ambayo Kikundi cha Uzima vinafanya na kujifunza. Nkandu hakuishi katika kijiji hicho lakini alitaka kitu kianzishwe ndani ya kijiji chake. Kikundi kilimwambia kuwa ni jambo rahisi, kwamba alihitaji watu watatu ama zaidi kujiunga naye, na achukue nakala ya kitabu kumsaidia kuanzisha mikutano.

Kwa hiyo, alienda nyumbani akaanza kuwakusanya watu. Kwanza, aliwaalika watu toka ndani ya kanisa lao la Angilikana. Wote walifika wakaunda Kikundi cha Uzima – hata hivyo baada ya majadiliano, walitambua kwamba waliwahitaji watu wengine na wakawatia moyo wengine kujiunga. Waliombea jambo hilo na Nkandu akawaambia kila mtu aende na kumleta mtu mwingine toka kanisa tofauti kwenye kikundi. Wiki iliyofuata, watu wengi walihudhuria kiasi kwamba Kikundi cha Uzima kilikuwa kikubwa ikabidi wagawanye view vikundi viwili tofauti!

**Jina limebadilishwa kutunza siri za ndani*

**Maswali: Tofauti inayofanywa na Vikundi vya Uzima**
Unakumbuka hadithi ya kijiji toka somo lililopita? Inazungumzia kuhusu kijiji kilichokuwa na ubishi na mashindano na hawakufanya kazi kwa pamoja.

- Vikundi vya Uzima ulizosoma habari zake leo zina tofauti gani na hadithi ya kijiji uliyosoma wiki iliyopita?
- Vikundi vya Uzima wamefanya nini?
- Unafikiri watu walijisikiaje walipokaribishwa na kwenda kwenye Kikundi cha Uzima?

*"Nilikuwa na wasiwasi kujaribu kufanya kitu kipya kijijini kwetu maana watu wengi hawataki mabadiliko na makanisa yamekuwa yakifanya mambo hayo hayo kwa miaka mingi. Nilitaka kuona makanisa yakifanya kazi pamoja na kuwafikia wanaoteseka, na nilisikia kama Mungu anasema natakiwa kujaribu kufanya kitu kipya. Kikundi cha Uzima wamefanya mambo ya ajabu, ilimaanisha watu wa toka makanisa tofauti walianza kufanya kazi kwa pamoja, kwa pamoja waliwasaidia waliokuwa wanateseka na njaa na wachungaji walifurahi walipowaona wakifanya kazi kwa pamoja. Ninayo furaha nilimwamini Mungu na akanipa ujasiri kwa sababu sasa nawasaidia watu kuanzisha Vikundi vya Uzima ndani ya jumuia nyingi nyingi!"*
- ***Mutambo***

**Omba**
Fungua kwenye kitabu chako cha kazi na ufungue ukrasa ulikoandika majina ya watu juu ya mawe. Waombee hao watu moja moja waweze kufanyika mawe yaliyo hai, waweke imani yao kwa Yesu na kuweka uzima yao kwenye msingi ambao ni Yesu. Omba kwamba wafanye kazi kwa pamoja kuleta mabadiliko kwenye kijiji na kwamba makanisa yafanye kazi kwa pamoja kuleta mabadiliko ndani ya kijiji.

*"Ndani ya vijiji vingi watu toka makanisa tofauti wanagombana na kushindana ni nani wa kuja kanisani kwao na nani anafanya vitu bora zaidi. Nkandu aliweza kuwaleta watu pamoja toka makanisa tofauti badala ya kugombana walitakiwa kutambua kuwa wao ni sehemu ya familia moja, familia ya Mungu, na wanaweza kusaidia watu zaidi kama wakifanya kazi pamoja."* – ***Asisi***

**Kufanya Wiki Hii**
Wiki hii mwombe Mungu akuonyeshe mtu atakayekuunga mkono kwa safari hii, mtu anayemfuata Yesu na anatamani kuona mabadiliko ndani ya kijiji. Fikiri namna unavyotaka huyo mtu kukuunga mkono kama wakikubali. Panga kukutana nao na uwashuhudie safari ya Dignity, waambie nini imekuvutia juu yake na namna ninyi nyote mnaweza kuwa sehemu yake. Waulize kama wanaweza kukuunga mkono kuanzisha Kikundi cha Uzima. Mwombe kwa pamoja Mungu aweze kuwasaidia kuanza kitu kipya ndani ya kijiji chako.

Hakikisha unawaambia jinsi unavyotaka wakuunge mkono!

Mtu huyu anaweza kuamua pia kujifunza ***Safari Kijijini*** pamoja nawe, au unaweza kupanga kukutana pamoja nao baada ya kujifunza kila somo na kuwashuhudia yale uliyoyajifunza.

**Andika Chini**
- Ni nani umekutana naye wiki hii kumshuhudia hadithi ya Dignity?
- Watakuunga mkono kuanza Kikundi cha Uzima?
- Ungependa wakuunge mkono namna gani?
- Je huyu mtu atajifunza vipindi pamoja nawe au kukutana nawe kila baada ya somo moja?

**Wiki hii, panga kuzungumza na mtu wako wa mawasiliano**

- Waambie hali ya kijiji chako nay ale ambayo ungependa kuyafanya.
- Waambie watu ambao tayari umezungumza nao.
- Andaa swali lolote la kuwauliza juu ya Dignity au kuanzisha Kikundi cha Uzima.

**Shughuli ya ziada**

Shughuli hizi za ziada zitakusaidia wewe kufikiri yale uliyojifunza, na kayaingiza kwenye mazoezi na kupanua uwelewa wako. Hupaswi kufanya shughuli zote za ziada lakini tunakutia moyo ufanye moja au mbili. Unaweza kuchagua moja unayoona itakusaidia au unayofurahia zaidi!

**Uchaguzi 1:** Nenda tafuta mawe kwenye kijiji chako, wakati unapotembea omba kwamba Mungu amfanye kila mtu jiwe lillilo hai.

**Uchaguzi 2:** Weka jiwe dogo ndani ya mfuko wako na ulibebe kwa wiki nzima. Kila mara unapolihisi jiwe, omba kwamba Mungu ayatumie mawe yaliyo hai ndani ya kijiji chako kufanya kazi pamoja na waunganike.

**Uchaguzi 3:** Tafuta ukuta ama jingo ndani ya kijiji chako na uende kutazama jinsi ilivyojengwa.

- Je ni imara?
- Mawe yameunganishwaje pamoja?
- Je mawe ni za muundo na vipimo tofauti?
- Ukuta/jengo ulijengwa juu ya? Je msingi ni imara ama dhaifu?

**Uchaguzi 4: Kama unayo rafiki ambaye ni kiongozi wa kanisa nenda jadili naye juu ya maswali haya.**

- Waulize wanaendeleaje?
- Waulize wanajisikiaje kuwa kiongozi wa kanisa. Wanafurahia? Je ni kazi ngumu? Changamoto ni zipi?
- Waulize wanajisikiaje kwa yale ambayo watu ndani ya kanisa lake wanafanya.
- Waulize kama makanisa yanafanya kazi pamoja. Kwa nini wanfanya ama kwa nini hawafanyi.
- Waulize kama kuanzisha Kikundi cha Uzima ni wazo jema na nani wa kumshirikisha hili wazo.

Andaa kumbukumbu toka kwenye majadiliano yako ndani ya kitabu chako cha kumbukumbu.



# CHOMBO CHA KAZI:
## Tembea na Yesu

**Alizaliwa mwezi wa tano 1832, James Hudson Taylor alikuwa mmisionari Mwingereza aliyeshuhudia injili kwa maeneo yasiofikiwa ya China. Anajulikana kuwa mwanzilishi wa umisionari wa ndani wa China, shirika lililotuma wamisionari mamia kushuhudia habari za Yesu katika taifa la China.**

Hudson Taylor aliingia kwenye umisheni kwa namna tofauti ya wamisionari wa kipindi hicho. Alijiunganisha kwenye mila na desturi kwa kujifunza lugha, akivaa mavazi ya wenyeji na kutengeneza nywele zake kama za wenyeji asili. Muda wake mwingi alitumia kutafsiri Biblia kwa lugha ya Mandarin na akajifunza kuwa daktari ili aweze kuwahudumia watu. Aliongoza pia vikundi vidogo, muda mwingi akiwa na watu akiwasaidia kukua katika Mungu.

Kwa ukiri wake mwenyewe, Hudson Taylor hakuwa mtu mwenye nguvu. Uzima yake kama mmisionari yalijazwa na kazi na magumu. Mke wake alifariki akiwa na umri wa miaka thelathini na tatu, mtoto wake wanne kati ya watoto nane alifariki kabla ya kufikisha miaka kumi, Hudson mwenyewe aliteseka na matibabu yasiyokuwa na idadi. Bado alisonga mbele, ndani ya akili yake hakuna kitu kilichokuwa cha muhimu kuliko kushuhudia Habari Njema kwa watu wa China.

Ndani ya moyo wa umisionari wake kulikuwa na hisia kali kwa Mungu. Alikuwa akijulikana kama askari wa maombi aliyetumia muda wake mwingi kujifunza neon la Mungu. Hata wakati wa udhaifu na mateso, alijua ataangukia katika mikono ya Mungu aliyempenda. Ndani ya kitabu chake cha kumbukumbu aliandika, *"Nimekuwa dhaifu siwezi hata kusoma Biblia yangu… hata kuomba, naweza tu kulala kwenye mikono ya Mungu kama mototo mdogo na kuamini."*

Ni huu uhusiano wake na Mungu ndiyo uliyomwendesha Hudson Taylor katika kazi yake, ilimsisitiza kuendelea na kumwezesha kujitoa kabisa kwa watu wa China. Uhusiano wake na Mungu ulikuwa ni msingi kwa kazi yake yote. Bila muda wake wa maombi, kujifunza Biblia na kuwa na ushirika na Mungu, hakuna unyayo wa Hudson Taylor ungeweza kuwezekana.

Maelfu ya Wachina walifikia kumjua Yesu kupitia kazi na mifano ya wamisionari kama Hudson Taylor na mpaka siku hii ya leo, China inayo makanisa yanayokuwa kwa haraka duniani kote. Hii yote imetokana na mbegu zilizopandwa zaidi ya miaka mia moja iliyopita.

Hadithi kama hiyo ya Hudson Tailor ni ya misukosuko na tunaweza kujaribiwa kufikiri kwamba Mungu hawezi kufanya mambo hayo katika uzima yetu. Hata hivyo ukweli ni kwamba walikuwa ni watu wa kawaida kama sisi, waliokuwa na uhusianao na Mungu mwenye uwezo mkubwa sana. Kwa maneno ya Hudson mwenyewe, *"Mungu hatafuti watu wenye imani kubwa, bali anawatafuta watu binafsi ambao wako tayari kumfuata."* Hii ina maana ya mtu binafsi toka mahali popote. Tunapochagua kumfuata Mungu, tunaingia kwenye mabadiliko ya uzima tunapotembea naye.

Wakolosai 2:6-7 inazungumzia juu ya mwendo huu na Yesu.

> *[6]Basi kama mlivyompokea Kristo Yesu, Bwana, enendeni vivyo hivyo katika yeye; [7]wenye shina na wenye kujengwa katika yeye; mmefanywa imara kwa imani, kama mlivyofundishwa; mkizidi kutoa shukrani.*

Tumemkaribisha na kumpokea Yesu uzima mwetu nah ii ina maana kuwa tunaishi uzima ya kweli na kuwa na uhusiano ulio hai na yeye. Kuna kifungu kwenye Biblia kinasema basi siyo sisi tena tunaoishi, bali ni Kristo ndani yetu (Wagalatia 2:20). Mikono yetu inakuwa mikono yake na miguu yetu inakuwa miguu yake.

Tumechagua uzima yake yawe yetu, kulingana na uzima yetu na maamuzi yetu kwa jinsi alivyo na vitu anavyovitaka kwetu. Yesu siku moja alitoa mfano wa mtu mmoja aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba (Mathayo 7:24-27). Dhoruba ikaja ikaipiga nyumba lakini kwa vile ilijengwa juu ya mwamba, msingi sahihi, nyumba ilisimama imara. Yesu ni kama mwamba kwenye mfano huu, kama tunataka kusimama imara katika imani yetu na katika uzima yetu basi tunatakiwa kujenga uzima yetu ndani yake.

Kifungu kwenye kitabu cha Wakolosai kinasema tunatakiwa kutiwa nguvu kwenye imani yetu. Kama tukifikiri juu ya imani yetu kuwa ya mahusiano na Yesu basi kinachotia nguvu imani yetu ni kukua karibu na Yesu. Tunafanya haya kwa kuwa na muda na yeye.

Kwa njia moja Hudson Taylor alikua katika imani yake kwa kusoma Biblia. Biblia ni maneno ya Mungu yaliyoandikwa na amezungumza na watu kupitia neno lake kwa maelfu ya miaka. Tunapokuwa na muda na neno la Mungu anafunua kweli kwetu, kutuonyesha kuwa heye ni nani na kuyatengeneza uzima yetu yafanane zaidi na yeye. Ni lazima kufahamu kuwa neno la Mungu ni chakula chetu yenye kupendeza na kutia nguvu imani yetu.

Katika mawasiliano yeyote, mawasiliano ni ya muhimu sana na maombi ni njia yetu ya kuwasiliana na Mungu. Siyo tu kwamba kuongea na Mungu, bali kumsikiliza pia. Maombi ni lazima yawe njia mbili ya majadiliano baina yetu na Baba yetu aliye mbinguni anayetufanya sisi kumfahamu kwa ndani zaidi, na kwa kututia moyo. Maombi yalikuwa ni sehemu ya muhimu sana katika uzima ya Yesu. Ilimtia Yeye nguvu, ujasiri na tumaini kuyaishi uzima yake hapa duniani. Pia sisi tunahitajika kuyapa maombi kipaumbele kama Yesu.

Mungu anahitaji uwe na muda naye. Anakutaka uombe; kuongea naye na kumsikiliza. Ametengeneza njia kwa uzima yako na anataka kutembea pamoja nawe ndani yake. Anatukaribisha sisi sote kukua katika uhusiano wa ndani pamoja naye. Mahusiano haya ni msingi ambao Mungu anaweza kufanya mambo ya ajabu mno ndani ya uzima yako zaidi ya unavyoweza kuomba au kuwaza (Waefeso 3:20).

**Fikiri juu yake**
Andika mawazo yako chini ndani ya kitabu chako cha kumbukumbu.

- Mahusiano yako na Mungu yanaonekanaje hivi sasa? Je unajisikia kuwa karibu na yeye au uko mbali naye?
- Je unajenga uzima yako ndani ya Yesu? Je unamchagua Yesu katika kila unayopitia?
- Ni hatua gani utachukua kukua karibu zaidi na Mungu? Je utaanza kutenga muda kila siku wa kukaa na Mungu?

3



# Injili ni Nini?

Katika hili tumelifahamu pendo, kwa kuwa yeye aliutoa uhai wake kwa ajili yetu; imetupasa na sisi kuutoa uhai wetu kwa ajili ya hao ndugu.

1 Yohana 3:16

**Lengo**
Somo hili litakusaidia kufahamu na kushuhudia injili, ujumbe wa Yesu.

**Mwisho wa somo hili utakuwa na:**

- Umeelewa injili ni nini
- Umeelewa kwa nini injili ni habari njema kwako, kwa kijiji chako na kwa dunia yote

**Tazama Nyuma**
Kila mwanzo wa kila somo tunataka kukutia moyo utazame nyuma kwenye somo lililopita na ufikiri yale uliyoyafanya na yale ambayo Mungu amekufundisha.

- Ulijifunza nini toka somo la mwisho kuwa sehemu ya hadithi ya Dignity?
- Umemshuhudia mtu yeyote hadithi ya Dignity? Aliipokeaje?
- Mungu amekuambia nini kuhusu kuanzisha kitu kipya ndani ya kijiji chako?

**Mafundisho: Injili ni nini?**
John Piper, mwalimu wa Biblia na mwandishi, alieleza injili katika njia ifuatayo:

> *“Injili ni habari njema isiyokuwa na kikomo na inayoongeza furaha isiyochosha, inayomtosheleza Kristo kuwa wetu bure na milele kwa imani kwa msamaha wa dhambi kupitia kifo chake na kupokea tumaini kwa kufufuka kwake Yesu Kristo.”*[1]
>
> *John Piper*

Kwa maneno mengine, njia imefunguliwa kwa Yesu Kristo na anatoa zawadi ya bure ya msamaha na uzima ya baadaye yenye uhakika ya kufufuka kutoka kwa wafu!

**Shughuli: Wewe unafikiri Injili ni nini?**
Waza kama unajaribu kumweleza mtu asiyefahamu lolote kuhusu Yesu injili ni nini. Ndani ya kitabu chako cha kumbukumbu jibu maswali haya:

- Injili ni nini?
- Injili ni kwa ajili ya nani?
- Nini kilichotokea uliposikia na kupokea injili?
- Nini kilichotokea kwa watu unaowafahamu waliosikia na kupokea injili?

**Ikiwa unajifunza na kikundi**
Mwambie kila mtu kuandika chini majibu yao kwa maswali kwenye shughuli hii, halafu kila mtu ashirikishe jibu lake na wengine ili kila mtu asikie jibu la mwenzake. Watu wengine wanaweza kushindana kwenye kujibu maswali haya au kuhitaji muda zaidi. Wahakikishie kuwa mwisho wa somo hili watafahamu injili ni nini na kuweza kuwaambia wengine.

[1] Piper, J 2002, *What is the Christian Gospel?* Njia ya kufikia 5 October 2020. Inapatikana kwa: https://www.desiringgod.org/articles/what-is-the-christian-gospel

**Hadithi: Chifu wa Kihindi**
Kulikuwepo na kabila fulani la Kihindi lililokuwa likiteseka kwa sababu ya ukame. Chakula kilikuwa cha shida na watu wakaanza kuibiana ili waweze kuishi.

Chifu alifahamu kuwa wizi ni husababisha kufa kwa kabila, hivyo akaweka sheria inayosema mtu mwingine akikamatwa akiiba atapelekwa katikati ya kijiji, na kufungwa juu ya nguzo na achapwe viboko hadharani. Chifu alijua kuwa lazima haki itendeke.

Siku ya pili, kwa hakika, mwizi alikamatwa. Kila mtu akataka kujua mwizi ni nani na kushuhudia adhabu.

Kila mtu alishtuka, kuona kuwa mwizi alikuwa ni mama yake mzazi wa Chifu. Atafanya nini? Alikuwa Chifu mzuri, na asingeweza kupuuza sheria aliyeiweka jana yake tu. Angetenda haki tu.

Lakini huyu alikuwa mama yake. **Alimpenda** sana. Pia alikuwa ni mzee na dhaifu; kichapo kingeweza kumwuua. Angemsababishaje kuteseka?

**Maswali: Chifu wa Kihindi**

- Unafikiri Chifu atafanya nini?
- Ikiwa Chifu atamwadhibu mama yake, angehakikisha **haki** inaonyeshwa. Je atatenda jambo hili? Kwa nini ama kwa nini asilitende?
- Kama Chifu akimwachilia mama yake na asimwadhibu, atahakikisha **upendo** unaonyeshwa. Je atatenda jambo hili? Kwa nini na kwa nini asilitende?
- Je Chifu ataonyeshwa vyote viwili upedo **na** haki?

**Hadithi: Chifu wa Kihindi (inaendelea)**
Chifu akatoa agizo vifundo vya mama yake vifungwe kwenye nguzo ili kichapo kianze. Akamwita mtekeleza adhabu afike mbele, na fimbo mkononi.

Alipokaribia kuamuru kuchapa ianze, Chifu akaingia katikati ya mama yake na mtekeleza adhabu. Akamzungushia mama yake mabega yake mapana kwa nyuma na mwili wa mama ukawa umezingirwa kabisa na mwili wa Chifu, akaamuru kichapo kiendelee.


Fimbo zilipokuwa zikianguka, zilianguka juu yake, akapokea mchubuko kamili wa adhabu ya mama yake. Kwa tendo hilo ikawa ametenda haki, kwa kubeba adhabu, na upendo, kwa kuteseka yeye mwenyewe.

Chifu alionyesha upendo kwa mama yake na akaonyesha haki.

Hivyo ndivyo Yesu alivyofanya kwa ajili yetu.

**Mafundisho: Alama 4**
Njia kuu ya kuielewa injili na kuieleza kwa wengine, ni kutumia njia rahisi inayoitwa ***Alama 4***.[2] Hii ni njia rahisi ya kukumbuka injili na kutumia picha 4 kufahamu na kushiriki injili.

[2] Tafuta zaidi kupitia tofuti yetu www.the4points.com



Picha 3 za kwanza zinatusaidia kuongea juu ya kweli ya injili, habari njema za Yesu. Picha ya mwisho inatualika kufanya maamuzi kuchagua kumfuata Yesu.



**Alama 1: Mungu ananipenda**
Mungu anakupenda. Upendo siyo kujisikia tu; ni tendo. Upendo hufanya jambo. Kama ilivyo, upendo wa Mungu ni tendo, inafanya jambo. Lakini upendo siyo jambo ambalo Mungu tu anafanya. Mungu ni pendo. Mungu ni mfano mkubwa wa upendowa halisi na bora. Kila jambo afanyalo Mungu inaambatana na upendo.
Mungu anasema:

> *Naam nimekupenda kwa upendo wa milele.*
>
> *Yeremia 31:3*

Mungu alitupenda upeo kiasi cha kumtuma mwanaye, Yesu, kufa badala yetu.

> *Katika hili tumelifahamu pendo, kwa kuwa yeye aliutoa uhai wake kwa ajili yetu; imetupasa na sisi kuutoa uhai wetu kwa ajili ya hao ndugu.*
>
> *1 Yohana 3:16*

Chifu kwenye hadithi alimpenda mama yake, hakusema tu kuwa anampenda bali alionyesha kwamba anampenda mama yake kwa tendo alilolitenda.



**Alama 2: Nimetenda dhambi**
Watu wengi wanaamini kuwa dhambi ni wakati tunapotenda kosa. Dhambi ni zaidi ya hilo. Biblia inatuambia dhambi ni mtazamo uliyoko ndani ya uzima yetu, kama tutachagua kuishi uzima yetu na Mungu ama bila Mungu. Tunapompa Mungu uzima yetu tunakuwa hai kamili. Tukiyashikilia uzima yetu mbali naye, tunakuwa tumekufa kiroho. Biblia inasema WOTE kwa sababu siku zote kuna wakati tu tulichagua kuishi bila Mungu ndani ya uzima yetu.

> *Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.*
>
> *Warumi 3:23*

Tunaposhikilia uzima yetu mbali na Mungu, anachokiita 'dhambi' inakua ndani ya uzima yetu na ndani ya dunia. Ikiwa ni uongo kidogo, wivu, usinzi ama kuua kila dhambi inatutenganisha na Mungu na ina matokeo yake na adhabu.

Yapo matokeo mengi ya dhambi. Dhambi inaharibu uhusiano wetu na Mungu, inaharibu uhusiano wetu na watu, jumuia zetu na taifa letu, hata inaharibu dunia.

Tunapotenda dhambi, tunachukua uamuzi wa kuishi wenyewe na kuwa kinyume na Mungu. Basi tutaishi na matokeo ya maamuzi tunayoyafanya. Biblia inasema mshahara wa dhambi ni mauti.

> *Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti*
>
> *Warumi 6:23*

Kama hatutaki kuishi na Mungu hapa na sasa, tunachagua kuishi bila yeye milele. Hii ni adhabu kwa kutochagua kuishi uzima yetu na Mungu na kuwa upande wa 'makosa' ndani ya dunia hii. Mungu anatupenda na anapenda kutujua, anataka kuitengeneza dunia tena. Mungu pia ni hakimu wetu na anafanya haki, kwa hiyo ataihukumu dunia na sisi na tutakuwa tunakabiliana na adhabu ya dhambi.

**Chifu kwenye hadithi alijua matendo ya mama yake kwamba yalipaswa kulipwa na kulikuwa na adhabu juu yake, kwa hiyo akatoa maagizo kuwa kichapo kianze.**

**Alama 3: Yesu alikufa kwa ajili yangu**
Yesu alizaliwa mwanadamu na Mungu pia na muda alipokuwa duniani hakutenda dhambi, aliishi uzima yake pamoja na Mungu kamili. Yesu alitoa uzima yake kulipa adhabu ya dhambi ZAKO na dhambi KILA MMOJA. Kwa kufanya hivi amefungua njia kwetu tuzaliwe upya, kuwa hai kiroho na kuishi na Mungu. Mungu anatutaka sisi kuishi naye na kwa ajili yake katika dunia hii na milele.

> *[16]Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. [17]Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye. [18]Amwaminiye yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu.*
>
> *Yohana 3:16-18*

Mungu anaipenda dunia sana kiasi cha kumtuma Mwanaye, Yesu, katika dunia. Hakumtuma Mwanaye ili kushtaki au kulaumu watu, bali alimtuma Mwanaye ili aje kusaidia kuiweka dunia sawa tena.

Yesu alikufa msalabani na kufufuka tena siku ya tatu. Hakubaki amekufa kwa sababu alikuwa Mwana wa Mungu na alikuwa na nguvu kuliko kifo chenyewe.

Chifu kwenye hadithi yetu alimpenda mama yake sana kiasi cha kulipa adhabu kwa ajili yake na akasimama sehemu yake kupokea adhabu ya makosa yake.

**Alama 4: Nataka kuamua kuishi kwa ajili ya Mungu**
Unao uchaguzi wa kufanya.

Upendo haujilazimishi wenyewe ndani ya uzima ya mtu. Upendo unatoa uhuru wa kuchagua. Vile Mungu ni pendo, hajilazimishi mwenyewe kwetu sisi lakini anaturuhusu kufanya maamuzi yetu wenyewe. Tunatakiwa kuamua kupokea zawadi yake ya msamaha ili tuwe huru na adhabu, na kukabidhi uzima yetu kwa Mungu na kuishi jinsi anavyopenda kuanzia sasa na kuendelea.

Tunapoishi kwa ajili ya Mungu, Roho wake huja na kuishi ndani yetu na kutufanya wapya. Anatusaidia kufikiri na kutenda zaidi kama Yesu ili sisi na wengine tuweze kuwa nguvu ya Mungu ndani ya dunia.

> *Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka.*
>
> *Warumi 10:9*

Tunapofanya maamuzi haya, tunapokea uzima mapya ndani ya Yesu sasa na tunapokea uzima wa milele na kuishi na Mungu milele.

*Na huu ndio ushuhuda, ya kwamba Mungu alitupa uzima wa milele; na uzima huu umo katika Mwanawe.*

*1 Yohana 5:11*

**Maswali: Alama 4**

- Unaposoma ***Alama 4***, nini kinacho kushangaza?
- Umesoma kitu chochote ambacho ni tofauti na jinsi unavyoielewa injili-- kama kipo ni nini?
- Kwa nini injili ni habari njema kwako?
- Kwa nini injili ni habari njema kwa kijiji chako?

> *"Nilifikiri injili ni yale niliyoyafanya kwa ajili ya Mungu, nimekuwa nikijaribu kufanya kila wakati mambo mema kumpendeza yeye na nimekuwa nikisika hukumu kila wakati ninapotenda jambo baya. Lakini nilipotambua kuwa wokovu ni zawadi ya bure toka kwa Yesu, nilibadilika kabisa! Sikuwa tena nafanya vitu kwa sababu ni lazima kufanya, badala yake nawapenda watu kwa sababu napenda kufanya kufanya. Sikushikilia tena kuwa na uchungu na watu kwa sababu napenda kuwa na uhusiano mzuri nao. Sikusikia hukumu kwa mambo mabaya niliyoyafanya au wakati mwingine kufanya, bali niliyaombea na kutubu na kukubali msamaha wa Mungu." –* ***Asisi***

**Mafundisho: Yale ambayo injili <u>siyo</u>**

Kufahamu injili ni nini, inatusaidia sisi kufahamu yale ambayo injili <u>SIYO</u>. Hapa kuna mifano michache:

- Injili maana yake siyo kwa sababu Mungu anatupa vitu. Hii ina maana:
  - Siyo kwa sababu Mungu anatupa fedha nyingi.
  - Siyo kwa sababu Mungu anatupa mafanikio.
  - Siyo kwa sababu Mungu anatupa afya njema.
  - Siyo kwa sababu tunakuwa na uzima mazuri bila kuteseka.
  - Siyo kwa sababu umejitosheleza.
  - Siyo kwa sababu Mungu anatupa bahati nzuri.
- Injili siyo kwa sababu rahisi tu ya kutenda matendo mema. Hii ina maana:
  - Siyo kwa sababu wewe ni bora kuliko mtu mwingine.
  - Siyo kwa sababu ya kupokea upendo wa Mungu kwa kutenda matendo mema.
- Injili siyo kufanyia 'dini kazi'. Hii ina maana:
  - Siyo juu ya mtu kuwa mtu wa dini.
  - Siyo tu kwa urahisi kuwa na mafundisho mazuri.
  - Siyo kwa sababu ya kwenda mbinguni. (Mungu anayafurahia uzima yako ya sasa.)
- Injili siyo kwa ajili yangu tu. Hii ina maana:
  - Siyo kwa sababu ya Mungu kuniokoa mimi tu. (Yesu alikufa kwa ajili watu wote.)
  - Siyo njia moja ya njia nyingi ya wokovu. (Yesu ndiye njia ya pekee.)

**Maswali: Yale ambayo injili <u>siyo</u>**

Soma pole pole orodha hii na kujibu maswali kwenye kitabu chako cha kumbukumbu:

- Kwa yale ambayo injili inasema <u>siyo</u> yako nje kwako? Kwa nini?

- Uliwahi kufikiri injili ni mmoja vitu hivi?
- Chukua moja ama mbili ya maelezo haya. Sasa waza kama ulifikiri hayo Ndiyo maana ya injili (badala ya kuwa siyo injili). Tazama yale asemayo Mutambo hapa chini kama mfano wa kuyatekeleza haya.
    - Hii inaleta adhari gani kwa yale unayofikiri kuwa Mungu ni nani?
    - Hii ina adhari gani namna ya unavyotenda kama Mkristo?

**"***Ikiwa tunaamini kuwa injili ni Mungu kutupa mafanikio basi tutafikiri kuwa Mungu anajali tu mambo ya* ***uzima*** *haya na mahitaji yetu. Tutawasahau wengine na kuwa wabinafsi. Kama tunaamini haya basi tutafikiri kuwa watu wenye mafanikio kwenye kijiji chetu ni watu wa Mungu na kuwadharau wale wasiyo na mafanikio (maskini, wagonjwa, wenye kuadhirika na kileo). Mungu anapendezwa na tabia zetu, jinsi tunavyowapenda wengine na na* ***uzima*** *yasiyokuwa na mwisho ya baadaye. Mungu anawaita watu wote, siyo tu wale wenye mafanikio, kuwa na mahusiano naye." -* ***Mutambo***

**Shughuli: Kwa sasa unafikiri Injili ni nini?**
Sasa umekuwa kwenye mafundisho, waza tena kama unajaribu kushuhudia injili kwa mtu asiyejua lolote kuhusu Yesu. Ndani ya kitabu chako cha kumbukumbu jibu maswali haya:

- Injili ni nini?
- Injili ni kwa ajili ya nini?
- Kwa nini Yesu alikufa?

**Ikiwa unajifunza pomoja na kikundi**
Tena, mwambie kila mtu kuandika majibu yao kwa maswali kwenye shughuli, halafu kila mtu anaweza kushirikisha majibu yao kwa wenzao ili watu waweze kusikia majibu ya wenzao.

*"Nilidhani injili maana yake ni kuyafanya uzima yangu marahisi, nilidhani Mungu atakufanya kuwa tajiri na mwenye mafanikio ukijaribu kujitahidi kubidiika. Lakini hii haikuwa kweli. Nimetambua kuwa siyo rahisi siku zote kuishi kwa ajili ya Mungu lakini mara zote yuko pamoja nasi na anataka kutusaidia. Hii ina maana kuwa sitawahukumu tena wale ambao ni maskini au wanaoteseka, lakini nataka kuwasaidia kama jinsi Mungu alivyotusaidia sisi. Nilishuhudia jambo hili kwa Kikundi cha Uzima na tukaamua kupeleka chakula kwa familia maskini ndani ya kijiji chetu mara moja kwa wiki." -* ***Agnes***

**Omba**
Sasa tunafahamu injili ni nini, labda sasa unataka kuyakabidhi uzima yako kwa Mungu tena, omba msamaha kwa mambo mabaya uliyoyafanya na kuukubali msamaha wake. Omba maombi haya:

*Mungu Baba,*
*Aksante kwa sababu ulikufa kwa ajili yangu na unataka nifanye vizuri katika kila hali.*
*Nisamehe kwa kukupuuza na kujifanyia mambo kwa njia yangu.*

*Sasa nimetambua kuwa dhambi zangu zilikujeruhi na watu walionizunguka na kwa jambo hili naomba unisamehe.*
*Aksante Yesu kwa sababu ulikuja na ukachukua adhabu ya dhambi zangu.*
*Aksante kwa sababu ulitoa uzima yako kwa ajili yangu.*
*Tafadhali nisamehe na unisaidie sasa ninapoamua kuishi uzima yangu kwa ajili yako.*
*Amina*

**Ikiwa unajifunza pomoja na kikundi**
Kipe kikundi nafasi ya kujibu, chukua muda kidogo ya kunyamaza kimya kufikiri juu ya injili ina maana gani. Kama mmoja wa kikundi atataka kukabidhi uzima yake kwa Mungu tena, omba maombi toka kwenye kitabu kwa pamoja.

**Mafundisho: Uadilifu**
Unakumbuka kwenye Somo la 1 tulijifunza kuwa watu wa Mungu kuwa miti mikubwa ya haki? Unaweza kukumbuka haki maana yake nini?

Haki kwa wepesi ina maana kuwa na haki mbele za Mungu na kwa watu pia. Yesu ndiye hitimisho la mwenye haki – alikuwa ni mwenye haki mbele za Mungu na kwa watu pia. Hatukuwa na haki mbele za Mungu na kwa watu wengine. Yesu alipokufa kwa ajili yetu alichukua makosa yetu (alichukua makosa yetu) na kutubadilisha kwa kuwa mwenye haki (alitufanya kuwa wenye haki pia). Tumefanywa haki mbele za Mungu na kwa watu siyo kwa sababu ya kitu chochote tulichokifanya bali ni kwa ambayo Yesu amefanya.

Yesu ametufanya kuwa haki mbele za Mungu. Hii ni HABARI NJEMA!

- Anataka kila mtu kuwa mwenye haki mbele za Mungu.
- Anataka kila mtu awe sawa na mwenzake.
- Anataka kila kitu ambacho ni kizuri, kamili na upendo kuonekane ndani ya vijiji vyetu, na dunia yetu.

Yesu alikuja kufanya kila kitu kuwa sawa tena. Kwa sababu anajali yale yanayotokea kwa sasa! Anataka dunia iwe na amani, tulivu, upendo na haki. Hii inaweza kuwa ni haki ya Mungu ikifanya kazi katika kila hali.

**Shughuli: Hiyo siyo haki!**
Kwa kawaida, kutokuwa na haki inaanza kwa kutokubaliana na ugomvi ambao tunayo ndani ya uzima yetu binafsi.

**1. Uzima yako:** Hebu chukua kama dakika tano fikiri juu ya watu ambao unao ugomvi nao, huwapendi, ama umewatendea hata vibaya bila haki. Inawezekana kuna mtu umemdanganya au kutomtendea vizuri. Inawezekana kuna kitu cha mtu ulichukua sehemu kabisa ikaweka tanzia katika uzima ya mtu huyo hapo mwanzo. Jibu maswali haya kwenye kitabu chako cha kumbukumbu:

- Je ni hali gani ama uhusiano gani katika uzima yako Mungu ameleta kwenye akili yako?
- Itafanannaje ukichagua kuanza kutenda kwa upendo?
- Itafananaje ukichagua kuanza kutenda kwa haki?

**2. Jumuia yako:** Chukua muda sasa kufikiri ni nini siyo cha haki katika jumuia yako. Jibu maswali haya kwenye kitabu chako cha kumbukumbu:

- Ni mahusiano gani siyo ya sawa? Nani anahusika?
- Ni hali gani isiyo sawa? Unafikiri kwa nini watu wanatenda kwa namna walivyo?

Kwa kuwa Mungu ametufanya kuwa wenye haki, tunaweza kushuhudia jambo hilo kwa wengine. Tumeitwa kuwa watu wa upendo, haki na waadilifu na kutunza sifa hizi kwenye uzima yetu, ndani ya jumuia na katika kila hali tutakayokutana nayo. Leo haya yote yanaletwa na Roho Mtakatifu wa Mungu akifanya kazi katika dunia hii, kupitia uzima ya hao waliompokea Roho Mtakatifu kwenye uzima yao. Haitoshi kabisa tunaposema tunamfuata Yesu lakini tukipuuza ama kusababisha vitu ambavyo siyo sawa ndani ya dunia yetu. Jambo hili mara zote siyo rahisi, ina maana tunatakiwa kuwa majasiri kwa sababu tuna taka watu wawe na haki mbele za Mungu na kila mtu kwa mwingine.

**3. Injili katika matendo:** Kama tunafahamu kuwa tuna haki mbele za Mungu basi tunakuwa na uhuru wa kuwapenda wengine na matamanio yetu ni wengine kuijua injili. Ukifikiria juu ya hali uliyoandika chini, jibu maswali haya kwenye kitabu chako cha kumbukumbu:

- Itaonekanaje kwa wale wanaohusika wakichagua kupendana?
- Itaonekanaje haki inapotendeka?
- Matokeo yatakuwa ni nini?
- Hii itakuwa na adhari gani kwa hao wanaohusika na kwa hao wanao wazunguka?

**Ikiwa unajifunza pomoja na kikundi**

1. **Uzima yako:** Waambie kikundi kujibu maswali wao wenyewe, halafu yaweke kwa watu wawili ama watatu kushuhudia majibu yao.
2. **Jumuia yako:** Uliza maswali haya kwenye kikundi na ongoza majadiliano.
3. **Injili kwenye matendo:** Uliza maswali haya kwenye kikundi na ongoza majadiliano.

**Hadithi wa Kikundi cha Uzima**

Katika kijiji cha Kundamfuma, kusini mwa Mansa, kulikuwa na Kikundi cha Uzima. Ndani ya kijiji hicho kulikuwepo na wanaume wawili, Salaka* na Ng'oma* walikuwa wakibishana juu ya motto wa Salaka aliyekuwa mgonjwa. Mganga wa kienyeji alikuwa amemwambia Salaka kuwa mtoto alikuwa mgonjwa kwa sababu Ng'oma kwa vyovyote alimlaani motto akamfanya kuwa mgonjwa.

Hii haikuwa sababu, na Ng'oma akakasirika sana na kuudhika. Mashindano yakawa mabaya sana wakaamua kupeleka shauri kwa Chifu. Hata hivyo, Chifu hakuweza kufikisha shauri mwisho. Kwa hiyo Ng'oma, ambaye hakuwa anafahamu jambo lolote, akampeleka Salaka mahakamani, akitaka malipo kwa jinsi tatizo lenyewe lilivyoadhiri uzima yake.

Kwa hatua hii, Kikundi cha Uzima kikaamua kumfuata Chifu kwa sababu ya shauri hilo na kutoa maana ya kwa sababu gani tukio hilo limetokea maana walikuwa wanajisikia vibaya kwa hali iliyokuwa ndani ya kijiji chao. Kikundi cha Uzima kikaomba kama wataruhusiwa kwenda kujaribu kuwapatanisha wanaume hao, hata ingawa kesi ilikuwa imeshaanza kusikilizwa. Chifu alijisikia vizuri kuona kuwa kulikuwepo na watu wengine walitaka kusaidia.

Jambo la kwanza walikwenda kwa Ng'oma wakamshauri amsamehe Salaka – na kwa mshangao alikubali! Kikundi cha Uzima kikamsaidia kulipa gharama za kuondoa shitaka mahakamani. Wakaenda kwa Salaka wakamwombea, wakamwambia amkaribishe Mungu kwenye hali ile na kufahamu kuwa ugonjwa kwa mtoto haikusababishwa na uchawi. Salaka akafikia mahali pa kuelewa na kuondoa tuhuma zote.

Kikundi cha Uzima kiliingia na kuwapatanisha watu hao tena. Walikuwa na adhari kubwa kwa hao watu wawili na kwa jumuia pia. Kijiji hakiteseki tena kwa sababu ya malumbano, wametambua kuwa kuna njia bora zaidi ya kutatua matatizo, waliwaona Wakristo kijijini wakifanya mabadiliko na wakaona injili katika matendo!

**Majina yamebadilishwa kutunza siri za ndani.*

**Maswali: Kikundi cha Uzima Hadithi**

- Tunajifunza nini toka kwenye hadithi hii?
- Kikundi cha Uzima kilifanya nini?
- Wanaume hao walifaidi namna gani walipopatanishwa?
- Kijiji kilifaidi nini baada ya wanaume hao kupatanishwa?
- Ni nini kingetokea kama Kikundi cha Uzima kisingefanya jambo lolote?

**Omba**

Tazama orodha ya yale ambayo hayako sawa kijijini kwako, mwombe Mungu akuonyeshe hali na watu wanaohusika jinsi anavyowaona. Omba juu ya upendo wa Mungu na haki katika kila hali na omba kwamba injili iwe hai ndani ya kijiji chako.

**Kufanya Wiki Hii**

Wiki hii andika orodha ya watu unaowafahamu ndani ya kijiji chenu wanaoishi kwa ajili ya Mungu na wanatamani kushuhudia upendo na ujumbe wa Yesu kwa wanakijiji. Mwombe Mungu akuonyeshe ni nani wa kumwandika kwenye orodha yako na uwaombee mmoja mmoja, wafanyike miti mikubwa ya Mungu. Fikiri juu ya watu toka makanisa tofauti na dini tofauti, wanaume kwa wanawake, wadogo kwa wakubwa na watu wa rika tofauti.

Wasiliana na watu 5 kwenye orodha yako, waeleze kwa uwazi kuwa unataka kuwasaidia na kuwafundisha yale unayojifunza ndani ya kitabu hiki, ili waweze kuwashirikisha wengine yale waliojifunza kwako. Waambie kwamba ungependa kufanya jambo hili kwa kufanya kazi pamoja kuanzisha kikundi kwenye kijiji, hii tunaiita Kikundi cha Uzima. Mnapofanya kazi pamoja, mtakuwa na nafasi ya kujifunza kwa pamoja, kuimarisha wengine kukua katika imani, kusaidia wanakijiji wengine na kuwafundisha wengine wanaowazunguka.

Waulize kama wangependa kuchukua hii nafasi. Waruhusu kukubali ama kukataa nafasi hii. Baadhi ya watu hawatataka kuwa sehemu nah ii ni sawa. Baadhi ya watu watataka. Waulize kama watapenda kukutana na wewe wiki inayofuata. Kikundi cha watu kitakuwa wanachama wa kwanza wa Kikundi chako cha Uzima, utakutana nao kupanga na kuomba kabla ya kuanzisha Kikundi cha Uzima na kuwakaribisha wengine ndani ya wiki chache.

**Andika Chini**

- Orodha ya hao unaowafahamu ndani ya kijiji chako wanaoishi kwa ajili ya Mungu na wenye hamu ya kushuhudia upendo na ujumbe wa Yesu na Wanakijiji. Chagua 5 wa kuwasiliana nao wiki hii.
- Umezungumza na nani wiki hii juu ya kuwa sehemu ya Kikundi cha Uzima?

- Walilipokeaje? Walifurahia? Walisita? Unafikiri walielewa yale uliyowaambia? Kama hawakuelewa utawasaidiaje waweze kuelewa?

**Shughuli ya Ziada**
Shughuli hizi za ziada zitakusaidia wewe kufikiri yale uliyojifunza, na kayaingiza kwenye mazoezi na kupanua uwelewa wako. Hupaswi kufanya shughuli zote za ziada lakini tunakutia moyo ufanye moja au mbili. Unaweza kuchagua moja unayoona itakusaidia au unayofurahia zaidi!

**Uchaguzi 1:** Chora picha moja moja ya zile alama 4 ndani ya kitabu chako cha kumbukumbu hapo na uandike sentensi pembeni yake kujulisha maana ya alama hiyo.

**Uchaguzi 2:** Tazama majibu yako nyuma kwa kazi inayosema ***Hiyo Siyo Haki!***
mahali ulipoorodhesha hali ambazo hazikuwa sawa katika uzima yako. Wiki omba namna utakavyoweza kubadilisha hali kuwa sawa. Je unahitaji kuomba msamaha? Ungependa kubadilisha njia zako? Ungependa kuwaonyesha watu upendo? Panga muda wa kwenda kuweka hali kuwa sawa na ulete badiliko la Mungu kwenye hali hiyo. Kama nafasi zikipatikana, shuhudia kwa nini unaweka mambo sawa nay ale uliyoyajifunza kwenye somo wiki hii. Andika chini chochote ulichoamua kufanya na adhari ya matendo yako.

**Uchaguzi 3:** Tazama nyuma kwenye majibu kwa kazi inayosema ***Hiyo Siyo Haki!***
ulikoorodhesha hali ambazo hazikuwa sawa katika jumuia yako. Wiki hii tenga muda uende wewe na rafiki yako mmoja ama wawili uzungumze na watu namna unavyopenda kuwasaidia moja ya hali ama mazingira yawe sawa na kuleta badiliko la Mungu katika hali. Kama nafasi ikipatikana, hakikisha unashuhudia kwa nini unaweka mambo sawa nay ale uliyoyajifunza kwenye somo wiki hii. Andika chini chochote ulichoamua kufanya na adhari ya matendo yako.

# 4



# Uzima ni Kupitia Familia

**Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake**

Yowana 1:12

**Lengo**

Mungu anatualika kwenye familia yake! Familia hufanya kazi kwa pamoja, kazi kupitia mgawanyo, kutazama yale yanayo waunganisha na kuwaalika watu wengine kuwa sehemu yao.

**Mwisho wa somo hili utakuwa na:**

- Umefahamu familia ya Mungu ilivyo na Mungu anafanyaje kazi ndani yake
- Umejifunza kinacho wagawanya watu na kinacho waunganisha watu
- Umejufunza jinsi Kikundi cha Uzima inavyounganisha Kijiji

**Tazama Nyuma**

Kila mwanzo wa kila somo tunataka kukutia moyo utazame nyuma kwenye somo lililopita na ufikiri yale uliyoyafanya na yale ambayo Mungu amekufundisha.

- Umejifunza nini toka somo lililopita juu ya injili tofauti inayofanya?
- Je umemshuhudia mtu yeyote injili ukitumia ***Alama 4***? Je ni rahisi ama ngumu? Walilipokeaje? Je wametaka kukabidhi uzima yao kwa Mungu?
- Umerekebisha hali kuwa sawa wiki hii? Ulifanya nini? Ilileta tofauti gani?
- Umemshuhudia mtu yeyote yale uliyojifunza wiki hii?

**Maswali: Familia Yangu**

- Kama wewe ni sehemu ya familia, familia yako inapenda nini?
- Kama hauna familia, umeona nini toka familia zingine?
- Nini kizuri juu ya kuwa familia?
- Nini kigumu unapokua na familia?

**Hadithi: Sherehe ya Chifu**

Paliondokea Chifu mmoja aliyewaalika watu wengi toka kwenye utawala wake kwenye sherehe kubwa sana. Watu walisafiri toka maeneo yote kuhudhuria sherehe hiyo kubwa. Watu walivalia nadhifu na kumletea Chifu sifa nyingi. Watu walikuwa wengi kutoka sehemu mbali mbali. Hii ilimfanya Chifu kufurahi. Aliwakaribisha kwa sababu alitaka kuona ufalme wake, na familia za watu aliowaongoza.

Baada ya siku kadhaa, alitambua kuwa watu wengi wa kabila lake walikuwa wanabishana. Ubishi ukawa juu ya nani aliyekuwa mzuri wa kudumisha mila. Walibishana juu ya nani aliimba wimbo bora. Walibishana hata na watu wa kijiji chao. Ilifikia hata mahali viongozi tofauti walikutana na watu tofauti na ilikuwa ni vigumu sana watu kukutana pamoja.

Jambo hili lilimtatiza Chifu na akashindwa kuelewa ni vipi mgawanyiko ulitokea. Akaamua kufanya jambo.

Usiku mmoja aliwakusanya viongozi wa makundi yaliyokusanyika. Juu ya chumba/bwalo kubwa aliweka kisu juu ya dari. Akawaambia viongozi yeyote ambaye angefikia kisu hicho angempa mamlaka ya kuwa Chifu. Angeweza kumpa kutawala ufalme wake wote.

Viongozi walishangaa na wakaanza kupigana wao kwa wao. Kila mmoja alijaribu kupanda ukuta, lakini akashindwa. Wengi wao walibaki kupigana mpaka wakasahau kufikia kisu kabisa. Baada ya saa moja kila mmoja alikuwa amechoka na kuvunjika moyo.

Kisha kwa busara chifu akawauliza, “Kwani nini mnadhani mnaweza kufanya kazi hii? Haiwezekani; dari iko juu sana kuifikia.” Akakusanya watu watano kusimama ardhini na watatu kusimama juu ya mabega yao, na wengine wawili juu yao. Viongozi hao walifanya jinsi walivyoagizwa na kila mmoja kusimama juu ya mwingine. Walikaribia kukifikia, ila hawakukifikia. Kisha chifu akapanda juu yao na kukifikia kisu mwenyewe.

Kila mtu alijua kile ambacho chifu alitaka kusema. Wakati walipokuwa wakitumia muda mwingi kubishana na kupigana, wakijaribu kumaliza kazi wao wenyewe bila mafanikio. Iliwagharimu ushirikiano wao wote kufaulu kufikia kisu. Chifu mwenyewe alihitaji msaada wao kuweza kukamilisha zoezi hilo.

**Maswali: Sherehe ya Chifu**

- Unafikiri hadithi hii inatufundisha nini?
- Kwa nini Chifu aliwaambia watu wajaribu kuchukua kisu?
- Walijifunza nini walipofanya kazi kwa pamoja?
- Unafikirije tabia za watu zilibadilikaje baada ya jambo hili?
- Kitu gani cha tofauti kingeweza kutokea waliporudi vjijini kwao?

**Mafundisho: Picha ya kanisa**

Hii ndiyo picha ya Kanisa lilivyo mashinani mwa bara la Africa. Inaweza pia kuwa kweli ya Kanisa mahali kokote kule. Kuna Chifu Mkuu ambaye ni Mungu, anatuangalia na kuona watu wake, Kanisa, tukigawanyika, tukipigana wenyewe na kutofautiana kwa mambo ya mila na desturi. Kama Chifu kwenye hadithi yetu anataka kuona watu wake, kabila lake, limeungana.

Wakati tunabishana, kama wale viongozi tunasahau juu ya kisu, na kusahau majukumu tuliyonayo. Wengi wanateseka; wengi hawamjui Mungu na tunasimama aidha kwa kujisaidia wenyewe ama tukibishana sisi kwa sisi.

Edmund Burke alisema, “Kilicho cha muhimu kwa uovu kuwepo ni pale watu wazuri wanapokosa kuchukua hatua.”[3] Wakati tunapojishughulisha na kukatishwa tamaa adui yetu anaendelea kufanya kazi zake, hapo mbele yetu ya macho yetu.

**Shughuli: Mgawanyiko kwenye Kijiji Changu**

Kumbuka kuwa kwenye somo letu la kwanza tuliangalia jinsi vijiji vingi vilivyogawanyika. Labda umezungumza na wengine ndani ya kijiji chako juu ya jambo hili. Jibu maswali yafuatayo kwenye kitabu chako cha kumbukumbu:

- Kama watu waliohudhuria sherehe ya Chifu, kuna mila na desturi zinazo wagawanya watu wanaomfahamu Mungu, Chifu Mkuu. Ni vitu vipi baadhi ambavyo watu wa kijiji kwako hawakubaliani navyo?

**Ikiwa unajifunza na kikundi**

Mjadili kama kikundi vitu ambavyo watu hawakubaliani navyo ndani ya kijiji chako.

[3] Imenakiliwa kutoka Burke, Edmund (1770) Wazo iliopo lisiloridhisha kwa wakati huu, Toleo la 3, Pall Mall, J Dodsley

*"Wazazi wangu kila mara waliniambia matajiri na maskini hawachangamani, na hata makanisa ya dini tofauti hazichangamani kamwe na makabila kamwe hawafanyi vitu pamoja hata kuzungumza mtu kwa mwingine. Hivyo ndivyo nilvyofikri tunapaswa kutenda. Lakini Mungu akanionyesha njia mpya ya kufanya vitu na kule mbinguni hakutakuwa na vikundi au makabila tofauti. Hivyo nikawaalika watu wa dini tofauti kwenye Kikundi chetu cha Uzima nikawaambia kuwa kwa vile wote tunamwamini Yesu hilo ndilo jambo linalotuunganisha na ni muhimu kulitazama jambo hilo. Nilizungumza na Chifu na akanisaidia kuzungumza na viongozi wa vijiji tofauti, nikawauliza kama kuna jambo tunaweza kufanya kuleta umoja. Wakaomba vyombo vya kufanyia kazi bustanini. Hatukuwa na uwezo wa kununua vyombo vipya, lakini tukaamua kutoa muda wetu na kuleta vyombo vyetu wenyewe kwa ajili ya kuvitumia. Sasa tuna lima bustani pamoja, kula pamoja na nawaeleza jinsi Mungu anavyotualika wote kwenye familia yake." – **Asisi***

**Mafundisho: Itakadi ya Wamasai**

Mungu hataki vijiji vilivyogawanyika, jumuia na makanisa. Anataka tufanye kazi pamoja na kujali na kupendana. Matamanio ya Mungu ni kuwa pamoja na kufanya kazi kama familia moja.

Njia moja ya kuanza kufanya kazi kwa pamoja ni kugundua yale tunayoyakubaliana. Hili ndilo jambo alilokuwa akijaribu kifanya Chifu ndani ya hadithi. Watu wanapaswa kuangalia tofauti zao, au waangalie yale ambayo itawaunganisha. Kupata kisu ni kitu ambacho kila mtu alitaka kufanya, walitakiwa kutazama jambo hilo na kufanya kazi pamoja kuweza kufanikio.

Mwaka 1960 wamasai wa Africa mashariki walifanya kazi na wamisionari kuandika *Itikadi ya Wamasai*. Hiki ni kipande cha maandishi kinachoeleza misingi ya imani ya Kikristo.

**Ikiwa unajifunza na kikundi**

Soma hiyo itakadi polepole na urudie tena polepole. Kama kikundi kuna kipengele chochote maalum kinacho washangaza na kwa nini?

Soma hii kwa sauti kubwa kama utaweza na soma polepole ili uweze kuchukua kila msemo.

*Tunaamini juu ya Mungu mmoja Aliye Mkuu, kwa upendo wake mkuu aliumba dunia nzuri na kila kitu kizuri ndani yake. Alimuumba Mwanadamu na akataka Mwanadamu awe na furaha duniani. Mungu anapenda dunia na kila taifa na kabila juu ya Dunia. Tulimfahamu Mungu huyu wa kweli tukiwa gizani, na sasa tunamfahamu katika nuru. Mungu aliahidi katika kitabu cha neno lake, Biblia, kwamba ataokoa dunia na mataifa yote na makabila.*

*Tunaamini kuwa Mungu alitimiza ahadi yake kwa kumtuma Mwanaye, Yesu Kristo, mwanadamu katika mwili, Myahudi kwa kabila, aliyezaliwa maskini kwenye kijiji kidogo, Aliyeacha nyumbani kwao na kila mara kuwa safarini akitenda mema, akiwaponya watu kwa nguvu za Mungu, akifundisha habari za Mungu na wanadamu, akionyesha maana ya dini ni upendo. Alikataliwa na watu wake, akateswa na akaangikwa msalabani, na akafa. Alibaki amezikwa kaburini, lakini fisi hawakugusa mwili wake, na siku ya tatu, Alifufuka toka kaburini. Alipaa mbinguni. Yeye ni Bwana.*

*Tunaamini kuwa dhambi zetu zote zimesamehewa kwa njia Yake. Wote wenye imani ndani Yake ni lazima wajutie dhambi zao, wabatizwe na Roho Mtakatifu wa Mungu, wakiisha kwa sheria ya upendo na kumega mkate kwa pamoja kwa upendo, kutangaza Habari Njema kwa wengine mpaka Yesu atakaporudi tena. Tunamngoja Yeye. Yu hai. Anaishi. Hili tuaamini. Amina.* [4]

Maelezo ya Itikadi ya Wamasai inaeleza nini maana ya kuwa Mkristo, Wakristo wanaweza kutokukubaliana juu ya baadhi ya vitu tofauti ndani ya kanisa lakini ni vema waamini kwamba hii ni kweli na kwa sababu wote wanakubali juu ya mambo haya wanaweza kufanya kazi pamoja. Tunapoona kuwa tulichonacho hufanana, vile vitu vinavyotuzuia kuungana vinatoweka.

**Vifungu vya Biblia**
Maandiko ya Biblia yanazungumzia juu ya utambulisho mpya na familia mpya ambayo sisi ni sehemu yake. Kitabu cha Yohana kiliandikwa na Yohana mwanafunzi aliyemjua Yesu. Mwanzoni mwa kitabu chake anazungumzia juu ya familia na sisi ni akina nani. Ni lazima ilikuwa ni muhimu kwake.

> *[10]Alikuwako ulimwenguni, hata kwa yeye ulimwengu ulipata kuwako, wala ulimwengu haukumtambua. [11]Alikuja kwake, wala walio wake hawakumpokea. [12]Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake; [13]waliozaliwa, si kwa damu, wala si kwa mapenzi ya mwili, wala si kwa mapenzi ya mtu, bali kwa Mungu.*

*Yohana 1:10-13*

**Maswali: Watoto wanakukumbusha juu ya nani?**
- Unao watoto ama unawafahamu watoto wowote ndani ya familia yako au kijijini kwako?
- Wanafanana na nani?
- Matendo yao yanafanana naya nani?

**Kikundi cha Uzima Hadithi**
Hope* ni mtoto mdogo wa watoto nane na kama mtoto alikuwa amezingirwa na upendo wa wazazi wake na ndugu zake. Sasa anao watoto watatu wakubwa wa kwake mwenyewe na ameweza kuwaonyesha huo upendo na uwema.

Hope sasa anaishi Nairobi mahali anakoamini kuwa kuna watoto kama 60,000 wanaoishi mabarabarani, wengi wao wakitumia madawa ya kulevya, wakinusa gundi na kujihusisha na makundi hatari.

Mwanzoni Hope alipohamia Nairobi, aligoma kwa kuona idadi ya watoto aliowaona barabarani. Alichanganywa na hao watoto na kujiuliza mbona hawakupendwa. Hakupata amani yeyote alipowafikiria akaanza kutafuta kuwajua na kuwajali kwa namna yeyote rahisi kwa jinsi alivyoweza. Nyakati zilipoendelea, watoto wakaanza kumfahamu na kumheshimu. Kwa ujumla waliacha kupigana kila mara wanapomwona akija.

Mpaka siku moja alipowaona wavulana wawili alitambua walikuwa wanapigana. Hata ingawa aliwafuata, waliendelea kupigana mpaka mmoja akasukumwa na kugongwa akapoteza fahamu.

[4] Itikadi ya Wamasai ilitungwa na Wamasai wa Afrika Mashariki wakishirikiana na Mkutano wa wamisionari wa shirika la Roho Mtakatifu. Tulinakili maandiko toka tovuti inayofuata: Haijulikani 9 March 2018, *Masai Creed* Njia ya kufikia 27 August 2020. Inapatikana kwa: https://en.wikipedia.org/wiki/Maasai_Creed

Katika hali hii, Hope akatambua kuwa mambo zaidi yanapaswa kutokea. Akaanza kukutana na kikundi cha akina mama 15 kujaribu na kufanya kazi kwa pamoja kuwasaidia watoto wa mabarabarani. Kwa pamoja na wengine, wameweza kuwasaidia watoto wanaoishi mabarabarani Nairobi kwa miaka 20 sasa.

Hope ameona kuwa tatizo halianzii Nairobi, bali ni kwenye jumuia wanakotoka watoto. Kwa huzuni, siyo jambo la kawaida kwa mama au baba walezi kutowahudumia au kutowajali watoto wanaowalea. Watoto hukimbilia mijini kwa kutoroka. Watoto mara nyingi hajaribiwa kuja na kujaribu kutafuta pesa kwenye miji mikubwa. Wanafikiri wanaweza kwenda mijini kwa muda mfupi, kutengeneza fedha kisha kurudi nyumbani. Lakini ukweli ni kwamba kwa haraka, kama ndani ya wiki 2, wanatambua kwamba wanapaswa kujiunga na genge la barabarani waweze kuishi. Magenge hayo ni yenye sifa mbaya kwa jinsi yalivyo funzwa.

Hope anasema kwamba namna ya kushughulikia tatizo ni lazima kwenda kwenye chanzo. Ni lazima kufanya kazi na vijiji mahali watoto wametokea kuzuiya kuondoka mahali walipo. Amejaribu jambo hili kwa idadi ya njia tofauti kwa miaka na ameona mafanikio kuwasaidia watoto kurudi nyumbani, lakini amepambana kutafuta hizo jumuia kushughulikia tatizo pamoja.

Hope anaamini kuwa Vikundi vya Uzima itawasaidia Wakristo kutazama nje ya kuta nne za makanisa yao na kuwajali hao wanaowazunguka. Anaamini kuwa umoja na tendo ambalo Vikundi vya Uzima wataunda italeta mabadiliko na kuwasaidia watoto kukaa nyumbani.

**Jina limebadilishwa kutunza siri za ndani*

**Maswali: Kikundi cha Uzima Hadithi**

- Unafikiri hadithi ya Hope inatufundisha nini?
- Alichukua hatua zipi?
- Matendo ya Hope yalikuwa na adhari gani kwa watoto?
- Matendo ya Hope yatakuwa na adhari zipi kwenye kijiji?
- Nini kingeweza kutikea kama hakuchukua hatua?

"Nafikiri kama watundani ya kijiji chetu wangetambua kuwa sisi sote ni sehemu ya kabila la Mungu wangetenda kwa tofauti. Kusingekuwa na matengano kati ya watu toka makanisa tofauti, kusingekuwa na mgawanyiko kati ya matajiri na maskini, watu wangeacha ubinafsi na kupenda zaidi kuwasaidia wengine." **– Agnes**

**Mafundisho: Familia ya Mungu**

Sisi ni watoto wa Mungu na watoto wanafanana na wazazi wao. Tunatakiwa kuonyesha upendo wa Mungu kwa kila mtu na kuwakaribisha kwenye familia ya Mungu, kwa jinsi walivyo.

Hope alikuwa sehemu ya familia yenye upendo hivyo ilivunja moyo wake alipowaona watoto hawakuwa sehemu ya familia. Alitaka kuwakaribisha watoto hawa kwenye familia ya Mungu.

Watoto wamekataliwa kwenye familia zao na wakapata familia kwenye magenge, walipokelewa pale lakini siyo jambo la kudumu. Magenge mabaya ni hatari kwa watoto kuwa sehemu yao.

Kila mtu anatamani kuwa sehemu ya familia na Mungu anasema watu wote wanakaribishwa kuwa sehemu ya familia yake! Vikundi vya Uzima inaweza kuwa njia ya kujenga familia kati ya watu tofauti na kuonyesha upendo na kukubalika na kila mtu ndani ya kijiji.

Familia ya Mungu ni kabila na sisi sote tunaweza kuwa sehemu yake.  Mwanafunzi wa Yesu Yohana aliandika maelezo jinsi mbinguni ilivyo kwenye kitabu cha Ufunuo.

> [1]*Kisha nikaona mbingu mpya na nchi mpya; kwa maana mbingu za kwanza na nchi ya kwanza zimekwisha kupita, wala hapana bahari tena.* [2]*Nami nikauona mji ule mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu, umewekwa tayari, kama bibi-arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe.* [3]*Nikasikia sauti kubwa kutoka katika kile kiti cha enzi ikisema, Tazama, maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao.* [4]*Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita.*
>
> *Ufunuo 21:1-4*

Kifungu hiki kinazungumzia juu ya Mungu akikaa na watu wake, hii ina maana kuwa Mungu yuko na watu hao walimwamini Yesu na wako ndani ya familia yake.

Yohana pia anazungumzia juu ya mbingu mpya na nchi mpya, namna ya kale ya kufanya vitu itapita. Biblia inatufundisha kuomba kwamba mbingu zije duniani. Tunaweza kuomba kwamba umoja wa mbinguni uje, uwepo vjijini mwetu na zaidi. Mbinguni hakuna makabila tofauti, rangi tofauti, tofauti za dini, tajiri au maskini, lakini kila mtu anakaribishwa kuwa sehemu ya familia ya Mungu – kabila mpya. Hivyo tunaweza kuomba kwamba familia ya Mungu duniani ilete namna hii ya umoja na mambo ya zamani ya kufanya vitu itabadilika.

**Maswali: Familia ya Mungu**

- Unafikiri watu watapokeaje kujifunza kuwa wote ni sehemu ya kabila la Mungu?
- Kikundi cha Uzima itasaidiaje kijiji chako kuwa familia moja?
- Kikundi cha Uzima vitashindaje baadhi ya matengano uliyotambua ndani ya kijiji chako?
- Unataka kumwalika nani kwenye Kikundi cha Uzima ili waweze kutambua kuwa wanaweza kuwa sehemu ya familia ya Mungu?



*“Nililelewa kwenye familia yenye upendo na yenye kujali. NilidhaniKila mtu alilelewa hivyo. Nilipoongeza miaka niligundua kuwa kulikuwa na watu wengi ambao hawakuwa na familia ama familia zao hazi kuwapenda. Hii ilinihuzunisha sana. Niliposikia kuwa wote tunaweza kuwa sehemu ya familia ya Mungu nilitaka kumkaribisha kila mtu kwenye familia ya Mungu. Nadhani baadhi ya watu kwenye makanisa wanafikiri kuwa Mungu anawataka watu maalum, au watu matajiri, ama watu wa dini. Lakini Mungu anawataka wat wote! Nilipowaambia Kikundi change cha Uzima juu ya jambo hili, wiki iliyofuata tulienda na kuwakaribisha hao wote wasio kuwa na familia ndani ya kijiji, na wasiodhaminiwa, au walio puuzwa. Walikuja kwenye Kikundi chetu cha Uzima tukawaonyesha upendo Na kuwaambia juu ya familia ya Mungu – wote walitamani kujua zaidi!” –* ***Agnes***

**Kufanya Wiki Hii**
Wiki hii panga muda wa kukutana na watu hao waliokubaliana na wewe kuanzisha kuanzisha Kikundi cha Uzima. Chukua muda kuomba na kuzungumzia ni nani Mungu anakuelekeza kumpenda kwa kuanzisha Kikundi cha uzima. Fikiri juu ya vikundi vya watu ndani ya jumuia yako waliodidimizwa na kutodhaminiwa, fikiri juu ya watu wasiomjua Yesu. Mwombe Mungu akuonyeshe ni nani anataka kumwalika kwenye famila yake kupitia Kikundi cha Uzima.

Zungumza na kuomba juu ya sehemu nzuri ya kukutania kama kikundi. Unatakiwa kufikiri juu ya eneo ambayo itakuwa salama kwa watu hao na kuwaridhisha.

Kufanya chaguzi hizi inakutaka wewe kujitoa sadaka. Mwombe Mungu akusaidie kuwaona hao watu na akikuonyesha akupe na hisia kali kuunda jumuia kwa ajili yao.

Uliza kikundi kama watapenda kukutana tena wiki inayofuata kujadili mnavyoweza kushirikiana kufanya pamoja.

Tazama kitabu chako cha kazi kutafuta kazi zingine za kukamilisha wiki hii toka kwenye somo hili.

**Andika Chini**
- Kufanya kazi pamoja, uliamua kumkaribisha nani kwenye Kikundi cha Uzima?
- Umechagua wapi mahali bora pa Kikundi cha Uzima kukutania na lini? Kwa nini umefanya uamuzi huu?

**Wiki hii, panga kuzungumza na mtu wako wa mawasiliano**
- Waambie ni nani umemwalika kukusaidia kuanzisha Kikundi cha Uzima.
- Waambie juu ya vitu ulivyovijifunza na namna vinavyoweza kusaidia jumuia yako.
- Andaa swali lolote utakalokuwa nalo kwo kuhusu Dignity ama kuanzisha Kikundi cha Uzima.

**Shughuli ya ziada**
Shughuli hizi za ziada zitakusaidia wewe kufikiri yale uliyojifunza, na kayaingiza kwenye mazoezi na kupanua uwelewa wako. Hupaswi kufanya shughuli zote za ziada lakini tunakutia moyo ufanye moja au mbili. Unaweza kuchagua moja unayoona itakusaidia au unayofurahia zaidi!

**Uchaguzi 1:** Zungumza na baadhi ya marafiki ambao ni wazazi na tafuta kujua familia zao zinafananaje:
- Ni vitu vipi unavyovifurahia unapokuwa sehemu ya familia?
- Famila inafanyaje kazi vizuri kwa pamoja?
- Je unawakaribisha watu wengine kwenye familia yako? Kwa nini na kwa nini huwakaribishi?
- Ni changamoto zipi unazokabiliana nazo kama familia?
- Watoto wako wanafanana na wewe?

**Uchaguzi 2:** Kama ulishawahi kuwa na mtu ambaye mlishawahi kuwa na jambo la kutokukubaliana, jitoe kukutana na mtu huyo na kuwa na amani naye. Hii inakuhitaji uwe jasiri, inawezekana kuomba msamaha na kusameheana. Hii inwezekana kuwa ngumu lakini ni jambo la muhimu kufanya kama familia.

**Uchaguzi 3:** Mtie moyo mtu ambaye hana familia ya kwao, kuwa na muda nao na waelezekuwa wanaweza kuwa sehemu ya familia ya Mungu kiroho. Washuhudie injili toka Soma la 3.



# CHOMBO CHA KAZI: Kuwatayarisha Watu wa Mungu

I Kule Kaskazini Mangaribi mwa Zambia kuna mji na vijiji vikubwa vya Mwinilunga. Hii ni mojawapo ya Mikoa ambayo wamisionari wa kwanza wa Kikristo ndani ya Zambia waliweka makao yao. Zaidi hivi karibuni, makao yao au vituo vya misioni wamekuwa wenyeji wa wamisionari wa Zambia na wamisionari wa kimataifa walioendesha miradi mingi kwenye miji na vijiji vilivyowazunguka. Zahanati zimejengwa, visima vya maji vimechimbwa na makongomano ya Wakristo zilifanyika, na haya yote ni kuwatumikia watu wa Mwinilunga. Watu walisafiri kuhubiri, wakiwatambulisha watu kwa Yesu na kuanzisha makanisa mapya.

Kuzungumza na kikundi cha waanzilishi wa makanisa walifunua kitu kilichoshangaza. Pamoja na kazi kubwa na mafanikio waanzilishi hao wa makanisa walivunjwa moyo. Walisema kwa pamoja, "Kila tulichokifanya hakikudumu! Tunaenda sehemu, tunaona mabadiliko ghafla zinasimama. Muundo msingi zinachakaa. Watu wanaondoka. Kazi tunayofanya siku zote hufa!"

Kama ni msaada maalum au kuhubiri injili, karibu linavunja moyo kwa uchunguzi toka kwa hao waliojitoa uzima yao kutumikia mkoa huo. Tatizo ni dhahiri. Kazi walioifanya haikudumu kwa sababu ya matatizo mawili. Jambo la kwanza, watu wa kawaida wa vijijini hawaijui injili na hawawezi kufundisha wao wenyewe na la pili, hawana mwongozo wa kuwasaidia kufundisha. Kwa miaka, kazi ya umisionari kaika bara la Africa wamekuwa na hadithi zinazolingana.

Suluhisho ni rahisi ila bado ni kubwa. Mungu amewachagua watu kuwa miti mikubwa ya haki ndani ya jumuia zao. Kazi yetu ni kuwaandaa na kuwawezesha watu hawa kuendelea na kazi ya kuhubiri injili, kuwafanya wanafunzi na kuwa badiliko la Mungu ndani ya jumuia zao. Biblia inazungumzia jambo hili kwenye kitabu cha Waebrania 13:20-21:

> *20 Basi, Mungu wa amani aliyemleta tena kutoka kwa wafu Mchungaji Mkuu wa kondoo, kwa damu ya agano la milele, yeye Bwana wetu Yesu, 21 awafanye ninyi kuwa wakamilifu katika kila tendo jema, mpate kuyafanya mapenzi yake, naye akifanya ndani yetu lipendezalo mbele zake, kwa Yesu Kristo; utukufu una yeye milele na milele. Amina.*

Maandiko haya ni maombi kwa watu wa Mungu. Kila mtu binafsi anayemfahamu Mungu anaitwa kubeba mapenzi ya Mungu. Moyo wa Mungu kwenye jumuia zetu ni kuona watu wamemgeukia na jumuia kufahamu upendo wa Mungu kwa kila hali. Anataka kuwaona wototo wake, kama kioo, ikirudisha sura kwenye uzima yao kuwahudumia majirani zao na kuwafikia waliopotea.

Kufanya jambo hili watu wanapaswa kuandaliwa. Wanahitaji kukua ndani ya mahusiano yao binafsi na Mungu, kuifahamu Biblia, na kufahamu wito wao. Wanapaswa kuwa sehemu ya mwili wa waaminio, familia, ili kufanya

jambo hili. Mali na vitu ambavyo Vikundi vya Uzima vinatoa kwa vitu wanavyovihitaji kufanikiwa kama waamini. Hii inafanya badiliko kwa kila mtu.

Mali yeyote ambao Dignity inatumia inatoa mafundisho ya Biblia na msingi imara kwa kila mtu anayependa kufikia jumuia. Wamezungukwa na wanafunzi wanaofikia kumjua Yesu na kuruhusu uzima yabadilishwe na yeye. Kutumia hazina ya Dignity ndani ya Vikundi vya Uzima inawapa watu njia ya kufanya haya pamoja kwa undani zaidi. Kuwafanya wanafunzi inaweza kufanyika kwenye eneo lako.




***Misingi*** ndiyo kiini cha hazina yetu inayowafanya watu kukua kwenye mahusianao yao na Mungu na kuwatia moyo kuhudumia jumuia zao. ***Misingi*** ni seti ya vitabu vinne, kila kimoja inayo mafundisho ya vipindi kumi na tatu vya Biblia ya kujifunza kwa pamoja na kutumia vifungu vya kukariri, hadithi, michezo na shughuli mbalimbali za kusaidia Vikundi vya Uzima kujua maana ya kuishi na Yesu. ***Misingi*** iliandikwa na watu waliojitolea wageni waandishi toka sehemu mbalimbali duniani na kuwekwa pamoja na kuhakikiwa na Dignity.

Tunatumia pia hazina inayofanana ambayo imetafsiriwa kwa mapana inayoitwa kuweka ***Mizizi Ndani ya Yesu***, (www.rootedinjesus.net). Tunaamini kuwa ni muhimu hasa watu kumjua Mungu kwa lugha yao. Mali hizo zote mbili humsaidia kila mwanakijiji kufikia na kuwafundisha watu na kuunda kikundi chao wenyewe.




***Panda*** ni hazina nyingine inayoweza kutumika na mtu yeyote, kutoa utambulisho wenye nguvu namna ya kuanzisha Kikundi cha Uzima. Inatoa mwanga wa kwa nini Vikundi vya Uzima ni wazo lenye nguvu na namna na kuanzisha na kuendesha Kikundi cha Uzima. Kama unataka kiongozi wa kumpa mtu fulani, hii ni hazina kubwa kutumia. Kama unaendesha Kikundi cha Uzima kwenye kijiji chako au unatafuta kuanzisha moja hapo karibu, tumia ***Panda*** kama kiongozi chako na kuwashuhudia wengine.




***Penda Yako…*** ni seti ya mtiririko wa mafundisho ya Biblia kwa mtazamo wa kuenda kwa matendo. Yesu alituambia tumpende Mungu na kupenda majirani zetu. Kanuni hii inapaswa iwe ndani ya moyo wa kila Kikundi cha Uzima. Hutuwezi tu kirahisi kusema sisi ni Wakristo, tunapaswa kupenda na kuishi kama Yesu alivyoishi. Kwa sasa vipo vitabu viwili katika mtiririko, ***Penda Kijiji Chako*** kinacho onyesha namna ya kupenda kijiji chetu, na ***Penda Watoto Wako*** ambayo inaonyesha mahali na umuhimu wa kuwafikia na kuwaangalia watoto ndani ya jumuia zetu.

Kwa kuwafikia watu na ujumbe wa Yesu, kuunda Kikundi cha Uzima na kuwatuma watu, tunafanya kazi ya Mungu kwenye maeneo yetu. Hazina hizi zitatusaidia sote kutuandaa kwa jambo hili. Kwa kuvitumia, utawatia watu nguvu kwenye eneo lako kuwa sehemu ya kazi inayokwenda mbali zaidi yako, na cha kudumu.



**Fikiri juu yake**
Kumbuka kuandika majibu yako kwenye kitabu chako cha kumbukumbu.

- Ni yapi mahitaji ya watu ndani ya Kikundi chako cha Uzima na kijijini? Ni vifaa gani unafikiri itakuwa vizuri kutumia ndani ya kikundi kwa muda huu?
- Kwa nini kuwaandaa watu kwa njia hii ni tofauti na yale ambayo kwa kawaida ndani ya kanisa? Unaweza kufikiri sababu inayosababisha kudumu na kuenea mbali?
- Utaenda kuhitaji nakala ya ***Misingi*** utakapoanza Kikundi cha Uzima mapema. Kama huna nakala ya ***Misingi*** unaweza kuzungumza na mtu wako wa mawasiliano au mtu wa Dignity anayejitolea. Kwa namna nyingine, Unaweza kuwasiliana na Dignity tovuti hello@dignityonline.org.uk au WhatsApp kwa no +447340573937.

# 5



# Kila mmoja anayo Mahali

Lakini nendeni, mkajifunze maana yake maneno haya, Nataka rehema, wala si sadaka; kwa maana sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi.

Mathayo 9:13

**Lengo**

Kila mtu anayo sehemu ya kutumika kwenye familia, kila mmoja ana jambo la kufanya ambalo kila mmoja atafaidi na unaweza kuwa mtu wa kuwasaidia watu kutambua jambo hili.

**Mwisho wa somo hili utakuwa na:**

- Umefahamu nini maana ya 'Mwili wa Kristo'
- Umefahamu kuwa wote waliyo ndani ya Yesu Kristo ni sawa na kila moja Amepewa kipawa chake cha kutumia
- Jifunze namna Kikundi cha Uzima vinavyofanya kazi kwa matendo ndani ya vijiji vyao

**Tazama Nyuma**

Kila mwanzo wa kila somo tunataka kukutia moyo utazame nyuma kwenye somo lililopita na ufikiri yale uliyoyafanya na yale ambayo Mungu amekufundisha.

- Ulijifunza nini kwenye somo lililopita juu ya uzima kama familia?
- Umezungumza na familia yeyote wiki hii? Umejifunza nini juu ya kuwa sehemu ya familia?
- Umeshuhudia yale uliyoyajifunza kwa mtu yeyote wiki hii?

**Hadithi: Kabichi Kubwa**

**Ikiwa unajifunza pomoja na kikundi**

Unapohadithia hadithi hii mchukue mtu mmoja wa kujitolea kuigiza nafasi hii ya mkulima. Mwalike huyo anayejitolea kusimama sehemu Fulani ambako kila mtu atamwona na kujifanya kung'oa kabichi toka ardhini. Mwambie huyu mtu wa kujitolea aende amchague mtu wa kuigiza sehemu ya mke wake. Huyu mtu mwingine wa kujitolea anaweza kumchagua mtu wa kuigiza sehemu ya kijana na kuendelea hadi mwisho wa hadithi wakati mtu mwingine anakuwa panya! Kuigiza sehemu zote itawasaidia watu kufahamu kinachoendelea na itafurahisha pia. Ifuatilie hadithi, mwache kila mtu aigize sehemu wakati mnavyoendelea.

Kama watu wanaojitolea wanafurahia, ni vizuri kusimama nyuma ya mkulima kwa mstari na kila mmoja ashiki kiuno ya mtu aliye mbele yake. Hii itaonyesha kuwa mnavuta kwa pamoja.

Kulikuwepo na kabichi kubwa ndani ya ardhi. Ilikuwa pana sana kiasi cha kwamba mkulima hakuweza kusubiri zaidi kuitoa na kuuza kwa fedha nyingi.

Mkulima alienda kung'oa kabichi toka kwenye ardhi. Alijitahidi kuvuta na kuvuta na kuvuta. Aliivuta kwa nguvu zake zote – lakini HAKUNA! Hakuweza kung'a kabichi hiyo.

Mkulima akawaza nani wa kumsaidia. "Nitenda kumwita mke wangu," alijisemea.

Mkulima na mkewe wakavuta na kuvuta na kuvuta. Lakini kabichi haikuweza kung'ooka. Hivyo wakaenda kumwita kijana wao.

Mkulima, mkewe na kijana wake wakavuta na kuvuta na kuvuta. Hata hivyo kabichi haikung'ooka. Hivyo wakaenda kumchukua binti yao.

Unaweza ukafikiri juu ya watu hawa wote kwenye jua kali wakijaribu kung'oa kabichi hii kubwa?

Mkulima, mkewe, kijana na binti yake wakavuta, wakavuta na kuvuta lakini haikung'oka. Walitokwa na jasho, jua kali na hawakujua la kufanya tena!

Baadaye mkulima akawakumbuka wanyama! Akaenda kumchukua mbwa kuja kusaidia.

Mkulima, mkewe, kijana, binti na mbwa wakang'oa na kungoa na kungo'a, lakini kabichi haikusogea hata kidogo!

Hivyo mke wake akaenda kumleta paka.

Mkulima, mke wake, kijana, binti, mbwa na paka wajaribu tena kung'oa na kung'oa na kung'oa wasiweze kuvuta zaidi. Walishakata tama! Baadaye kijana akawa na wazo la kumwita panya. Mkulima alicheka sana kwa sababu alifahamu kuwa panya mdogo hawezi kuleta msaada wowote lakini kwa vile hakuwa na wazo bora mbadala, wakaenda kumleta panya.

Kwa hiyo sasa Mkulima, mkewe, kijana, binti, mbwa, paka NA panya wakajaribu kuvuta na kuvuta na kuvuta. Kabichi ikaanza kusogea, ikaanza kuyumba na kuachia, ghafla kwa 'kishindo' iling'ooka.

Kwa msaada wa panya mwishowe walifaulu kung'oa kabichi.

**Maswali: Kabichi Kubwa**

- Unnafikiri hadithi ya Kabichi Kubwa inatufundisha nini?
- Kwa nini mkulima alijaribu kung'oa kabichi mwenyewe?
- Mkulima alitarajia nini walipomwomba panya kusaidia?
- Nani alikuwa na nguvu mtu au panya?
- Kwa msaada wa nani kabichi iling'ooka mwishoni? (Mtazamo: jibu haliko Kwenye herufi yeyote kwenye hadithi!)

**Vifungu vya Biblia**

Barua kwa makanisa ya Wagalatia na Wakorintho yaliandikwa na Mtume Paulo. Kwa barua zake, umoja, kufanya kazi pamoja na usawa ni wazo ambalo amelitaja kila wakati. Hii ina maana kuwa ni mambo ya muhimu sana. Ni muhimu sana kusoma nyaraka hizo zote kamili. Unaweza kutaka kulinganisha maandiko ya Wagalatia na Kabichi Kubwa tuliosoma. Waraka kwa Wakorintho inafuata nyuma kutoka hii.

> *[26]Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa Mungu kwa njia ya imani katika Kristo Yesu.*
> *[27]Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo. [28]Hapana Myahudi wala*
> *Myunani. Hapana mtumwa wala huru. Hapana mtu mume wala mtu mke. Maana ninyi*
> *nyote mmekuwa mmoja katika Kristo Yesu. [29]Na kama ninyi ni wa Kristo, basi, mmekuwa*
> *uzao wa Ibrahimu, na warithi sawasawa na ahadi.*

*Wagalatia 3:26-29*

> *[12]Maana kama vile mwili ni mmoja, nao una viungo vingi, na viungo vyote vya mwili ule,*
> *navyo ni vingi, ni mwili mmoja; vivyo hivyo na Kristo. [13]Kwa maana katika Roho mmoja sisi*

*sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja, kwamba tu Wayahudi, au kwamba tu Wayunani; ikiwa tu watumwa au ikiwa tu huru; nasi sote tulinyweshwa Roho mmoja. [14]Kwa maana mwili si kiungo kimoja, bali ni vingi.*

*[15]Mguu ukisema, Kwa kuwa mimi si mkono, mimi si wa mwili; je! Si wa mwili kwa sababu hiyo? [16]Na sikio likisema, Kwa kuwa mimi si jicho, mimi si la mwili; je! Si la mwili kwa sababu hiyo? [17]Kama mwili wote ukiwa jicho, ku wapi kusikia? Kama wote ni sikio ku wapi kunusa? [18]Bali Mungu amevitia viungo kila kimoja katika mwili kama alivyotaka. [19]Lakini kama vyote vingekuwa kiungo kimoja, mwili ungekuwa wapi? [20]Lakini sasa viungo ni vingi, ila mwili ni mmoja.*

*[21]Na jicho haliwezi kuuambia mkono, Sina haja na wewe; wala tena kichwa hakiwezi kuiambia miguu, Sina haja na ninyi. [22]Bali zaidi sana vile viungo vya mwili vidhaniwavyo kuwa vinyonge zaidi vyahitajiwa zaidi. [23]Na vile viungo vya mwili vidhaniwavyo kuwa havina heshima, viungo vile twavipa heshima zaidi; na viungo vyetu visivyo na uzuri vina uzuri zaidi sana. [24]Kwa maana viungo vyetu vilivyo na uzuri havina uhitaji; bali Mungu ameuungamanisha mwili, na kukipa heshima zaidi kile kiungo kilichopungukiwa; [25]ili kusiwe na faraka katika mwili, bali viungo vitunzane kila kiungo na mwenziwe. [26]Na kiungo kimoja kikiumia, viungo vyote huumia nacho, na kiungo kimoja kikitukuzwa, viungo vyote hufurahi pamoja nacho. [27]Basi ninyi mmekuwa mwili wa Kristo, na viungo kila kimoja peke yake.*

*[28]Na Mungu ameweka wengine katika Kanisa, wa kwanza mitume, wa pili manabii, wa tatu waalimu, kisha miujiza, kisha karama za kuponya wagonjwa, na masaidiano, na maongozi, na aina za lugha. [29]Je! Wote ni mitume? Wote ni manabii? Wote ni waalimu? Wote wanatenda miujiza? [30]Wote wana karama za kuponya wagonjwa? Wote wanena kwa lugha? Wote wafasiri? [31]Takeni sana karama zilizo kuu. Hata hivyo nawaonyesha njia iliyo bora.*

*1 Wakorintho 12:12-31*

**Mafundisho: Sote tunayo nafasi ya utendakazi**

Kila mmoja wetu anayeishi kijijini na anamjua Yesu, anaweza kutumia na Yeye kufanya mambo ya ajabu. Kuna imani kwamba ili umtumikie Mungu lazima uwe na ujuzi, mchungaji au mwinjilisti. Kuna imani nyingine kwamba washirika wa kwaida hawaruhusiwi kufanya kazi za Mungu katika jamii zao. Jambo hili halina ukweli wowote!

Hebu tuwaze juu ya vifungu katika kitabu cha Wagalatia ambayo tayari tumevisoma. Lengo la vifungu hivi vinasema kwa vile sote tuna Bwana mmoja Yesu Kristo basi pasiwepo na mgawanyiko kati yetu. Ikiwa ni kabila, umuhimu, rangi, elimu n.k. Sisi wote tuko sawa mbele za Mungu. Mchungaji hawezi kwa urahisi tu kuambia kusanyiko lale jambo la kufanya, mamlaka yake yasiwe hivyo. Mtu aliye tajiri kwenye kusanyiko hana sauti juu ya mtu maskini. Kwa kuwa ukweli ni kwamba wote tu sawa hii ina maana kuwa tuendeshe makanisa yetu na Vikundi vya Uzima kwa tabia ya kuwahudumia watu wote sawa.

Mtume Paulo anatumia Mwili kutusaidia kuelewa somo hili. 1 Wakorintho 12:12-31 ni maelezo ya Mwili wa Kristo. Kila mtu, kila sehemu ni muhimu kuendesha mwili vizuri.

**Maswali: Sote tunayo nafasi ya utendakazi**

- Kama sisi wote ni sehemu ya mwili, hii ina maana gani kwa makanisa yetu?
- Hii ina maana gani wakati tunapofikiria kuanzisha Kikundi cha Uzima?

- Je watu wa 'kawaida' wanaweza kufanya mambo ya kushangaza ya Mungu au unahitajika kuwa mtu 'maalum'?
- Kwa nini hakuna mgawanyiko kati ya watu wanaomfuata Yesu?

**Mafundisho: Hakuna mtu anayepaswa kutengwa**
Ukweli wa ajabu katika waraka kwa Wakorintho ni kwamba viungo dhaifu vilivyoonekana kutokuwa na heshima vilipewa heshima zaidi. Hii ina maana kuwa viungo vile tunavyoviona dhaifu au kudharauliwa, Mungu yeye anaviheshimu. Jinsi Mungu anavyowafikiria watu ndani ya vikundi vyetu na vijiji ni tofauti sana na jinsi sisi tunavyowafikiria. Mtazamo wetu ni tofauti sisi tunawaangalia watu wa muhimu kwanza.

Kidole kidogo cha mguu kinaweza kuonekana kuwa hakina umuhimu wowote. Unaweza kuamini kuchukua panga na kukikata kuondoa na hakutakuwepo na tofauti yeyote. Utakuwa umekosea sana. Bila kidole hicho kidogo ni vigumu kuwa na uwiano. Watu waliopoteza vidole vyao vidogo ilibidi kujifunza kutembea tena.

Vipi juu ya kidole chako kikubwa? Siyo sehemu kubwa au yenye nguvu kwenye mwili. Hata hivyo, ukipoteza hutaweza kuinua kitu juu na kutumia. Hata ingawa ni kidogo ni cha muhimu sana!

**Sote tunapaswa kutumia karama zetu**
Kuwa na usawa na Kristo akiwa kichwa, inamaanisha sote tuna karama na vipawa ambavyo vya kutoa mchango wetu. Tukiangalia hadithi ya Wakorintho tunaona mifano kama:

- Mitume
- Manabii
- Waalimu
- Miujiza
- Uponyaji
- Masaidiano
- Uongozi
- Kunena kwa ndimi

Kuna karama nyingi zaidi zimetajwa katika Bibilia. Katika orodha hiyo Paulo anapeana mfano kwa kanisa la Wakorintho. Anauliza ikiwa yupo mmoja anayeweza kufanya haya yote? Jibu ni la!

Vivyo hivyo tunahitajiana na karama ambazo kila mmoja amepewa na Mungu ametupa. Tukiwa kwa ushirikiano tutakuwa na nguvu na tunaweza fanya zaidi na kwa uzuri zaidi.

**Walio nje ya Kanisa hawafai kuachwa nje!**

**Maswali: Hakuna mtu anayepaswa kutengwa**

- Kila mtu analo jambo la kufanya na kila mmoja ni wa muhimu kwa Mungu, hii ina maana gani kwa watu walio nje ya kanisa?
- Je watahudumiwa kama watu wa nje ama watatiwa moyo wawe sehemu ya familia?

**Vifungu vya Biblia**
Mathayo aliandika matukio ya uzima ya Yesu kwa ajili yetu ili tuweze kufahamu yaliyokuwa ya muhimu Kwake. Masomo haya ni mfano namna Yesu alivyowakumbatia waliokuwa nje ya watu wa Mungu na akawa na muda nao. Hili ni jambo la muhimu sana kwa Mungu.

*9 Naye Yesu alipokuwa akipita kutoka huko aliona mtu ameketi forodhani, aitwaye Mathayo, akamwambia, Nifuate. Akaondoka, akamfuata.*

*10 Ikawa alipoketi nyumbani ale chakula, tazama, watoza ushuru wengi na wenye dhambi*
*walikuja wakaketi pamoja na Yesu na wanafunzi wake.*
*11 Mafarisayo walipoona,*
*waliwaambia wanafunzi wake, Mbona mwalimu wenu anakula pamoja na watoza ushuru*
*na wenye dhambi?*

*12 Naye aliposikia, aliwaambia, Wenye afya hawahitaji tabibu, bali walio hawawezi.*
*13 Lakini*
*nendeni, mkajifunze maana yake maneno haya, Nataka rehema, wala si sadaka; kwa maana*
*sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi.*

*Mathayo 9:9-13*

**Mafundisho: Kuwakaribisha watu wa nje**

Mara nyingi katika Ukristo na Kanisa, tunakaa mbali na wale tunaowaona ni wenye 'dhambi'. Tunaamini kuwa tunapaswa kujitenga nao. Tunaamini ya kuwa baadhi yao ni watu waovu na wakati mwingine wanaweza kutupoteza kama tukishirikiana pamoja nao. Hii si kweli na hayakuwa mafunzo ya Yesu.

Katika mfano huu Yesu alikula na watoza ushuru na wenye dhambi. Watoza ushuru walihesabiwa kama watu waovu sana. Mahali alipoishi, ambayo sasa inajulikana kuwa ni Israel, ilitawaliwa na majeshi ya Warumi. Watu walichukia jambo hili. Watoza ushuru waliwafanyia Warumi kazi, wakikusanya fedha na kuwapa Warumi. Wakati wote waliwalaghai na kula rushwa na kutunza fedha nyingi kwa ajili yao wenyewe. Walikuwa miongoni mwa kikundi cha watu waliochukiwa sana katika Palestina. Hata hivyo Yesu aliienda nje ya njia yake na kutumia muda wake pamoja nao.

Hatukukusudiwa kuwa kila moja ni sawa na mwingine. Tulikusudiwa kuwa ni wenye kuwakaribisha wale walio nje kujiunga nasi. Tunawaalika watu wawe pamoja nasi na Yesu. Vikundi vyetu vya Uzima vinapaswa kuwa huru kwa KILA MMOJA na yeyote katika jamuiya, pasipo kuzingatia wao ni kina nani na haijalishi wamefanya nini.

Yesu hakuja kwa wale Wanaomjua, bali kwa wale Wasiomjua. Tunapaswa kutenda vile.

**Maswali: Kuwakaribisha watu wa nje**

- Ni watu wa aina gani kwa kawaida wanatengwa au kuwekwa kando ndani ya kijiji chako?

*"Kulikuwa na kikundi cha watu kimeketi kando mto siku nzima wakinywa, hakuna mtu aliyewakaribia na wakawadharau. Nilipomuuliza Mungu ni nani wa kumwalika kwenye Kikundi cha Uzima nilijisikia kwenda na kuzungumza nao. Sikutaka kufanya hivyo mwanzoni kwa sababu walikuwa harufu mbaya na nikajiuliza watu wengine watanifikiriaje. Lakini nilijua Mungu anawapenda na anataka kuwakaribisha kwenye familia yake. Hivyo nikaenda na kukaa nao kwa muda wa saa moja, niliwauliza juu ya uzima yao nao wakanishuhudia kwa uchungu jinsi walivyokataliwa. Nikawaambia kwamba Mungu anayo sehemu kwa ajili yao kwenye familia yake na kama wangependa kusikia zaidi watapata kwenye Kikundi chetu cha Uzima. Wote walipendezwa! Wamekuwa wakija kila wiki, walichangia hoja, kila mtu*

*aliwakaribisha, nao wametaka kuishi na Yesu, na kuachana na kilevi na wakawasaidia wanakijiji wengine pia!"- **Agnes***

**Hadithi: Kila mtu Kutumia Kipawa Chake**
Hadithi hii inaonyesha jinsi Kikundi cha Uzima inavyoweza kufanya kazi. Inaonyesha pia jinsi vipawa tofauti vya watu inavyotia moyo vinavyotumika kwa pamoja na namna inavyoweza kufanya uzima na kufanya kazi ya huduma kuwa imara.

**Ikiwa unajifunza pomoja na kikundi**
Waambie watu wa kujitolea wawili kuja mbele, mwanamume na mwanamke. Eleza kuwa watu hawa wawili wameamua kuunda Kikundi cha Uzima ndani ya kijiji chao, majina yao sasa ni Nyirenda na Masiye.

Waambie watu hao wa kujitolea wawachukue watu wengine sita, ambao watakuwa ni kikundi chao. Wote ni lazima wasimame mbele kwenye mstari, wakitazama kikundi.

Soma hadithi na maigizo na mtambulishe kila mwanakikundi, waambia waigize kutumia vipawa walivyonavyo.

Nyirenda na Masiye walioana kwa miaka 5 na wana watoto 4. Wanaishi kwenye kijiji cha Mabanga na wameishi uzima yao yote hapo. Waliwapenda watu ndani ya kijiji, bado ni jambo la dhahiri kwao kwamba mambo yanahitaji mabadiliko. Watu walipuuzwa vijijini mwao, na waliachwa na watu wakawa wanagombana. Wakasikia Kikundi cha Uzima inavyosaidia jumuia kwenye kijiji cha jirani wakaamua kuanzisha kimoja wenyewe. Walizungumza na marafiki zao juu yake, wakapenda wazo hilo. Wakawakaribisha watu wachache tofauti toka makanisa tofauti na jumuia kubwa. Baada ya miezi 6 kikundi kikaongezeka idadi, watu wakija toka makanisa tofauti na hata watu watatu wasiokwenda kanisani! Kila mtu akakua kwenye ufahamu wa Kimungu na kuwapenda wengine. Walianza kufanya kazi kubwa ndani ya kijiji kumsaidia kila mtu.

Wapo watu 16 kwenye Kikundi cha Uzima. Unaenda kukutana na wachache wao sasa…

Faith na Beatrice ni wamama wenye watoto watatu kila mmoja, wamekuwa marafiki wazuri ingawa wanaenda makanisa tofauti. Nyirenda na Masiye walitambua kuwa wao wamekuwa watu wazuri kwa kuzungumza na kuwafundisha watoto. Waliwatia moyo kufikiri namna wanavyoweza kusaidia watoto wasiojihusisha na kanisa. Faith na Beatrice walipendezwa kwamba wanaweza kufanya mabadiliko ndani ya uzima ya watoto wengine. Waliamua kuanza kuwafundisha watoto juu ya Yesu, waliwafanya watoto kuigiza hadithi na kujihusisha na michezo ya vichekesho kuwafundisha watoto! Haya yametokea kwa sababu walitiwa moyo kutumia vipawa vyao kwenda kufanya jambo fulani.

Thandiwe ni mzee aliyefiwe na mke. Anafurahia kuzunguka kijijini akimsalimia kila mtu. Kikundi cha Uzima kilipokutana Thandiwe alielewa mafunidsho haraka na akafurahia kuwaeleza watu wengine yale aliyoyajifunza. Hata ameshajaribu kufanya majaribio machache kuongoza mafundisho na akafurahia sana! Nyirenda na Masiye wamemwambia wanafikiri Mungu amempa kipwa cha kufundisha na wamemtia moyo kwenda kwenye kijiji cha jirani na kuanzisha Kikundi cha Uzima hapo, kuwafundisha watu wengine.


Elijah ameshakuwa mtunza bustani kwa uzima yake yote na anayo bustani nzuri yenye kutoa mavuno mazuri. Charles ni kijana wake na pia anafurahia kazi za bustani. Wote wawili wanahudhuria kanisani hapo kijijini. Walimkaribisha rafiki yao Royd kujiunga na Kikundi cha Uzima, yeye haendi kanisani lakini anataka kusaidia kijiji na anapenda kazi za bustani pia kwa hiyo akaanza kuhudhuria kwenye kikundi chao. Siku moja walipokuwa wakifanya kazi bustanini kwa pamoja wakapata wazo la kuwafundisha watu ustadi wa kutengeneza bustani. Walianza kwa kuwakaribisha watu wachache kujiunga nao na kuwafundisha ustadi wa msingi. Kwa hiyo watu wengi wakafurahia na sasa wameshapata shamba ambalo wote wanaweza kufanya kazi kwa pamoja na kuzalisha chakula cha kuwapa watu maskini. Baadhi ya watu waliofundishwa wameanza kuhudhuria Kikundi cha Uzima na wanataka kufahamu mengi zaidi kuhusu Yesu.

Nyirenda na Masiye wametiwa moyo kwamba washirika wa Kikundi cha Uzima wanagundua vipawa ambavyo Mungu amewapa na wanavitumia kufanya kazi ya Mungu ndani ya kijiji!

**Ni muhimu sana kufahamu namna Kikundi hiki cha Uzima kilivyofanya kazi kwa pamoja, kila mmoja akitiwa moyo kutumia vipawa vyao tofauti kuwapenda wale waliowazunguka. Unapaswa kusoma hadithi hii tena kuhakikisha unaielewa.**



*"Kulikuwepo na kijana mdogo aliyeanza kuhudhuria Kikundi chetu cha Uzima, alikuwa mtulivu mwenye wasiwasi. Mwanzoni sikuwa na uhakika ni namna gani ningeweza kumtia moyo kutumia kipawa chake, watu wengine walisema hana kipawa chochote. Lakini Mungu anataka kumtumia kila mtu, hivyo nikamuuliza yale anayopenda kufanya. Akasema anapenda mchezo wa mpira. Nilimtia moyo kumuuliza Mungu namna anavyoweza kutumia upendo wake na ustadi wake wa mpira kushuhudia habari za Yesu. Wiki chache baadaye aliniambia kuwa ameanzisha timu ya mpira, aliwaalika vijana na wasichana wa umri mdogo toka makanisa tofauti ambao kamwe hawakuwahi kukaa pamoja. Walianza kucheza kila wiki na kila wiki aliwaambia kuwa timu hiyo yao ya mpira ni kama familia ya Mungu maana kila mmoja alikuwa anahusika na kila mtu alikuwa na kipaji cha tofauti. Vijana wawili wameanza kuhudhuria Kikundi chetu cha Uzima kwa sababu ya timu hii ya mpira." **- Asisi***



**Shughuli: Mwili wa Kristo**
Ndani ya kitabu chako cha kumbukumbu, chora picha kubwa ya mtu.

- Andika 'Yesu' ndani ya kichwa
- Andika majina ya watu wengine kwenye sehemu mwili fikiri kuandika kwa namna mtu anavyofanania
- Andika kwa nini umeweka jina la kila mmoja mahali maalum ulikoweka

Kwa mfano, mtu ambaye ni mzuri kulimana anaweza kuwafundisha wengine kulima, andika majina yao kwenye mikono kwa sababu wanafanya kazi kwa bidii shambani. Mtu ambaye ni mzuri kufundisha, andika majina yao kwenye mdomo.

**Ikiwa unajifunza pomoja na kikundi**
Ndani ya kitabu chako cha kumbukumbu, chora picha kubwa ya mtu. Kama kikundi kina kalamu na karatasi waambie wachore viungo vya mwili. Kama siyo, hivyo basi tumia kitabu chako cha kazi. Kama kikundi kufikiri juu ya watu ndani ya kikundi au kwenye kijiji, tafuta vipawa vyao na namna watakavyotumia. Andika majina yao kwenye viungo vya mwili inayowafanania kulingana na vipawa vyao.

Kwa mfano, mtu mzuri kw kulima na anaweza kuwafundisha wengine kulima, andika majina yao kwenye mikono kwa sababu wanafanya kazi ngumu shambani. Mwingine ambaye ni mzuri kwa kufundisha, andika majina yao kwenye mdomo.

**Mafundisho: Pekee tunaweza kufanya ikatokea!**
Kumbuka kuwa sisi ni miti mikubwa ya haki na mawe yaliyo hai. Sisi ni watu ambao Mungu ametuchagua na kutuweka ndani ya vijiji vyetu kuwapenda na kuwasaidia wengine. Kama tunatumaini kuwa watu kutoka nje watakuja na kushughulika na matatizo yaliyomo ndani ya vijiji vyetu, tutasubiri na kusubiri na hakuna ambacho kitatokea. Hii itakuwa ni shida kubwa. Tunatakiwa kukumbuka Mungu ametuumba kuwa akina nani na tunatakiwa kuchukua hatua kuleta uzima wake ndani ya jumuia zetu.

**Kikundi cha Uzima Hadithi**
Chalwe* anaishi Kasempa na ameweza kuanzisha Vikundi 3 vya Uzima, Cha kwanza kilianza 2016 na vingine vikafuata kila mwaka. Anatarajia kutakuwepo na kingine kitaandaliwa mapema.

Alienda kwenye mikutano ya Dignity na akasikia namna Vikundi vya Uzima vinavyoweza kuunganisha vijiji na kuleta mabadiliko. Alirudi kwenye jumuiya yake huku akiwa amejawa na matamanio ya kuanzisha kitu cha ajabu. Akitumia mali zake mwenyewe na ushawishi, alianza kuwakusanya watu kwenye Kikundi cha Uzima.

Elimu ya Faith kwenye jijiji ilikukuwa duni, na watu wakaona kanisa ni mahali pa kwenda mara moja kwa tu. Lakini Vikundi vya Uzima kilipokutana Chalwe akawatia moyo kushuhudiana uzima yao kiroho na magumu ili waweze kusaidiana siku zingine sita zinazofuata katika wiki.

Chalwe anayo kipaji cha kilimo hamu yake ni kutumia kipajii alichonacho kusaidia jumuia na kuwapatia chakula wana kijiji wote. Aliamua kutoa elimu ndani ya Kikundi cha Uzima kuanzia Misingi ya Kilimo. Lengo la wazo kuu ni kujifunza kilimo salama na bora zaidi na kupalilia sehemu ndogo ndogo ili kila mmoja aweze kuwa na chakula cha ziada kwa ajili ya familia, marafiki na wale wenye mahitaji. Vikundi vya Uzima cha Chalwe wamekuwa na tabia sasa ya kila mmoja kuleta lita 5 ya mahindi kwenye kikundi kwa lengo la kuwasaidia watu wakati wa msimu wa mvua.

Kijana mmoja kijini aliyeadhiriwa na kileo na hakuwahi kulima, hivi karibuni alijiunga na moja na Vikundi vya Uzima. Akawa Mkristo na kukaribishwa kwenye familia ya Mungu. Kama sehemu ya familia ya Mungu alitambua pia kuwa na kipawa cha kulima akaanza kupanda mboga zake mwenyewe na kuwagawia majirani zake chakula.

**Majina yamebadilishwa kutunza siri za ndani.*

**Maswali: Kikundi cha Uzima Hadithi**

- Unafikiri hadithi ya Chalwe inatufundidha nini?

- Chalwe alichukua hatua gani?
- Matendo ya Chalwe yalikuwa na adhari gani?
- Ni nini ambacho kingeweza kutokea kama Chalwe hakutumia kipawa chake kuwasaidia wengine?
- Unafikiri Yule kijana alijisikia vipi alipokaribishwa kwenye familia ya Mungu ndani ya Kikundi cha Uzima?

**Omba**

Tunatakiwa kuomba ili Mungu avunje matengano, uasi na kutokusamehe ndani ya kijiji chetu. Pata muda wa kutosha kuombea mambo yafuatayo:

- Omba kwamba Mungu ayakusanye makanis tofauti kupitia kuanzisha Kikundi cha Uzima.
- Omba kwamba kama kuna uasi wowote uliosalia ndani ya kijiji, omba kuwa ifike mwisho.
- Omba kwa ajili ya msamaha mahali inapohitajika kwa matukio yaliyopita ndani ya jumuia.

**Kufanya Wiki Hii**

Wiki hii kutana na wanachama wa kwanza wa Kikundi cha Uzima. Fikiri na mwongee kwa pamoja kuhusu kutenda kwa matendo kila mmoja kutumia kipawa chake kuanzisha Kikundi cha Uzima pamoja. Mtie moyo kila mmoja kwenye Kikundi kufikiri juu ya vipawa na ujuzi, namna wanavyotumia sasa na namna wanavyoweza kutumia kama sehemu ya Kikundi cha Uzima. Kama mtu hajui kipawa chake, uliza kikundi wanafikiri kipwa cha mtu huyo ni kipi. Mtu huyo inawezekana bado hajagundua kipawa chake na kwa mapana atatiwa moyo na kikundi kutumia kipawa chake.

Unaweza kuuliza kikundi maswali haya:

- Kuna mtu aliye mzuri kwa kusikiliza? Labda wanaweza kwenda na kuzungumza na Chifu wa kijiji na kumwambia juu ya Kikundi cha Uzima kuanza, na kumwuliza yale anayoyafikiri na namna kikundi kitasaidia jumuia.
- Kuna mtu yeyote anayejua kupika? Labda wanaweza kupika chakula pamoja na kuwakaribisha watu toka makanisa tofauti, na kushirikisha juu ya kuanzisha Kikundi cha Uzima na kuwauliza kama wanaweza kuwa sehemu ya kikundi.
- Kuna mtu yeyote aliye mzuri juu ya kujenga mahusiano? Labda wanaweza kufikiri ni nani wanaweza kuunganika naye kwenye jumuia na kumkaribisha kwenye Kikundi cha Uzima.
- Kuna mtu yeyote aliye mzuri kwenye mipango? Labda huyu mtu anaweza kukusaidia kupnga vipindi kila wiki kwa Kikundi cha Uzima, wanaweza kukusaidia kuwaeleza watu wengine ni lini na wapi Kikundi cha Uzima kipo na kuhakikisha unacho kila kitu unachokihitaji kwa kipindi.
- Kuna mtu yeyote anayeweza kuongoza mjadala? Labda mtu huyo anaweza kukusaidia kuongoza majadiliano utakapoanza Kikundi cha Uzima na wengine. Waulize kama wangependa kusoma somo lingine ndani ya kitabu hiki pamoja nawe ambalo linaeleza zaidi juu ya kuongoza majadiliano.
- Je kuna mtu aliye mzuri kusimulia hadithi? Labda huyu mtu anaweza kukusaidia kusema hadithi na kuongeza maigizo utakapoanzisha Kikundi Cha Uzima na wengine.
- Je kuna mtu mwenye karama ya ukarimu? Labda anaweza kuwa mtu wa kusaidia kuwakaribisha watu mnapoanzisha Kikundi cha Uzima, wataweza kuongea na hao watu ambao ni wageni na wenye wasiwasi.

Unaweza kuwa na mawazo zaidi ya haya, haya tu ni kukusaidia tu kufikiri namna kila mmoja ataweza kutumia kipawa chake!

Wiki ijayo utakuwa unaanzisha Kikundi cha Uzima kwa kuwakaribisha watu wengine mkitumia hazina iliyoandikwa na Dignity kuongoza vipindi. Waulize wanachama wa mwanzo wa kikundi kuwa tayari kutumia vipawa vyao na kupanga mambo ya kufanyika wiki hii na kuandaa.

Tazama ndani ya kitabu chako cha kazi kutafuta shughuli za kukamisha wiki hii kutoka kwenye somo hili.

**Andika Chini**

- Ulipozungumzia juu ya vipawa vyenu pamoja, nani alikuwa mwepesi kutaja kipawa chake? Ilikuwa vigumu kwa nani? Uliwasaidia kwa namna gani?
- Ikiwa mtu amegundua kipawa chake na namna ya kutumia, Walijisikiaje? Walifurahia? Wamekuwa na wasiwasi? Walishangazwa?
- Andika chini majina ya wanachama wa kwanza wa Kikundi cha Uzima uliyokutana nao. Pembeni ya majina yao andika chini vipawa mlivyojadili kuwa wanavyo kusaidia kuanzisha Kikundi cha Uzima. Unaweza kulinganisha na orodha hii.

**Shughuli ya ziada**

Shughuli hizi za ziada zitakusaidia wewe kufikiri yale uliyojifunza, na kayaingiza kwenye mazoezi na kupanua uwelewa wako. Hupaswi kufanya shughuli zote za ziada lakini tunakutia moyo ufanye moja au mbili. Unaweza kuchagua moja unayoona itakusaidia au unayofurahia zaidi!

**Uchaguzi 1:** Sisi ni watoto wa Mungu na watoto ni kama wazazi wao. Mungu ametuita kufanana naye na kuwapenda wengine. Fikiri juu ya maswali haya:

- Nitayatumiaje macho yangu yafanane na ya Mungu?
- Nitayatumiaje masikio yangu yafanane na ya Mungu?
- Nitatumiaje mdomo wangu ufanane na wa Mungu?
- Nitatumiaje akili yangu ifanane na ya Mungu?
- Nitatumiaje miguu yangu ifanane nay a Mungu?
- Nitatumiaje mikono yangu ifanane na ya Mungu?

**Uchaguzi 2:** Tumia mkono wako kuombea kijiji chako! Andika vitu unavyoviombea kila kimoja juu ya vidole vilivyoorodheshwa hapa chini. Rudia maombi kila siku, ukikumbuka kila kidole ina maanisha nini.

- **Kidole kidogo:** waombee watoto kijijini mwako kwa waonyeshwe upendo na familia zao na kijiji
- **Kidole cha pete:** yaombee makanisa ili kwamba yaanze kufanya kazi kwa pamoja na wakijiona kuwa sehemu kubwa ya familia ya Mungu
- **Kidole cha kati:** mwombee Chifu, ili kwamba waongoze kijiji vizuri na kuhusika kuwaleta watu pamoja.
- **Kidole cha kuonya:** mwombe Mungu akusaidie kuanzisha Kikundi cha Uzima ambayo itakuwa ni sehemu ya familia na upendo
- **Gumba:** waombee hao ambao mara nyingi huachwa, omba kwamba wafanyike sehemu ya familia ya Mungu na waweze kuonyeshwa upendo na kukubalika

**Uchaguzi 3:** Chukua muda Fulani ukipitia kitabu cha ***Misingi 1***. Jizoeze mwenyewe kwa kadri na 'Namna ya kutumia kitabu hiki'. Unaweza kufanya mazoezi kupitia somo la 1 wakati utakapokuwa unafanya hili mapema na Kikundi chako cha Uzima.

6



# Kuendesha Vikundi Vikunda vya Uzima

**Nisalimieni na kanisa lililomo katika nyumba yao.**

Warumi 16:4

**Lengo**

Vikundi vya Uzima ni ya muhimu sana kwa Mungu kufanya kazi ndani ya kijiji chako, inawaleta watu pamoja na kuifanya injili hai! Somo hili litakusaidia kuendesha Kikundi cha Uzima kwa matendo ndani ya kijiji chako.

**Mwisho wa somo hili utakuwa na:**

- Fahamu kuwa vikundi vidogo vinafanya kazi bora zaidi ya kuhubiri
- Jifunze mbinu za namna ya kuendesha vipindi kwenye vikundi vidogo
- Jifunze namna Kikundi cha Uzima kitakavyoweza kukutana kila wiki.

**Tazama Nyuma**

Kila mwanzo wa kila somo tunataka kukutia moyo utazame nyuma kwenye somo lililopita na ufikiri yale uliyoyafanya na yale ambayo Mungu amekufundisha.

- Ulijifunza nini kutoka somo la mwisho juu ya kila mtu kutumia nafasi yake kwenye familia?
- Je ulimtia moyo mtu yeyote wiki hii kwa kuwaambia vipawa unavyofikiri wanavyo na wavitumie kwa ajili ya Mungu? Nini kimetokea?
- Umemshuhudia mtu yeyote yale uliyoyajifunza wiki hii?

**Hadithi: Jumba Limewaka Moto!**

Paliondokea kijiji kimoja ndani ya msitu. Msimu wa mvua ulikuwa umeisha na nyasi kando ya kijiji zilikuwa nyingi. Nyoka na wanyama wengine wengi walijikinga na jua kwa kujificha kwenye nyasi.

Precious na Phiri walikuwa wavulana wawili wadogo kijijini. Mojawapo wa mambo walilopenda kufanya siku kwa siku ni kutega na kushika wanyama wadogo wadogo kama panya. Ili kuweza kuwapata Precious angewasha moto upande mmoja wa msitu na wanyama wote wangetorokea upande wa Phiri ambapo angewakamata. Hii ilikua furaha kwao isiyo na kipimo kwa kufanya jambo hilo na walikamata chakula pia. Kila mara wangepika na kula mawindo yao baadaye!

Mara nyingi Precious na Phiri walitoweka nyumbani Jumapili asubuhi. Waliona ibada ni ya kuchosha na ndefu.

Siku moja Precious na Phiri waliwasha moto, lakini siku hiyo upepo ulikuwa mkali. Baada ya moto kuwaka, upepo ulivuma na kusambaza moto ukawa mkubwa sana zaidi ya siku zote. Kwa muda sehemu yote ya nyasi ikashika moto. Haukuweza kuzuilika.

Precious na Phiri walikimbia huku na kule wakijaribu kuuzima moto lakini wakashindwa kwa sababu ulikuwa ni mkali kuwashinda. Miale ilikuwa mikubwa sana. Muda si mrefu baadhi ya nyumba zikashika moto. Mali za watu zilikuwa hatarini.

Precious na Phiri walikimbia kwenda kutafuta msaada, lakini hapakuwepo na mtu karibu. Wakambuka watu wote wlikuwa kanisani maana ilikuwa jumapili. Walipofika kanisani, mahubiri yalikuwa yameanza. Wanawake walikaa upande mmoja na wanaume upande wa pili wakimsikiliza mchungaji aliyekuwa akihubiri. Precious na Phiri walijaribu kusimamisha mhubiri ili wapeane habari ila walionywa wasisumbue mara kadha. Hakuna aliyewasikiliza.

Hatimaye mchungaji alipochoka na usumbufu aliagiza watolewe nje ya kanisa. Wasaidizi wawili waliwaendea ili kuhakikisha wananyamaza. Hapo ndipo Precious alipaza sauti, “ninyi hamwelewi. Nyumba zenu zinaungua!”. Watu walishtuka na kuchanganyikiwa wakakimbia nje kushuhudia kilchokuwa kinatokea.

Kwa hakika, nyumba nyingi zilikuwa zimeshika moto. Watu kutoka kanisani wakaanza kushirikiana kuzima moto. Walifanikiwa kuokoa baadhi ya nyumba na mali ndani yak. Baadhi ya nyumba zilichomeka pamoja na mali za watu.

Watu walikasirika na kuwauliza, “Kwa nini hamkutuambia?” Precious na Phiri wakaanza kulia. “Tulijaribu,” walisema, lakini hamkusikiliza kwa sababu mlikuwa mnanasikiliza mahubiri. “Ijapokuwa Precious na Phiri walianzisha moto kwa bahati mbaya walisamehewa na watu wakashirikiana kusaidia wale waliopoteza kila kitu. Watu waliapa kusikizana kwa makini kuanzia siku hiyo!

**Maswali: Jumba Limewaka Moto!**

- Unafikiri hadithi ya Precious na Phiri inatufundisha nini?
- Kila mtu alimsikiliza Precious na Phiri? Kwa nini hawakuwasikiliza?
- Mambo yangekuwaje tofauti kama watu wangewasikiliza Precious na Phiri?
- Mambo yangekuaje tofauti kama Precious na Phiri walikuwa na mahali kanisani?

**Mafundisho: Vikundi Vidogo kwenye Bibilia**

Katika Bibilia tunajifunza juu ya Wakristo kukutana pamoja kwenye vikundi vidogo vilivyokutana manyumbani na sehemu zinginezo. Kikundi kidogo ni kama Kikundi cha Uzima tulivyovizungumzia hapo awali. Ni kikundi cha watu wanaokutana kila mara:

- Kusoma na kuchambua Bibilia
- Kushuhudiana na kutiana moyo katika uzima
- Kumkumbuka Yesu na kumega mkate pamoja
- Kuomba pamoja
- Kuwa wakarimu, kutoa pesa na kutenga muda
- Kuabudu pamoja
- Kushuhudia pamoja[5]

Kama tulivyoona haya ni mambo ambayo tunafanya katika Vikundi vya Uzima.

Watu wengi hujiuliza mawazo ya vikundi vidogo vinatoka wapi. Vinatokana na mambo yaliyofanywa na Wakristo wa kwanza tunavyo ona katika Bibilia. Makanisa ya kwanza hayakuwa makubwa watu walikuwa chini ya 50. Barua ya Paulo kwa Wagalatia izawezekana kua iliandikua kwa kwa kikundi kidogo kushinda vile unawaza.

Vikundi vya Kikristo vilikutana manyumbani, nje ya hekalu, na masinagogi (makanisa ya Kiyahudi). Hawakuwa na majengo tuliyo nay oleo. Hakuna jengo la kanisa limetajwa katika agano jipya isipokuwa vikundi vidogo vya watu manyumbani.

[5] Pastors.com/Rick Warren, 2012. *Seven Marks of a Healthy Small Group*, njia ya kufikia 28 June 2017. Inapatikana kwa: http://pastors.com/seven-marks-of-a-healthy-small-group

**Vifungu vya Biblia**

Makanisa ndani ya vitabu vya Warumi na Philemoni vilikuwa Roma nap engine ni kwenye mji wa Wakolosai. Makanisa haya yalikutana ndani ya nyumba za watu, na siyo kwenye majengo ya makanisa.

> *[3]Nisalimieni Priska na Akila, watenda kazi pamoja nami katika Kristo Yesu; [4]waliokuwa tayari hata kukatwa kichwa kwa ajili ya uzima yangu; ambao ninawashukuru, wala si mimi tu, ila na makanisa ya Mataifa yote pia; nisalimieni na kanisa lililomo katika nyumba yao.*
> *[5]Nisalimieni Epaineto, mpenzi wangu, aliye malimbuko ya Asia kwa Kristo.*
>
> *Waroma 16:3-5*

> *Na kwa Afia, ndugu yetu, na kwa Arkipo askari mwenzetu, na kwa kanisa lililo katika nyumba yako.*
>
> *Filemoni 1:2*

Ni sawa kabisa kukutana kwa mashirika na vikundi vidogo kama Kikundi cha Uzima katika kijiji chenu. Ni haki yaki Bibilia kutekeleza.

**Hadithi: Mifano ya Vijiko Virefu**

Kikundi cha wanakijiji waliondoka kwenda kuanzisha jumuia mpya msituni. Kila mmoja alifurahishwa kwa matarajio waliokuwa nayo kwa mwanzo mpya na nafasi ya uzima mapya. Walipata mahali pa kukaa penye maji safi toka mtoni, miti ikikua yenye matunda matamu ya kila aina na ardhi yenye rutuba ya kuotesha mboga za kila aina. Walitengeneza karamu tamu na walifurahia kula chakula. Hata hivyo walikuwa na shida: walihitaji vijiko vya kulia chakula, lakini vijiko tu walivyokuwa navyo vilikuwa ni virefu sana, kupita hata mikono yao!

Kila wakati wa kula kikundi kiliudhika na kuwa na njaa kwa sababu kila wakati wa kula hawakuweza kula kitu chochote kwa sababu hawakuweza kupeleka vjiko kwenye midomo yao. Wakaanza kuwa dhaifu na wagonjwa na wakaanza kuchanganyikiwa wao kwa wao. Kijiji kipya haikuwa sehemu nzuri tena ya kuishi hata kidogo.

Mama mmoja akasema lazima kuwa kuna njia bora ya kula chakula walichokiandaa. Kila mtu alijaribu kula kwa namna yake mwenyewe, lakini kwa hakika kwa pamoja wangetatua tatizo. Muda mwingine wa chakula ulipofika, yule mama akachukua kijiko chake kirefu na kuingiza kwenye dishi la chakula, badala ya kujaribu kujilisha alikinyoosha kupitiliza kumlisha mtu aliyekuwa upande wa pili. Huyu mtu alishtuka lakini alikula chakula toka kwenye kijiko na kuonekana kufurahi! Kila mtu aliona kilichotokea na wakataka kula kama mtu yule, lakini wapoendelea kumwangalia akirudia kumlisha yule mtu mwingine wakatambua kuwa ili kulishwa ni muhimu kutanguliza mahitaji wa wengine kwanza na wote wakaanza kufanya kazi kwa pamoja. Watu wengine wachache wakaanza kuwalisha wenzao na wale waliolishwa nao wakawalisha wale waliowalisha.

Wanakijiji wakakubaliana kulishana kila wakati wa chakula na kila mmoja akashiba na kuwa na afya! Kijiji pakawa ni mahali pa ajabu kuishi wakanza kuhudumiana kwa upendo kila mmoja akimjali mwenzake.

Hadithi hii inatufundisha kuwa tunayo nafasi ya kutumia kile tulichonacho kuwasaidia watu wengine, lakini shida inakuwa mara nyingi tunafikiri zaidi juu ya mahitaji yetu. Kijiji hicho hicho kinaweza kuwa na mali zinazo fanana na hata kuwahudumia watu vizuri ili kila mtu ajisikie

kujaliwa AU wanaweza kuwa wabinafsi na itakuwa ni sehemu ya kutisha na mahali pagumu pa kuishi kwa kila mtu.

Unaweza kuwa sehemu ya kanisa ambayo tayari inavyo vikundi vidogo vinavyokutana tayari. Je ninyi mnapenda tu kukutana wenyewe ama Mungu anakuelekeza kukutana kwa namna nyingine kwa huduma ya kanisa pana na jumuia?

Unaweza kuanzisha Kikundi cha Uzima ndani ya kijiji chako kinacho wakaribisha watu wote, haijalishi ni kanisa gani ama unatokea wapi kwa ajili ya kujifunza habari za Yesu, kukua na kuwapenda wengine. Kwa pamoja mnaweza kupeleleza kile ambacho mnaweza kufanya kwa kanisa kwa mapana na jumuia pia. Kama hadithi ya kijiko kirefu mnaweza kukuunganika na watu wenye historia za nyuma kujifunza habari za Yesu. Je mnaweza kufanya kazi pamoja kwa faida ya jumia yako?

**Maswali: Mifano ya Vijiko Virefu**

- Umeona mfano gani kwa watu wanaofanya kazi kwa pamoja kutatua tatizo kwa kila mtu?
- Unafikiri ni jambo gani linalo wakwamisha watu kufanya kazi kwa pamoja kila mara?
- Ni nini kinachoweza kuwatia watu moyo kufanya kazi kwa pamoja zaidi?

**Vifungu vya Biblia**

Waraka wa Yakobo imejaa ushauri wa matendo na hekima. Jambo kubwa alilojihusisha nalo ni kwamba mara nyingi hawaweki imani yao kwenye matendo, wanaizungumzia tu! Vikundi vya Uzima inaweza kuwa sehemu ya kuwasaidia watu kufikiri juu yake na kuingiza imani kwenye matendo, wanaweza kufanya jambo hili kwa pamoja na wengine.

> [22]*Lakini iweni watendaji wa neno, wala si wasikiaji tu, hali mkijidanganya nafsi zenu.* [23]*Kwa sababu mtu akiwa ni msikiaji wa neno tu, wala si mtendaji, mtu huyo ni kama mtu anayejiangalia uso wake katika kioo.* [24]*Maana hujiangalia, kisha huenda zake, mara akasahau jinsi alivyo.* [25]*Lakini aliyeitazama sheria kamilifu iliyo ya uhuru, na kukaa humo, asiwe msikiaji msahaulifu, bali mtendaji wa kazi, huyo atakuwa heri katika kutenda kwake.*
>
> *Yakobo 1:22-25*

**Maswali: Zaidi ya kusikiliza**

- Wewe unafikiri kifungu cha Biblia kina maana gani na Yakobo anatutia moyo kufanya nini?
- Kitatokea nini tukifanya hivyo?
- Utaiwekaje imani yako kwenye matendo?
- Kikundi cha Uzima itawasaidiaje wengine kuingiza imani yao kwenye matendo?

*"Katika kifungu hiki, Yakobo anatutia moyo kukumbuka maneno tuliyosoma ndandi ya Biblia na kuyaingiza kwenye matendo. Tukiyafanya haya basi tutabarikiwa kwa kila tunalolifanya. Naweza kuyafanya haya nikisoma Biblia na kufikiri yale ambayo Mungu ananiagiza kufanya na niyafanye! Tunaweza kuyafanya haya kwenye Vikundi vyetu vya Uzima pia. Kuwasaidia wengine kuweka imani yao kwenye matendo ningependa kuanza kwa kuwauliza kama wamefanya yale waliyosema watafanya na kuwasaidia kufanya."* ***– Asisi***

**Mafundisho: Tumejifunza nini mpaka hapa**
Mpaka hapa tumejifunza:

- Kukutana pamoja kwenye vikundi vidogo, kama Vikundi vya Uzima, katika fani ya Biblia
- Vikundi vya Uzima ni njia ya kumfanya kila mtu kuwa sehemu ya kanisa
- Vikundi vya Uzima ni sehemu ya kujifunza Biblia, kushuhudiana kuhusu uzima, kumkumbuka Yesu na kushiriki meza ya Bwana pamoja, kuomba pamoja, kuwa wakarimu, kutoa pesa na muda, kuabudu pamojan na kushuhudia pamoja
- Vikundi vya Uzima ni njia ya kusaidia kanisa kwa mapana na jumuia pia
- Vikundi vya Uzima inawakaribisha na kuwaunganisha watu toka tabia tofauti tofauti
- Vikundi vya Uzima inawasaidia watu kuweka imani yao kwenye matendo pamoja na wengine

**Kwa kuweka muktasari: Vikundi vya Uzima maana yake kila mtu ni sehemu ya kanisa, kukutana pamoja, kujifunza, kukaribishana, kuwasaidia wengine na kuingiza imani yao kwenye matendo!**

**Mafundisho: Namna ya Kuongoza Kikundi cha Uzima**
Kwenye sehemu hii tunaenda kujifunza namna ya kuunda na kuongoza Kikundi cha Uzima.

<u>Ni Wapi na Lini Tutakapokutana</u>
Kikundi cha Uzima kinaweza kukutana kokote katika kijiji. Wanawezakutana chini ya mti, shuleni, kwenye vibanda na hata mashambani. Jambo la muhimu la kutazama ni kwamba iwe mahali ambapo kila mtu atakuwa sawa kukutana na ifanyike wakati kila mmoja anaweza kukutana. Unaweza kutaka kuepuka jingo la kanisa ikiwa hiyo itawazuia watu kuhudhuria.

<u>Kuendesha mikutano ya Kikundi cha Uzima</u>
Wahubiri kanisani hunena SANA na watu husikia. Nyakati zingine watu hawaelewi, wamechoka au hata wameacha kusikia. Hakuna nafasi ya kuuliza maswali. Watu hujifunza kutoka kwa kiongozi.

Katika Kikundi cha Uzima kiongozi hunena KIASI na kueleza zaidi. Kuna nafasi ya kuuliza maswali na kujadiliana kupata maana, ujuzi, maarifa na maelezo zaidi. Watu wataomba pamoja na kuombea mahitaji na mambo yanaywazuia wasimtumikie Kristo vyema zaidi. Pia kuna nafasi ya kujiuliza neno la Mungu linahusiana vipi na uzima yao.[6]

<u>Kuwa rafiki: Ni muhimu kukutana na watu kenye mikutano ya Kikundi cha Uzima</u>
Ni muhimu sana kufahamu kuwa kutiana moyo siyo kwenye mikutano ya Kikundi cha Uzima tulivyo navyo. Inaweza kutokea mtu kuwa na shida au anahitaji kutiwa moyo kutumia kipawa alichopewa na Mungu. Kama mwandaaji wa kikundi au mwanachama aliyeaminiwa na kikundi, unapaswa kuwatembelea wanakikundi kila wiki. Hii pia inawahusu watu wanaohudhuria kikundi nab ado siyo Wakristo. Watembelee, uwe na muda nao ukiwatia moyo. Hii itawatia moyo.

<u>Kikundi kinapaswa kuendeshwa kwa wakati uliowekwa</u>
Vipindi vya Kikundi cha Uzima isizidi masaa 2. Kwa njia hii watu watahudhuria kwa urahisi. Wote wawepo kwa muda mliokubaliana na kila wiki. Tusipokutana kila wiki watu watavunjika moyo. Isipoendeshwa kila wakati watu watakata tama. Hata kwa maeneo ya Africa vijijini ambayo muda unaweza kurahisishwa tu, mambo haya ni ya muhimu.

[6] Mfano wa 'Kuzungumza Maneno Machache ama Mengi' imechukuliwa toka kwenye asili ya mafundisho ya Kawaida ya Yesu. Revd. Dr. A. Morgan. Mathetes Inayoaminika. (www.rootedinjesus.net)

**Shughuli: Mchezo wa Mpira**[7]

Nenda chukua mpira, kama unayo moja, au kipande kidogo cha tunda. Tunaenda kuelezea juu ya hali inayoweza kutokea katika Kikundi cha Uzima.

**Ikiwa unajifunza pomoja na kikundi**

Wakati sehemu hii inakuambia uwaze unacheza na mpira na wengine, unaweza kuigiza sehemu hii na wengine, na tumia mpira kuelezea alama. Hii ina maana utakuwa na muda wa kukamata mpira wewe mwenyewe na kumrushia mwingine, wengine wakikurushia kati yako na mtu mwingine na wakati mwingine kuwarushia hao kwenye kikundi chote. Watie watu moyo kurushiana badala ya kila mara kurudisha kwako.

Waza kama uko na Kikundi chako cha Uzima na unaongoza kipindi. Anza kucheza na mpira wako mwenyewe, rusha juu na kudaka, tena na tena.

Ikiwa utaendelea kucheza mpira mwenyewe utakuwa unajifurahisha mwenyewe lakini hakuna mtu yeyote mwingine anayejifunza namna ya kucheza. Baada ya muda mfupi watu watachoka kukuangalia wewe uukicheza mwenyewe. Hii inafanana na kiongozi wa kikundi mwenye kuchukua muda mrefu akizungumza. Baada ya muda watu wataacha kumsikiliza na wakuwa wameelewa kidogo sana.

Sasa jifanye kuwa mnarushiana mpira na mtu mwingine – unaweza hata ukarusha kwenye ukuta ili irudi kwako.

Kama utacheza mpira na mtu mwingine, wataanza kuelewa maana ya mchezo wa mpira unafananaje. Pengine wakauliza maswali ama wanaweza kueleza maana ya kifungu cha Biblia ina maana gani kwa uzima yao. Wanahusika kwenye mchezo. Hata hivyo, ni juu yako na huyo mtu mwingine. Kila mtu mwingine hahusiki na utakuwa ni wewe ndiye mwenye kufundisha mafundisho yote na kuzungumza.

Unaweza sasa kujifanya unarusha mpira mbele na nyuma kwa kila mtu – unaweza ukaurusha tena kwenye kuta 2 au 3 tofauti.

Kwenye Kikundi cha Uzima ni bora kama kila mtu atahusika. Sasa kila mwanachama wa kikundi atakuwa na nafasi ya kuuliza maswali na kusema kifungu cha Biblia kina maana gani ndani ya uzima yao. Kila mtu anajifunza. Kila mtu anahusika. Hii ni bora.

Na njia nyingine bora zaidi ni kwamba siyo kiongozi kujibu maswali yote. Ni bora zaidi wakati mwingine watu kujibiana maswali wao kwa wao na kueleza jinsi walivyoyatatua matatizo kwenye uzima yao wenyewe. Unaweza kudhani ni kukundi cha watu wakirushiana mpira, mtu mwingine kwa mwingine na kuendelea. Huu ni mchezo bora wa mpira.

**Maswali: Mchezo wa Mpira**

- Ni njia ipi ya kucheza mpira au kuendesha kikundi inayomsaidia kila mmoja kushiriki na kujifunza zaidi?
- Je unaweza kufikiri muda ambao ulijifunza jambo fulani kwenye kikundi iliyoandaliwa namna hii? Kama ni hivyo, ulijifunza nini na ulijisikiaje kujifunza kwa njia hii?

[7] Shughuli hii ilichukuliwa kutoka kipindi cha Mafundisho ya Kozi ya Alpha: Namna ya kuongoza Kipindi Kidogo. Alpha Kimataifa.

*“Hakika nilikuwa mahiri kuongoza Kikundi cha Uzima. Tayari nilishaongoza vitu kanisani kwetu. Lakini nilipoanza kuongoza Kikundi cha Uzima nilitambua kuwa hii ni tofauti kwa sababu Mungu alitaka kila mtu aongee, siyo mimi tu! Nilihitajika kujifunza kuwasaidia wengine kujibu maswali na kumruhusu kila mtu kuzungumza. Sasa watu wanaweza kuja kwangu na wazo la kuabudu au kuwapa maskini fedha.” - **Agnes***

**Mafundisho: Matatizo Yaliyopo kwa Wote na Namna ya Kutatua**
Matatizo yanaweza kuwepo ndani ya baadhi ya vikundi ambayo ni lazima kiongozi ashughulike nayo kufanya kikundi kuwa na nguvu. Kama kikundi kikianza kuendeshwa vibaya watu hawatavutiwa kujiunga.

Hapa kuna baadhi ya mifano:

<u>Mtu asizungumze sana</u>
Kumbuka jinsi ulivyotumia mpira kufafanua majadiliano kwenye kikundi? Waza kama kulikuwepo na mtu mmoja aliyeng’ang’ania mpira asitake kurusha mbele wala nyuma kwa wengine. Mara nyingi kwenye kikundi kunakuwepogo mtu anayependa kujibu kila swali na kutoa mchango kwa kila kitu. Wanaongea sana kiasi cha kwamba wengine hawapasti nafasi ya kuchangia lolote.

Kama kiongozi, utafanya nini juu ya jambo hili? Utasema nini waweze kunyamaza?

Kama utasema, “Joni umezungumza sana acha kuongea sasa,” Joni atajisikiaje? Atakwazika na anaweza asirudi kwenye kikundi.

Badala yake ungeweza kusema kitu kama hiki, “Hilo ni jibu zuri Joni lakini watu wengine wangependa kusema nini?” Joni hatakwazika lakini atatambua kwamba sasa anatakiwa kunyamaza kuruhusu wengine kuongea.

<u>Mtu mwenye aibu asiyejibu maswali au kuongea</u>
Waza kama unarusha mpira kuzunguka kikundi na mtu mmoja kila wakati mpira unamkosa au hataki kudaka mpira. Huyu mtu hataki kuongea, pengine anaona aibu ama anakuwa na uoga kukosea.

Utafanya nini kumsaidia huyu mtu kuongea?

Kama ukisema, “Mbona huongei, wewe ni mjinga?” Ana atajiona mjinga na pengine asirudi tena. Badala yake sema kitu kama hiki, “Ana unaonekana kuwa na mawazo mazuri. Umepata jambo lolote unaloweza kusema juu ya jambo hili?” Atajisikia huru kuweza kuongea.

Wakati mwingine watu watasema, “Hapana, sina jambo la kusema.” Kama hilo ndilo jibu basi waache waendelee kusikiliza. Mara nyingi wakati kiundi kimeendelea kwa muda watu hawa watakuwa na ujasiri zaidi na wanaweza kujiunga na majadiliano kwa wiki zinazofuata.

<u>Mtu anayesema jibu hilo ni kosa</u>
Kama mtu akisema kitu kama hiki, “Siamini kuwa Yesu ni mwana wa Mungu.”

Unaweza kujibu ukisema kitu kama hiki, “Hata mimi niliamini hivyo mpaka nilipokutana naye na akabadilisha uzima yangu” au “Wengine wetu hapa tunaamini tofauti, tuendelee kujifunza na kuona yale ambayo Biblia inataka kusema.”

Kama mtu akisema kitu ambacho ni kibaya sana unaweza kusema kitu kama hiki, “Hiyo inapendeza sijawahi kumsikia mtu akisema hivyo kule nyuma.”

Unafikiri watajisikiaje ukisema, “Umekosea, unaaminije hilo!” Itawafanya kujisikia vibaya sana. Inawezekana kamwe hawatarudi tena kwenye kikundi na utakuwa umepoteza nafasi ya kushuhudia kweli ya Yesu kwao. Usijali kwa wiki ya kwanza watu wanapojionyesha kuelewa kila kitu. Wachache wetu ghafla tulifikia kumjua Yesu. Wengi wetu hujifunza kidogo kidogo.

<u>Watu hupinga Kikundi vytu cha Uzima</u>
Wakati mwingine watu hupinga Kikundi vyetu cha Uzima kwenye kijiji. Watu wanakuwa na mashaka haraka. Njia bora ya kushinda jambo hilo ni kuwasiliana vizuri na watu na kuombea jambo lenyewe. Kuwa wazi kwa yale unayoyafanya na namna unavyofanya. Chukua muda kuwaeleza watu. Ukisikia jambo lolote ambalo siyo sawa hakikisha unaenda kulielezea vizuri kwa huyo mtu aliyemsikia akiongea. Tumeona hali hizi zikikabiliwa mara nyingi.

Kumbuka hadithi ya Precious na Phiri tulipoanza somo? Kama wanakijiji wangewasikiliza kijiji kingeunganika, au hata Precious na Phiri wangepata nafasi kanisani na kamwe wasingekuwa wakicheza na moto wakati watu wote walikuwa kanisani!

*“Nilikuwa na wasiwasi juu ya kuongoza Kikundi cha Uzima lakini Mungu akanipa ujasiri wa kufanya, na sasa napenda! Hazina inayotolewa na Dignity ni rahisi na zinasaidia. Nimelelewa inkiwa jasiri na nimeanza kuwafundisha wengine kuongoza vipindi ili waweze kuanzisha Vikundi vyao vya Uzima.”* - ***Mutambo***

**Kikundi cha Uzima Hadithi**
Mabo* alikuwa kiongozi wa Kikundi cha Uzima na alitaka kuwaeleza hadithi ya Noa kwenye kikundi chake kwa wiki moja. Alitaka kuifanya kuwa na sifa kubwa, ishirikishwe na ichangamshe ili waweze kuikumbuka hadithi na kuiingiza kwenye matendo. Aliamua kuiigiza, ataenda kujifanya kuwa kama Noa na kuzungumza na Mungu kwa simu.

Kwa hiyo kwenye mkutano wa Kikundi cha Uzima alisimama mbele ya kila mtu akajifanya anaongea na Mungu kwenye simu. Aliieleza hadithi kwa mtazamo wa Noa akifanyia kazi yale ambaye Mungu anamwambia kufanya. Sauti yake ilikuwa kubwa na tena ikawa kimya, alitembea akizunguka na akakimbia akizunguka. Kila mtu alisikiliza kwa makini, walidhani ilikuwa ni ya kuchekesha lakini pia ilifanya hadithi kuwa hai. Walifahamu jinsi Noa alivyokuwa jasiri kwa kutekeleza yale aliyoagizwa na Mungu.

Kiongozi mwingine alikuwepo pia hapo akimwangalia Mabo akiigiza hadithi. Aliipenda sana akaamua kuitumia kufundisha Kikundi chake cha Uzima hadithi zingine!

**Jina limebadilishwa kutunza siri za ndani*

**Omba**

Andika chini kwenye kitabu chako cha kumbukumbu mambo yote yanayo kusisimua juu ya kuanzisha Kikundi cha Uzima na juu ya wasiwasi uliyonayo juu ya kuanzisha Kikundi cha Uzima. Mwambie Mungu juu ya kusisimuka na wasiwasi wako na mwombe hekima na uongozi. Mwombe akufunulie watu wa kuwakaribisha kwenye kikundi.

**Kufanya Wiki Hii**

Ni wakati wa kuanzisha Kikundi cha Uzima! Unahitaji kupanga muda, siku na mahali pa kukutana. Rudia kufikiri uamuzi uliyofanya juu ya mahali na lini kukutana kwa njia ambayo itakuwa rahisi kwa wale watu uliopanga kuwafikia.

Waambie wale ambao wamekuwa wakikusaidia kupanga juu ya kikundi chako kwenda na kushuhudia kila kitu juu ya Kikundi cha Uzima kwa wale watu ndani ya jumuia ambao tayari wamekaribishwa. Pengine unaweza kuwakaribisha wale uliyo na uhusiano nao kwenye jumuia yenu na wale wanaokataliwa na jumuia kwa sababu fulani. Hii ndiyo nafasi ya kuwakaribisha kwenye familia ya Mungu.

Itakuwa ni vizuri kualika watu kama 20 kwenye kikundi chako kipya. Waambie jinsi itakavyokuwa na nini kitatokea mtakapokutana.

Unaweza kutumia ***Misingi***, chombo iliyoandikwa na Dignity kuongoza kila kipindi kwenye Kikundi cha Uzima, inayoitwa. Umesoma kidogo juu yake kwenye makala iyopita ya Chombo cha Kazi, ***Kuwaandaa Watu wa Mungu***. Kama huna nakala ya ***Misingi***, unaweza kuongea na mtu wako wa mawasiliano au mtu wa Dignity anayejitolea au unaweza kuwasiliana nasi kwa hello@dignityonline.org.uk au kwa WhatsApp no +44 7340 573 937.

Tazama kwenye kitabu chako cha kazi angalia kazi ambazo utazimaliza wiki hii toka kwenye somo hili.

**Andika Chini**

- Mmekutana wiki hii kama Kikundi cha Uzima? Nini kilichoendelea vizuri?
- Ni nini cha tofauti utafanya wiki ijayo?
- Kwa kujiandaa kuanzisha Kikundi chako cha Uzima, mmejadili kila mtu ana kipawa gani. Umetumiaje wiki hii?

**Wiki hii, panga kuzungumza na mtu wako wa mawasiliano**

- Waambie unafikiri nani Mungu anakuambia umfikie ndani ya jumuia yako.
- Jadili jinsi unavyojisikia juu ya kuanzisha Kikundi cha Uzima
- Andaa swali lolote ulilonalo juu yao juu ya Dignity au kuanzisha Kikundi cha Uzima.

**Shughuli za Ziada**

Hii itakusaidia kufikiri yale uliyoyajifunza, ingiza kwenye matendo na upanue uelewa wako. Huhitajiki kufanya kazi zote za ziada lakini tunakutia moyo kufanya moja ama mbili kwa kila somo. Unaweza ukachagua moja ambayo utaona itakusaidia au unayoipenda zaidi!

**Uchaguzi 1:** Waulize marafiki 3 au 4 kucheza mchezo wa mpira na wewe. Mwende kwenye mandhari tofauti na kucheza mchezo kwa njia tofauti, ukiwaeleza marafiki zako kila moja ina maana gani.

**Uchaguzi 2:** Soma hali tofauti hapo chini ambazo zinaweza kutokea kwenye Kikundi cha Uzima, linganisha na yale uliyojifunza na fikiri jinsi utakavyoweza kukabiliana na hali.

1. Hivi karibuni mikutano imekuwa ikiendelea kwa masaa 2 na watu wakaacha kuhudhuria na kukata tamaa. Umetambua kuwa hii ni kwa sababu wanakikundi wawili kila mara huongea sana na kubadilisha lengo la majadiliano. Utatatuaje jambo hili mbele ya hao watu hao wawili?
2. Mmoja wa kikundi hicho mara zote hujibu maswali kwanza, wanakuwa na shauku lakini unataka kuwaruhusu wengine kujibu maswali pia. Utafanya nini?
3. Mmoja wa wana kikundi amekuwa akihudhuria kwenye Kikundi cha Uzima kwa wiki 5 sasa, na bado ni mkimya sana na hata hachangii majadiliano. Utamtiaje moyo naye achangie?
4. Mmoja wa wana kikundi anasema kwenye mkutano kuwa yeye hamwamini Yesu. Utajibuje?
5. Mmoja wa wana kikundi anakuambia kwamba wanakabiliana na matatizo ya familia. Utawasaidiaje?



# CHOMBO CHA KAZI: Kuwa Mchungaji

T Hapo mwanzo kulikuwepo na mchungaji moja mzee aliyeongoza kanisa dogo kijijini. Mchungaji huyu aliongoza kanisa hilo kwa miaka mingi kwa uaminifu. Mapema alianza kuwaza kustaafu na alikuwa amemwandaa kijana wake kuchua nafasi yake atakapostaafu.

Miezi michache ikapita kabla kijana wake hajafika kutoka mjini. Huyu mtu alikuwa tofauti sana kwa kila njia na baba yake. Aliwasisimua wanakijiji alipogeuza kichwa chake ndani ya gari lake na suti. Kwa siri walitumaini kuwa huyu mchungaji mpya atatumia pesa nyingi, kuwasaidia na kulifanya kanisa lifanane na yale waliyoyaona mjini.

Ibada ya kijana ya kwanza ilikuwa ni maarufu kwa kusanyiko lake jipya. Aliwaeleza mipango aliyonayo kwa kanisa lake. Alitaka kujenga jengo jipya kubwa katikati ya kijiji. Alikuwa na marafiki matajiri nchi za nje ambao wangewasaidia kuwa vyombo na mali. Kila mtu alifikiri mtu huyu wazi ni 'mtu wa Mungu'.

Mwaka ulipoendelea kanisa lilikuwa tofauti kabisa. Mchungaji mpya alipata matakwa yake ya kanisa jipya na akajisikia kuwa kanisa lake limestawi. Kila Jumapili, watu walikusanyika kwenye huduma yake na kwa shauku aliongoza akiwa mbele. Kwan je, kila kitu kilionekana kinaenda vizuri bado kiundani kuna kitu kimejificha ambayo ilkuwa ni tatizo.

Mchungaji kijana alikua akipenda madaraka aliyokuwa nayo na hakumwamini mtu yeyote kufanya chochote kwenye kusanyiko lake. Viongozi wa kanisa na wazee wa kanisa walikuwa marafiki wa karibu lakini hawakumwamini mtu yeyote ndani ya kanisa. Kila kitu kanisani ilifanyika kwa namna yake na mtu yeyote aliyejaribu kupendekeza jambo lolote au kusaidia aliwekwa kando na kupuuzwa. Matokeo yake, hakuna hata mmoja kwenye kusanyiko aliyemjua Yesu kwa undani.

Kijana mchungaji alipenda kusikilizwa. Kwa nyakati akawa mtu mwenye kiburi na kwa muda watu wakamtazama kwa juu, naye akawa anawatazama kwa chini. Pia alikuwa mnafiki. Katika mahubiri yake atawaambia watu wasipoteze uzima yao kwenye kunywa na kucheza miziki lakini yeye kwa siri aliendа kwenye mabaa na majumba ya starehe kule mjini usiku.

Baadaye, huyu mchungaji kijana alipewa kazi kwenye kanisa kubwa mjini. Tamaa yake ikagundulika! Siku hiyo hiyo, alipakia mabegi yake na kuondoka bila kusema neno. Hakufikiri kuwa kusanyiko lake lililokuwepo lilikuwa na umuhimu wa kutosha kuendelea kulihudumia na wanakijiji hawakuwahi kumwona tena na waliumizwa na kupotea kwake. Kukosekana kwa familia ya kweli na mafundisho ndani ya kanisa ilimaanisha kuwa wanakijiji hawakuwa wanaandaliwa kuwa kanisa wao wenyewe. Kunisa linateseka hadi leo.

Hadithi hii ni marundiko ya mifano ambayo viongozi hawapaswi kufanya. Mchungaji kijana alijivuna, mwenye kiburi na mwenye mamlaka yaliyozidi. Alitaka kila mtu amfuate na utawala wake, kila kitu kingine haikuwa na

umuhimu kwake. Aliyafuata mambo mabaya bila kujali watu wake hivyo hakuweza kuwasaidia kukua katika wajibu na imani.

1 Petro 5:2-4 ameweka kielelezo namna kiongozi wa kweli anavyopaswa kuwa.

> *[2]Lichungeni kundi la Mungu lililo kwenu, na kulisimamia, si kwa kulazimishwa, bali kwa hiari kama Mungu atakavyo; si kwa kutaka fedha ya aibu, bali kwa moyo. [3]Wala si kama wajifanyao mabwana juu ya mitaa yao, bali kwa kujifanya vielelezo kwa lile kundi. [4]Na Mchungaji mkuu atakapodhihirishwa, mtaipokea taji ya utukufu, ile isiyokauka.*

Viongozi wanaelezewa kuwa wachungaji wanaolitazama kundi la kondoo. Kila siku, wanapaswa kuwaongoza kondoo kwenye malisho mazuri. Wanawaongoza kondoo kwenye malisho mahali pa kulishwa, penye maji waweze kunywa na kuwalinda kondoo wasishambuliwe na wanyama wakali. Wachungaji wanawakuza kondoo zao na kuwasaidia kukua.

Kifungu kinaonyesha kuwa kazi ya kiongozi ni sawa na ile ya mchungaji. Mungu amewaweka watu ndani ya uzima yetu, tunapaswa kuwasaidia kuwaongoza watu hawa, kusadia kuwalinda na kuwasaidia kukua katika imani. Kama una moyo wa kusaidia watu kwenye kijiji chako, hapa ndipo inapoanzia.

Katika kitabu cha Yohana 10:14, Yesu anasema mimi ndimi mchungaji mwema, *"Nawajua kondoo zangu nao wanijua mimi."* Tunapoongoza Vikundi vya Uzima kwenye vijiji vyetu tunapaswa kujua na kufahamu watu ambao ni sehemu yao, kuwaonyesha kuwajali hasa katika uzima yao na kutoa muda kwa ajili yao.

Mwonekano wetu ni wa muhimu sana. Tunaelekezwa kutotafuta faida kwenye uongozi wetu bali tutamani kutumika. Kama viongozi tunatakiwa kujiuliza kwa nini tunataka kuongoza. Ni kwa sababu tunajisikia kupata faida kwenye nafasi zetu kwa namna fulani? Je tunawaongoza kwa sababu tunawajali watu tunaowatumikia na tunataka kuwasaidia kukua, hata kwa gharama zetu?

Kama viongozi hatutakiwi kuwa mabwana kwa watu kwenye vikundi. Mara nyingi watu wanawaona viongozi kama 'watu wa Mungu', watu wa muhimu, lakini Biblia haisemi hivyo. Katika waraka wake kwa Wakorintho, Mtume Paulo alitumia neno la Kigiriki "huperetes" kueleza tabia za viongozi. Hii moja kwa moja inafafanua maana yake ni 'kuwa chini ya makasia' –hawa walikuwa watumwa waliowekwa kwenye kiwango cha chini kabisa cha ngalawa. Hii ilikuwa ni nafasi ya chini kabisa, sehemu ya chini muhimu, nasi kama viongozi tumeitwa 'kuwa chini ya makasia' wa Yesu.

Hii ina maana kuwa wajibu wetu wa kwanza ni kuwahudumia watu ambao Mungu amewaweka katika uzima yetu. Siyo tu kwa yale ambayo Mungu anayafanya kupitia uzima yetu, ni muhimu ivuke zaidi ya uzima yetu kuyafikia uzima ya wengine. Tunapaswa kuwasaidia watu hawa kukua kwenye mahusiano, kuwatia nguvu na kuwawezesha kuwa watu wa Mungu kwa namna anavyotaka wawe.

Hitimisho kama wachungaji tunao mfano halisi wa kufuataa ndani ya Yesu. Yeye ni Mchungaji Mwema aliyeyatoa uzima yake kwa ajili ya kondoo. Tunapozungumzia juu ya kifo chake, Yesu wazi alisema Mwana wa Adam hakuja kutumikiwa bali kutumika (Mathayo 20:28). Tunapaswa kuwa na akili hiyo ya Yesu ndani ya Vikundi vyetu vya Uzima tunazoziongoza; kupenda, kutumikia na kuwapa wengine nguvu kutumika.



**Fikiri juu yake**
Kumbuka kuandika majibu yako kwenye kitabu chako cha kumbukumbu.

- Sababu zako ni zipi kutaka kuanzisha na kuongoza Kikundi cha Uzima? Sababu hizi zinaongozwa na Mungu ama ni za binafsi?
- Je wewe ni mtumishi wa kupenda ndani ya Kikundi cha Uzima? Unaongoza kutumika au kutumikiwa?
- Je Mungu anawaita watu kufanya nini kwenye Kikundi cha Uzima? Utawasaidiaje watu hawa kukubali kutumikia wengine pia?

# 7



# Shuhudia Upendo na Ujumbe wa Yesu

**Basi, nendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi**

Mathayo 28:19

**Lengo**
Injili ni habari za ajabu na Mungu ametuita kushuhudia habari hizi kwa wengine waweze kupata uzima mapya! Somo hili litakusaidia kushuhudia upendo na ujumbe wa Yesu kwa wengine.

**Mwisho wa somo hili utakuwa na:**

- Umefahamu kwa nini Wakristo wanashuhudia injili kwa wengine
- Jifunze namna ya kushuhudia hadithi yako mwenyewe
- Umefahamu ni muhimu namna gani kuwa rafiki na watu, kuwapenda na kuwakaribisha kwenye jumuia ili waweze kupata uzima wao wenyewe

**Tazama Nyuma**
Kila mwanzo wa kila somo tunataka kukutia moyo utazame nyuma kwenye somo lililopita na ufikiri yale uliyoyafanya na yale ambayo Mungu amekufundisha.

- Umejifunza nini toka somo lililopita juu ya kuongoza Kikundi cha Uzima kwa matendo?
- Umekutana na Kikundi cha Uzima wiki iliyopita? Nini kiliendelea vizuri? Utafanya nini cha tofauti wiki ijayo?
- Umemshuhudia mtu yeyote yale uliyoyajifunza wiki hii?

**Shughuli: Kwa nini Umshuhudie mtu Injili?**
Tazama nyuma kwenye Somo 3: Injili ni nini? Andika kwenye kitabu chako cha kumbukumbu sababu zote unazo fikiri kuwa lazima kushuhudia injili kwa wengine.

**Ikiwa unajifunza pomoja na kikundi**
Waambie watu waandike chini majibu ya maswali kwenye shughuli, halafu kila mmoja amshirikishe mwenzake majibu ili watu wote waweze kusikia jibu la kila mmoja.

Watu wangine wanaweza kushindana kujibu maswali haya na kuhitaji muda zaidi au msaada.

**Vifungu vya Biblia**
Amri ya mwisho aliyosema Yesu kbla ya kurudi kwa Baba yake ni hii:

> 18*Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na*
> *duniani.* 19*Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina*
> *la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu;* 20*na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru*
> *ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.*
>
> *Mathayo 28:18-20*

**Mafundisho: Kwa nini Tunashuhudia Injili?**
Tunayo kazi kubwa ya muhimu ya kufanya, kazi iliyo kubwa duniani! Kuwafanya wanafunzi wa Yesu, kuwabatiza na kuwasaidia kumtii yeye. Inawezekana siyo kazi rahisi kufanya, lakini ni nyepesi na Yesu aliahidi kuwa pamoja na sisi katika kila hatua. Sisi ni mabalozi wa Mungu hapa duniani, tunamwakilisha mahali popote tunapokuwepo.

Waza kama kila Mkristo atamua kushuhudia injili na kuwafanya wanafunzi wa Yesu. Hiyo ingefanya tofauti gani! Hebu waza kama kwenye kijiji chako wamejaa watu wanaomjua Mungu, wanaomfuata, wanaowapenda wengine, wakitumia karama zao kuwasaidia wengine, wenye amani na furaha na kuwatendea wengine mema – kijiji chako kitakuwa ni mahali pa tofauti sana!

Yesu aliyazungumza maneno haya ya Isaya toka kwenye kitabu cha Agano la Kale na akasema amekuja kuyakamilisha:

18 *Roho wa Bwana yu juu yangu,*
*Kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema.*
*Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao,*
*Na vipofu kupata kuona tena,*
*Kuwaacha huru waliosetwa,*
19 *Na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa.*

*Luka 4:18-19*

Ujumbe wa Yesu ni habari njema kwa maskini, inaleta uhuru na uponyaji! Yesu anawaleta maskini pamoja, kusimama pamoja. Tunapomshuhudia Yesu, mambo haya yanawezekana watu wanapokutana na Yesu na uzima yao kubadilishwa. Upendo na ujumbe wa Yesu inabadilisha jumuia zote ikiwa na maana zaidi na watu wengi zaidi watamfahamu Yesu.

Kwenye somo hili tutaenda kuangalia njia kadhaa za kushuhudia yote mawili UPENDO na UJUMBE wa Yesu.

Ni muhimu kushuhudia UJUMBE wa Yesu kwa maneno yetu kwa sababu Biblia inasema ‘imani huja kwa kusikia’ (Warumi 10:17).

Ni muhimu kuwaonyesha wengine UPENDO wa Yesu, kwa sababu Biblia inaagiza hivyo, *‘Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za malaika, kama sina upendo, nimekuwa shaba iliayo na upatu uvumao’ (1 Wakorintho 13:1).*




**Shughuli: Tunamshuhudia nani Injili?**

**Ikiwa unajifunza pomoja na kikundi**
Mwambie kila mtu amalize shughuli hii, halafu mshuhudie mtu aliye karibu nao. Wawili wawili wanaweza kuwaombea watu waliowaandika chini.

Ndani ya kitabu chako cha kumbukumbu anza ukrasa mpya.


Chora mduara katikati na andika jina lako ndani yake.




Yetu alipotuombea, hakutuombea tu sisi bali aliwaombea watu ambao wengeamini baada ya sisi kuwashuhudia.

*Wala si hao tu ninaowaombea; lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao.*
*Yohana 17:20*

Sasa fikiri ni nani unamfahamu ambaye yuko mbali na Mungu. Pengine ni rafiki, au mwana familia au mtu unayefanya naye kazi. Chora miduara kadhaa kuzunguka ile ya kwanza na andika majina majina yao ndani ya miduara hiyo. Kidogo itafanana hivi:





Sasa fikiri juu ya watu ambao umewaandika chini na ni akina nani wamehusiana nao. Wameoa/wameolewa? Wanao watoto? Wanayo familia? Wanao marafiki? Wanafanya kazi na watu wengine?

Chora baadhi ya miduara yaunganishe na kila mtu kwenye mchoro wako na andika majina ya watu wanaoweza kushuhudia upendo na ujumbe wa Yesu nao. Ni lazima ifanane kidogo na ule mchoro kwenye ukrasa unaofuata.

Unapochora ramani yako ya marafiki utaona athari kubwa tutakayokuwa nayo kama tutashuhudia habari za Yesu na wengine na kila mmoja kushuhudia kwa wengine pia. Ni muhimu kwetu kuwaeleza wengine ujumbe wa Yesu, injili lakini ni muhimu pia kuwa tunawafundisha wengine kushuhudia injili pia.

Mchoro huu ni kama jicho la ndege likitazama watu unaowafahamu kwenye kijiji chako. Jitoe kuwaombea watu kila siku. Omba wafunguliwe wasikie injili na Mungu atakupa ujasiri na nafasi ya kushuhudia upendo, msaada wa matendo na ujumbe wa Yesu pamoja nao.




**Shughuli: Hadithi Yako ina Nguvu**
Kushuhudia habari zako namna ulivyompokea Yesu na kuweka imani yako kwake itakuwa na nguvu sana. Wengine watajifananisha na mapito yako kwa kusikia mfano wa uzima halisi aliyoyabadilisha Yesu kwenye uzima yako.

Kuna hadithi ndani ya Biblia watu wakikutana na Yesu, kuweka imani yao kwake halafu kushuhudia waliyoyajifunza kwa wengine. Mwanamke mmoja alikutana na Yesu kisimani, alikwenda kisimani wakati wa jua kali kuwakwepa wanawake wengine waliokuwa wakimhukumu. Yesu alizungumza naye kwa upendo akamweleza mambo yahusuyo uzima yake ambayo hakuna mtu mwingi aliyeyafahamu. Alijitambulisha kwake kuwa ni Mwokozi naye akaamini. Alipendezwa na habari hizi njema kiasi cha kurudi mjini akamweleza kila mtu aliyeweza, nao walikuja kuamini pia! Unaweza kusoma haya kwenye kitabu cha Yohana 4:1-26, 39-42.

*Na katika mji ule Wasamaria wengi walimwamini kwa sababu ya neno la yule mwanamke, aliyeshuhudia kwamba, Aliniambia mambo yote niliyoyatenda.*

*Yohana 4:39*

Hadithi ya kila mmoja ni tofauti – baadhi ya watu wanayo hadithi ya kukutana na Yesu na uzima yao ghafla yakabadilishwa, wengine wameweza kumjua Yesu uzima yao yote.

Inaweza kusaidia kutumia njia hizi nyepesi ya kushuhudia historia yako sehemu tatu. Ama inawezekana ukashuhudia historia yako namna ambayo umekuwa ukimfahamu Yesu athari ambayo hiyo imefanya.

- **Kabla ya Yesu:** Uzima yako yalikuwaje kabla ya kukutana na Yesu? Labda ulikuwa mtu wa wasiwasi, mwenye kumiliki au kufanya kitu ambacho ulifahamu ni makosa. Pengine ulijisikia kuwa ulikuwa unaishi uzima mazuri lakini ukajihisi hujakamilika kiko kitu kimepungua.
- **Kukutana na Yesu:** Ulikutanaje na Yesu? Nini kilitokea? Labda kuna mtu alikushuhudia injili au ulienda kanisani ukapitisha uamuzi wa kumfuata Yesu. Hiyo ilifananje?
- **Baada ya Yesu:** Uzima yako yamefananaje sasa baada ya kukutana na Yesu? Labda sasa unayo furaha na amani, unafahamu kuwa unapendwa na umesamehewa na unalo kusudi ndani ya uzima yako. Nini kimebadilika ndani ya uzima yako kwa sababu ya Yesu?

Ndani ya kitabu chako cha kumbukumbu, andika majibu ya maswali hapo juu, halafu utakuwa na alama za kukumbuka kushuhudia historia yako na wengine.


**Ikiwa unajifunza pomoja na kikundi**
Kwa wawili wawili chukua kikundi kufanya mazoezi wakishuhudia hadithi zao.



*"Siku zote niliogopa kushuhudia historia yangu kwa watu kwa sababu niliona ni ya aibu na sikutaka watu kunicheka. Nilishuhudia kwa muda mfupi na mtu mmoja akajiunga na Kikundi cha Uzima akaamua kuishi kwa ajili ya Yesu! Nilitiwa moyo nikataka kumweleza kila mtu historia yangu, wakati mwingine watu walinicheka lakini kwangu ikawa sawa kwa sababu nafanya kwa ajili ya Yesu. Baadhi ya watu walisikiliza historia yangu na wakataka kumjua Yesu wenyewe, ambayo ni ajabu!"* - ***Asisi***

**Mafundisho: Mweleze mtu Fulani**
Utamshuhudia nani hadithi yako wiki hii?

Unakumbuka kujifunza juu ya ***Alama 4***, njia ya kusaidia kushuhudia injili. Alama ziko hapa – unakumbuka zote zina maana gani?



Kama hutakumbuka zote, chukua sasa muda kuyarejea kwenye ***Somo la 3: Injili ni Nini?***

**Ikiwa unajifunza pomoja na kikundi**
Kwa wawili wawili chukua kikundi kufanya mazoezi kumwambia mtu mwingine juu ya ***Alama 4****.*

Historia yako na ***Alama 4*** vifaa viwili vyenye nguvu vya kutumia unaposhuhudia UJUMBE wa Yesu na watu. Utamshuhudia nani historia yako na ***Alama 4*** wiki hii?

Katika Somo la 3, tulijifunza pia kuwa injili ni zaidi ya kusamehewa tu. Ni kwa ajili ya kila mtu na inaweza kufanya tofauti kubwa ndani ya kijiji chote au jumuia. Pale tunapoamua kupokea upendo wa Mungu na msamaha tunahesabiwa haki sawa na Mungu na tunaweza kwenda na kurekebisha mambo ndani ya kijiji chetu. Tunaweza kushuhudia UPENDO wake.

Injili ni habari njema. Inahusu tumaini, msamaha, upendo na uzima. Kufahamu ujumbe wa injili, makanisa waliweka mikutano kufafanua na kukubali juu ya kweli ya Mungu. Waliandika 'itikadi za imani' ambayo ni kiini ya 'itikadi' tunayoshikilia juu ya Yesu. Kila mstari ni kweli muhimu yenye nguvu ya kutubadilisha na kubadilisha jumuia zetu. Itikadi ya Itikadi ya Mitume ni moja maelezo ya kwanza ya imani. Iliandikwa miaka 150 baada ya mitume wote kufariki. Bado inatusaidia leo kwa sababu inatukumbusha kuwa imani ya Kikristo.

**Itikadi ya Mitume**
*Ninamwamini Mungu, Baba Mkuu,*
*muumba mbingu na nchi.*

Hii inatukumbusha kuwa kuna Mungu mmoja, siyo mamia ya miungu au mababu, na yeye ndiye ameumba kila kitu.

*Namwamini Yesu Kristo, Mwana wake wa*
*pekee, Bwana wetu,aliyepata mimba kwa*
*uwezo wa Roho Mtakatifu,*
*aliyezaliwa na Bikira Mariamu,*

Hii inatukumbusha kuwa Yesu ni Bwana, ni mwana wa Mungu na anazo nguvu za kutusamehe, na alikuja katika mwili, na alipitia kila adha ya uzima ya mwanadamu.

*akateswa na Ponsio Pilato,*
*akateswa, akafa, na akazikwa;*
*akashuka kwa wafu.*
*Siku ya tatu akafufuka;*
*akapaa mbinguni,*
*ameketi mkono wa kuume*
*wa Mungu Baba,*
*na atakuja kuwahukumu walio hai*
*na waliokufa.*

Hii inatukumbusha kuwa Mungu alikuwa na mpango wa kuwaokoa watu wake, Yesu alikufa kulipa gharama ya dhambi zetu na akafufuka na kushinda mauti.

*Ninamwamini Roho Mtakatifu,*

Hii inatukumbusha kuwa Roho Mtakatifu ni 'nafsi ya tatu' katika utatu, iliyotolewa toka na Baba, kwa njia ya 88amoja88 yuko 88amoja nasi.

*Kanisa takatifu la katoliki,*
*umoja wa watakatifu,*
*msamaha wa dhambi,*
*kufufuka kwa mwili,*
*na uzima ya milele.*
*Amina*[8]

Hii inatukumbusha kuwa kwa wale wote wanaomwamini Yesu, kwa wakati wote, gharama ya dhambi imeshalipwa, hivyo Mungu anaweza kuishi ndani yetu na sisi ni watu wake.

**Maswali: Itikadi ya Mitume**

- Andika chini sentensi tatu kutoka kwenye itikadi hii inayoweza kuleta tumaini ndani ya kijiji chako na kwa nini? Kwa mfano, 'akateswa na Ponsio Pilato' inatoa tumaini kwa sababu Yesu anajua jinsi mateso yalivyo na kuna watu wengi wanaoteseka ndani ya kijiji changu ambao nitawashuhu dia habari hizi.
- Fikiri juu ya mtu ambaye bado hajatoa uzima yake kwa Mungu. Ni sentensi ipi itakuwa ni habari njema kwao? Kwa nini itakuwa ni habari njema kwao?
- Fikiri mtu anayeshindana ndani ya imani yake. Ni sentensi ipi itakuwa ni itakuwa ni habari njema kwao? Kwa nini ni habari njema kwao?

**Mafundisho: Kuweni Marafiki**

Kushuhudia upendo na ujumbe wa Yesu ni kujenga urafiki wa upendo na watu! Tunaposhuhudia habari njema kwa wengine hatutaki kumwona mtu huyo kuwa lengo, au mwenye dhambi, bali ni rafiki. Mungu anatutaka sisi kuwa marafiki, siyo maadui. Kwa hiyo tunapaswa kuwa marafiki na watu wengine pia. Urafiki maana yake kushuhudiana juu ya uzima, na kuwa na muda nao, ukiwapenda na kujitoa kwao. Tunapaswa kuwa na muda wa kutosha wa kufahamiana na watu, kuwaelewa na uzima yao, uliza maswali, wapende na wasaidie waijue injili. Pengine umewashuhudia historia yako, na kuwashuhudia injili na bado hawaja amini. Hiyo ni sawa. Tunaamini kuwa Mungu anafanya kazi hata wakati ambao hatuoni. Endelea kumwombea mtu huyo, uwe rafiki wao na uwaonyeshe UPENDO.

Kuna sababu nyingi zinazowazuiya watu kupokea UJUMBE wa Yesu moja kwa moja. Kwa mfano, mtu fulani amekuwa akitusiwa na baba yake na inakuwa kweli hasa shida kumkubali Mungu kuwa Baba yake. Au pengine mtu mwingine hajawahi kupendwa na marafiki au familia yake, hivyo inakuwa vigumu kwake kupokea upendo wa Mungu. Watu kama hawa itawachukua muda kuja kwa Mungu na majeraha yao na kumpa Mungu. Mara wanapofanya hivyo Mungu anawaponya maumivu yao na kuwaonyesha upendo usiokuwa na kipimo.

Katika kitabu cha Wathesalonike, Mtume Paulo anaandika si tu kwamba walishiriki injili, bali waliwapenda watu na kuwashuhudia juu ya uzima yao.

[8] Itikadi ya imani ya Mitume iliundwa kwenye karne za mwanzo wa kanisa. Tumechukua nakala ya maandishi toka kwenye tovuti zifuatazo: The Church of England, *What We Believe*, Njia ya kufikia 6 October 2020. Inapatikana kwa: https://www.churchofengland.org/our-faith/what-we-believe/apostles-creed

*7 Bali tulikuwa wapole katikati yenu, kama vile mlezi awatunzavyo watoto wake mwenyewe.*
*8 Vivyo hivyo nasi tukiwatumaini kwa upendo mwingi, tuliona furaha kuwapa, si Injili ya*
*Mungu tu, bali na roho zetu pia, kwa sababu mmekuwa wapendwa wetu.*

*1 Wathesalonike 2:7-8*

**Maswali: Kuweni Marafiki**

- Marafiki zako ni akina nani sasa?
- Utawahudumiaje kama vile mama anavyowahudumia watoto wake, ukiwashuhudia habari za Yesu na uzima yako kwao kama rafiki yao?

*“Mara zote nilifikiri kuwa injili ni kwa wale watu walioko makanisani tu na sikuwahi kuwashuhudia habari za Yesu kwa watu wasiokwenda kanisani. Baada ya kusoma somo la injili, nikatambua kuwa tunapaswa kuwaeleza wengine habari za Yesu kwa sababu analeta uhuru na uponyaji na kuyabadilisha uzima na vijiji! Niliamua kushuhudia upendo na ujumbe wa Yesu kwa majirani zangu kwa kuwa rafiki yao. Nawakaribisha kwenye chakula, na kuwauliza juu ya uzima yao, kuwaangalia watoto wao na kuwasaidia kulima. Jinsi tulivyozidi kuwa marafiki ndivyo walivyozidi kuniuliza maswali juu ya Yesu na niliweza kuwaambia ‘Alama 4’ na wakatamani kufahamu zaidi!” – **Agnes***

**Mafundisho: Penda**

Sababu kubwa inayotufanya kuwapenda wengine, ni kwa sababu Mungu alitupenda kwanza.

*Sisi twapenda kwa maana yeye alitupenda sisi kwanza.*

*1 Yohana 4:19*

Tunamtazama Mungu kama mfano wa kuwapenda wengine. Mungu alitupenda tukiwa mafisadi, wahanga na wakarimu pia. Anatuita kuwapenda watu wa aina hiyo. Tunapowaonyesha wengine upendo, tunawaonyesha upendo wa Mungu.

**Maswali: Penda**

- Utamwonyesha nani upendo wiki hii?
- Ni nani unaona vigumu kumpenda na ni namna gani utawaonyesha upendo wiki hii?

**Mafundisho: Uwe Jumuia**

Sehemu ya kuwapenda wengine ni kuwakaribisha kwenye jumuia. Hatutakiwi kuwasubiri mpaka wampokee Yesu kabla ya kuwakaribisha kwenye Kikundi cha Uzima. Kwa kawaida jumuia ni njia ya kuwasaidia watu kufikia kumjua Yesu. Kazi yetu ni kuwaelekeza watu kwenye uzima mapya ndani ya Yesu na kuwaonyesha uzima mapya yaliomo ndani ya jumuia.

Mwanzo wa somo hili, tunataka ufikiri kama kila Mkristo ndani ya kijiji chako anashuhudia injili na watu wakawa wanaamua kuishi kwa ajili ya Mungu. Hebu fikiri kama kijiji chako chote kitaishi kwa ajili ya Mungu. Hawa watakua watu wengi sana! Hautakuwa mtu pekee anayeshuhudia injili, lakini kila Mkristo anaweza akashuhudia historia yake, kushuhudia injili, kuwa rafiki na wengine, waonyeshe upendo na uwakaribishe kwenye Kikundi cha Uzima.

**Maswali: Uwe Jumuia**

- Utamkaribisha nani kwenye Kikundi chako cha Uzima wiki hii ambaye bado hajaamini?
- Utawafanyaje wajisikie kukaribishwa na kustareheshwa kama sehemu ya kuwaonyesha uzima yako mapya ndani ya Yesu?
- Utawasaidiaje wengine waweze kushuhudia vyote viwili UJUMBE na UPENDO wa Yesu? Fikiri juu ya vifaa na somo ambalo tayari umekwisha jifunza – je utafundishaje kwa wengine na kuwatia moyo kuwafikia watu wanaowazunguka?

**Kikundi cha Uzima Hadithi**

Comfort* kutoka Petauke alikwenda kwenye kongamano la Biblia na Kikundi chake cha Uzima. Usiku moja kulikuwa na chemsha bongo ya Biblia na Kikundi chake kilifanya vizuri sana na watu wakapendezwa sana na majibu yao. Jinsi walivyojibu maswali, ndivyo walivyozidi kujulikana na watu wakaanza kuuliza siri yao ni nini. Hii iliwapa nafasi ya ajabu ya kumshuhudia Yesu na Kikundi chao cha Uzima. Walijieleza kuwa wao hukutana kila wiki kijijini na kuwakaribisha watu kuhudhuria na kujifunza zaidi neno la Mungu. Watu wachache walipokea wito na kuhudhuria Kikundi cha Uzima kwa wiki nzima. Walitiwa moyo kurudi kwenye vijiji vyao, na kuanzisha vikundi vyao vya Uzima hapo.

Comfort alisema tofauti ambayo Vikundi vya Uzima vilifanya kwenye uzima yao ya binafsi imekuwa kubwa. Watu ambao watakunywa na kuvuta kila mara wataacha baada ya kuhudhuria kikundi. Ni ajabu kuona watu wanaomfuata yesu kwa Pamoja kwenye jumuia yenye upendo, kama Kikundi cha Uzima, inakuwa na watu mmoja moja wakiendelea kujiunga.

**Jina limebadilishwa kutunza siri za ndani*

**Omba**

Wiki hii waombee hao watu wote ndani ya ramani yako ya marafiki, omba kwamba upate nafasi ya kushuhudia, ujumbe, kweli na upendo wa injilina wao na wataamua kuishi kwa ajili ya Mungu na kumshuhudia Yesu kwa watu wanaowafahamu.

**Kufanya Wiki Hii**

Wiki hii shuhudia UJUMBE wa Yesu ukitumia historia yako na ***Alama 4*** kwa rafiki ambaye hujawahi kumshuhudia habari za Yesu. Waambie juu ya Kikundi cha Uzima ulichokianzisha na uwakaribishe kujiunga.

Wiki hii mwonyeshe mtu UPENDO wa Yesu. Fikiri namna utakavyompenda mtu kama yeye – wanahitaji nini? Pengine utawapikia chakula, au kujitolea kuwatengenezea kitu fulani au kuwaazima baiskeli yako au kuwasikiliza kwa muda na kuomba pamoja nao. Wakikuuliza kwa nini unawasaidia waeleze historia yako au injili ukitumia ***Alama 4***.

**Wiki hii endelea kukutana kama Kikundi cha Uzima sehemu pale pale, kwa siku na muda waliokubaliana.**

Tazama kitabu chako cha kazi na kuangalia kazi ya kumaliza wiki hii toka kwenye somo hili.

**Andika Chini**

- Ulimshuhudia nani injili ukitumia Alama 4 na historia yako? Uliona rahisi au ngumu? Walilipokeaje? Je walitaka kukabidhi uzima yao kwa Yesu?
- Ulimpenda nini wiki wiki hii? Uliwapendaje? Uliwashuhudia injili?

**Shughuli za Ziada**

Hii itakusaidia kufikiri yale uliyoyajifunza, ingiza kwenye matendo na upanue uelewa wako. Huhitajiki kufanya kazi zote za ziada lakini tunakutia moyo kufanya moja ama mbili kwa kila somo. Unaweza ukachagua moja ambayo utaona itakusaidia au unayoipenda zaidi!

**Uchaguzi 1:** Omba kila siku kwa wale watu uliowaandika kwenye ramani yako ya mahusiano.

- Omba wafunguliwe kusikiliza injili
- Omba Mungu akupe ujasiri na kukupa nafasi ya kushuhudia upendo, kwa matendo na ujumbe wa Yesu kwao

**Uchaguzi 2:** Fanya mazoezi kumsikiliza mtu wiki hii, labda rafiki au mwana familia. Wasikilize kwa makini wanachokisema, waulize maswali ili uweze kuwaelewa zaidi, usiwaingilie na uwaachie nafasi kubwa ya kuongea.

**Uchaguzi 3:** Kama utapanga kukutana na rafiki zako wiki hii, waulize kama unaweza kuwakaribisha watu wengine muwe na muda nao ili wote muweze kufanyika marafiki pia.

**Uchaguzi 4:** Mweleze mtu fulani hadithi ya Chifu aliyepaswa kuchagua kati ya upendo na haki (tazama Somo la 3: Injili ni Nini?). Fanya mazoezi ukiwaeleza kwa mchezo wa maigizo na kupanua jinsi hali ya Chifu ilivyokuwa na jinsi mama alivyojisikia.

# 8



# Waombee Watu

Hata walipokwisha kumwomba Mungu, mahali pale walipokusanyika pakatikiswa, wote wakajaa Roho Mtakatifu, wakanena neno la Mungu kwa ujasiri.

Matendo 4:31

**Lengo**
Maombi huleta mabadiliko na kuomba na wengine inakuwa na nguvuna kukuza mahusiano yetu na Mungu! Somo hili litakusaidia kufahamu nguvu ya maombi.

**Mwisho wa somo hili utakuwa na:**

- Umefahamu maombi ni nini na namna ya kuomba
- Umefahamu umuhimu wa kuomba kwa pamoja
- Umejifunza namna ya kuomba na wengine

**Tazama Nyuma**
Kila mwanzo wa kila somo tunataka kukutia moyo utazame nyuma kwenye somo lililopita na ufikiri yale uliyoyafanya na yale ambayo Mungu amekufundisha.

- Umejifunza nini toka somo la mwisho juu ya kushuhudia upendo na ujumbe wa Yesu?
- Ulishuhudia ***Alama 4*** na mtu yeyote? Uliona ni rahisi au ngumu? Walijisi kiaje? Walitaka kutoa uzima yao kwa Mungu?
- Umeshuhudia yale uliyoyajifunza na mtu yeyote wiki hii?

**Shughuli: Maombi ni Nini?**
Ndani ya kitabu chako cha kumbukumbu jibu maswali haya:

- Maombi ni Nini? Andika chini maneno yeyote yanayokuja kwenye mawazo yako, msemo wowote na njia tofauti unavyoweza kuomba.
- Unaomba namna gani na namna yako ya kuomba imebadikaje kwa nyakati?
- Umepokea majibu yapi kwa maombi?
- Umeomba na watu wengine? Hiyo inafananaje?

**Ikiwa unajifunza pomoja na kikundi**
Mwambie kila mtu kuandika chini majibu yao kwa maswali kwenye shughuli hii, halafu kila mtu ashirikishe jibu lake na wengine ili kila mtu asikie jibu la mwenzake.

**Mafundisho: Maombi ni Nini?**

> *'Maombi hutubadilisha na inabadilisha dunia inayotuzunguka, kwa sababu inatufanya kufanan na Yesu Kristo zaidi.'*
>
> *Justin Welby, Askofu mkuu wa Canterbury*[9]

Watu wengi huomba, hata kama maombi hayo siyo kitu zaidi ya, 'Msaada!' Maombi ni njia bora ya asili ya kuwasiliana na Mungu. Ni 'uzima yetu' kwa Mungu na njia bora ya kudhihirisha imani. Hakuna njia iliyopangwa ya kuomba. Maombi hayana mfumo, na ni jambo ambalo tunaweza kukua na kubadilika tunapokuwa kwenye imani yetu.

[9]@archbishopofcanterbury, 29 July 2020. Njia ya kufikia 6 October 2020. Inapatikana kwa: https://www.facebook.com/archbishopofcanterbury/posts/prayer-changes-us-and-it-changes-the-world-around-us-because-it-makes-us-more-li/3109601985760593/

Maombi yanaweza kuwa:

- Kumlilia Mungu wakati wa mahitaji.
- Ni sauti ndefu iliyokuzwa ya furaha, ya kutarajia kupokea zawadi.
- Kuomba kwa niaba ya mahitaji ya watu wengine.
- Kumwabudu na kumwomba Mungu.
- Ni muda wa kutulia na kusikiliza kwenye uwepo wa Mungu.
- Kutulia mbele za Mungu kwa kupokea upendo wa Mungu.

Maombi siyo shughuli tunayofanya kwa kupaaza sauti tu na hatupati majibu. Maombi yanabubujika kwa uhusiano wetu na Mungu. Inaweza onekana ni ngumu pale mwanzoni, lakini tunapotambua kuwa Yesu yuko pamoja na sisi na tunaweza kuongea naye moja kwa moja inakuwa rahisi zaidi. Jinsi tunavyofanya mazoezi, maombi yetu yanakua na kubadilika. Tunajifunza namna ya kuwasiliana na Mungu kwa kujisikia kwa ndani, mazingira tunayojikuta ndani yake na dunia inayotuzunguka. Maombi yetu yanabadilika kuwa matendo na inafanya mabadiliko. Maombi ni namna ya kujifunza kusikiliza, kutenda na kutembea ndani ya Roho wa Mungu. Tunapoomba na wengine hivi ndivyo Roho wa Mungu anavyotembea ndani ya jumuia na vijiji vyetu.

**Vifungu vya Biblia**

9 *Basi ninyi salini hivi;*
*Baba yetu uliye mbinguni,*
*Jina lako litukuzwe,*
*Ufalme wako uje,*
10 *Mapenzi yako yatimizwe,*
*hapa duniani kama huko mbinguni.*
11 *Utupe leo riziki yetu.*
12 *Utusamehe deni zetu,*
*kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu.*
13 *Na usitutie majaribuni,*
*lakini utuokoe na yule mwovu.*

*Mathayo 6:9-13*

Yesu alitumia muda mwingi kuomba kwa Baba yake Mungu. Ndani ya kifungu hiki cha Biblia anawafundisha wafuasi wake maombi ambayo leo tanaiita 'Sala ya Bwana'. Zaidi ya kutufundisha namna ya kuomba, inatuelekeza mambo ya kuyaombea.

Tutaenda kuangalia kila kifungu ya Sala ya Bwana kujifunza Mungu ni nani, sisi ni nani, anayoyahitaji kwanza na ni mahitaji ya namna gani tunahitaji kwake. Unaweza kutumia Sala ya Bwana kukuongoza kuomba kwa njia tofauti:

- Unaweza kuomba mwenyewe, kama ukiomba kwa sauti ama kimya kimya, ukitumia lugha inayokupendeza haina shida.
- Unaweza kuandika chini maombi yako yakusaidie kukupa mwelekeo.
- Unaweza kuomba na mtu mwingine, mkijadili kila alama na pengine Mungu atakua anasema nini, mkishirikiana maombi na kuombeana.

**Mafundisho**: **Sala ya Bwana**
Tunaenda kuangalia kila kifungu kwenye Sala ya Bwana kuona inatuambia nini. Unaposoma sehemu hii, andika kila mstari wa maombi kwenye kitabu chako cha kumbukumbu na pumzika kidogo kuomba sawa na maelekezo. Andika kitu unachokiombea. Kwa njia hii utarudi kuona yale ambayo Mungu amejibu kwenye maombi yako.

***'Baba yetu uliye mbinguni'***
Hii inatuelekeza kukumbuka Mungu ni nani, na namna ya kumwendea. Kama Baba yetu wa Mbinguni. Siyo tu Baba yake Yesu, ni Baba yetu pia nah ii ina maana kuwa anatujali: anapenda kusikia toka kwetu.Yeye pia ni Baba wa Mbinguni kwa kila mtu anayempokea na kumkubali.

- Namshukuru Mungu kwa sababu ni Baba yetu na tu sehemu ya familia yake.
- Biblia inasema kila kilicho chema hutoka kwa Baba yetu wa Mbinguni. Mwambie Mungu yale unayomshukuru na maombi yeyote aliyojibu.

***'jina [Mtakatifu] lako litukuzwe'***
*Hii inatueleza kuwa Mungu ni Mtakatifu, ni Baba yetu na pia ni Muumbaji wa dunia yote, na ni mkuu zaidi ya jinsi tunavyofikiria.*

- Mshukuru Mungu kwa uumbaji na kwa kukuumba.
- Mshukuru Mungu kwa kuwaumba wengine na yale unayoyashukuru kwa watu wengine.

***'ufalme wako uje'***
*Hii inatuambia kuwa anao mpango na tunapaswa kuliombea iwe kwenye matendo. Yesu alitufundisha kuwa Ufalme wa Mungu umekaribia: tunauhitaji Ufalme wake, wakati mamlaka yake juu ya vitu vyote duniani imekamilika, kuja mapema.*

- Waombee watu wote, mazingira na maeneo ambayo unataka Mungu ayafikie.

***'mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni'***
Huko Mbinguni mapenzi ya Mungu yametimizwa, hivyo tunaomba hayo yafanyike hapa duniani pia – ili dunia ibadilishwe.

- Mwombe Mungu akusaidie kufuate mpango wake na siyo mpango wako, na akuonyeshe mapenzi yake ni yapi.
- Omba kwamba mapenzi yake yafanyike kwa watu wengine pia.

***'Utupe leo riziki yetu'***
Hii inatuambia kuwa tumwamini Mungu kwa mahitaji yetu ya siku kwa siku. Kwamba tuishi kwa kumtegemea yeye na siyo kujitegemea.

- Mwombe Mungu mahitaji yako. Yaweke wazi na uwe jasiri.
- Mwombe Mungu kwa mahitaji ya wengine.

***'utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu'***
Hii inatuambia kuwa Mungu ametusamehe sisi. Hizi ni habari kubwa ila msamaha huu uwafikie wale waliotujeruhi au wale tunaowadai pia.

- Fikiri siku za nyuma na mwombe Mungu akuonyeshe makosa yako ya nyuma. Omba msamaha kwa mambo hayo. Kama uko na wengine, labda tubu kwa watu wengine uliowakosea na mwombe kwa pamoja.
- Mwombe Mungu akuonyeshe kama kuna mtu wa kumsamehe leo? Mwombe Mungu akusaidie uweze kuwasamehe wengine kabisa na kuwapenda. Na kwa wale uliowakosea pengine unapaswa kuwaomba msamaha.

***'na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu.-'***

Hii inatuelekeza kuomba kwa ajili ya ulinzi kinyume na majaribu na kukombolewa kutoka kwenye nguvu za Shetani. Omba kwamba Mungu akuepushe majaribu na kazi za Shetani.

- Inasema 'tuongoze sisi' na 'tuokoe sisi' hivyo omba ulinzi kwa marafiki zako, familia, Kikundi cha uzima na kijiji pia.

*"Nilipokuwa nakua siku zote niliwaza maombi ni njia ya kumwomba Mungu vitu. Kwa sasa nimefahamu kuwa maombi ni njia ya kuwa na mawasiliano na Mungu na kuyakabidhi uzima yetu kwenye mapenzi yake. Kwa sasa namwomba Mungu afanye kazi yake, siyo kazi ninayotaka yeye afanye. Natamani kuwaeleza wengine watambue haya pia. Wiki hii wanakikundi wa Kikundi chetu cha Uzima watazunguka kijijini kuwaombea wagonjwa, tumemwona Mungu kwenye miujiza ya kushangaza!" –* ***Mutambo***

**Hadithi: Mungu Hujibu Maombi**

*'Uganda kihistoria inafahamika kuwa watu waliofanya agano na miungu ya kikabila kwa kutoa sadaka za watu. Imani hiyo potofu ikafungulia roho ya mauti na uharibifu wan chi hii iliyokuwa imestawi. Uonevu wa uongozi wa Iddi Amin Dada, Milton Obote, na wengine wakiwaacha watu wa kawaida kwenye hofu daima. Mwaka 1984, vifungo, mateso na vifo yalikabidhiwa jeshi kulitesa kanisa: mamilioni walikufa. Zaidi ya hayo, Shirika la Afya Duniani mwaka 1997 walitangaza kuwa theluthi moja ya idadi ya watu watafagiliwa na ukimwi.*

*Mateso haya ndiyo yaliyosababisha maombi na mikutano kwenye mapango kuenea nchi nzima ya Uganda. Makanisa katika nchi yakaanza kuunganika kwa hari, kumwomba Mungu kuonekana na kusimamisha vifo na uharibifu.'*[10]

Hii ni sehemu ya kitabu kilichoandikwa na Daniel Bernard. Kwa matokeo ya maombi haya Bernard alishuhudia kuwa idadi ya makosa Kitaifa yalipungua, na maambukizo ya ukimwi na gonjwa lenyewe la ukimwi ikapungua Uganda. Maombi hufanya mabadiliko, hasa wakati kikundi cha watu wanapokuwa pamoja.

**Mafundisho: Kuomba Pamoja**

Wengi wetu tunaomba wenyewe na tunapenda kufanya hivyo kwa sababu inatusaidia, siyo kosa kuomba kwa ajili ya mahitaji yetu. Bado tukiomba kwa pamoja kunakuwepo na nguvu ya jumuia. Kunakuwepo na nguvu wakati waumini wanapokusanyika pamoja kwa aajili ya kuomba, kama jinsi tulivyosoma habari za Uganda na tofauti iliyofanyika watu walipoomba pamoja. Kikundi cha

---

[10] Daniel Bernard, *Praying up a Storm* (Shippensbury, PA.: Destiny Image Publishers Inc., 2004), p122

Uzima vinatoa nafasi kwa watu kuomba pamoja, kama labda hawajawahi kuomba pamoja au hawajaomba kwa miaka.

Vifungu vya Biblia vifuatavyo inaweka mambo haya wazi. Kifungu hiki kiliandikwa wakati uliokuwa mgumu kwa kanisa. Kanisa lilikuwa likiteswa na mamlaka (inafanana kidogo na kanisa la Uganda mwaka 1984). Petro na Yohana, viongozi wa kanisa wa wakati huo, walikuwa kwenye hatari na walikuwa wameachiliwa tu kuto gerezani. Walikuwa kwenye presha kubwa kuzuiwa kumwakilisha Yesu. Kwenye nyakati hizi za kukatisha tamaa, Petro na Yohana walikuwa na kanisa lililokuwa linawasaidia wao.

**Vifungu vya Biblia**

> *23 Hata walipofunguliwa, wakaenda kwa watu wao, wakawapasha habari ya mambo yote*
> *waliyoambiwa na wakuu wa makuhani na wazee. 24 Nao waliposikia, wakampazia Mungu*
> *sauti zao kwa moyo mmoja, wakisema, Mola, wewe ndiwe Mungu, ndiwe uliyefanya mbingu*
> *na nchi na bahari na vitu vyote vilivyomo; 25 nawe ulinena kwa Roho Mtakatifu kwa kinywa*
> *cha babaetu Daudi, mtumishi wako,*
>
> *Mbona mataifa wamefanya ghasia,*
> *Na makabila wametafakari ubatili?*
> *26 Wafalme wa dunia wamejipanga,*
> *Na wakuu wamefanya shauri pamoja*
> *Juu ya Bwana na juu ya Kristo wake.*
>
> *27 Maana ni kweli, Herode na Pontio Pilato pamoja na Mataifa na watu wa Israeli,*
> *walikusanyika katika mji huu juu ya Mtumishi wako mtakatifu Yesu, uliyemtia mafuta, 28 ili*
> *wafanye yote ambayo mkono wako na mashauri yako yamekusudia tangu zamani yatokee.*
> *29 Basi sasa, Bwana, yaangalie matisho yao; ukawajalie watumwa wako kunena neno lako*
> *kwa ujasiri wote, 30 ukinyosha mkono wako kuponya; ishara na maajabu vifanyike kwa jina la*
> *Mtumishi wako mtakatifu Yesu. 31 Hata walipokwisha kumwomba Mungu, mahali pale*
> *walipokusanyika pakatikiswa, wote wakajaa Roho Mtakatifu, wakanena neno la Mungu kwa*
> *ujasiri.*
>
> *Matendo 4:23-31*

**Mafundisho: Kuomba Pamoja**
Mstari wa 23 inatukumbusha umuhimu wa kuwa na watu wanaotujali sisi, watu hawa wanaunda Mwili (au familia) wa Kristo. Petro na Yohana walikuwa na kikundi cha watu waliokuwa wanawasaidia waliomwamini na kumfuata Yesu. Watu hao walijiunga na kitu tunachokiita maombi ya ushirika. Waliungana kufurahia kuachiliwa kwao lakini pia wakishirikiana mizigo yao. Jambo hili kwa uhakika hawakuwa na kitu kikubwa cha kutarajia zaidi ya kuamini ndugu na dada wakiwasaidia.

Kwenye mstari wa 25 na 26 tuliona kuwa waaminio waliomba Zaburi 2:1-2 pamoja. Katika mstari wa 27-29 walichukua kifungu hicho cha maandiko na kuomba juu yake kwa hali waliokuwa nayo, wakijukumbusha kuwa njama yeyote kinyume na Mungu, au upinzani juu yake ni bure. Ukweli huu ungaliwatia moyo kabla hawajaingia kwenye maombi yao yaliyofuata.

Mstari wa 29 na 30 inaturuhusu kusikia maombi yaliyofuata waliombea nini. Kwenye maombi tunaona mambo 3 wazi yaliyostahili kuombewa:

- **Walimwomba Mungu kuingilia kwa niaba yao.** Walimtambua kuwa ni mwisho wa nguvu zote; MFALME MWENYE ENZI (ana mamlaka ya juu na nguvu nyingi mno). Yuko juu ya vyote, na anaona na kufahamu matisho waliopokea.
- **Waliomba wapewe UJASIRI waweze kulinena neno la Mungu.** Kwa kawaida tungewatarajia kuomba majaribu yaondoke au ulinzi juu ya uzima yao, bado wakaongozwa na Roho Mtakatifu, wakaomba wapewe UJASIRI kuzungumza neno zaidi.
- **Waliomba miujiza kupitia mkono wa Yesu Kristo.** Inaonekana kuwa walipotishwa, kila mara walitenda kwa njia yenye mantiki: hapa wanamwomba Mungu kufanya MIUJIZA zaidi kupitia wao. Hii inaweza kusababisha umoja tu wakati miujiza ya Mungu inapoonekana katikati yetu.

Petro, Yohana na wafuasi wa Yesu wengine waliomba kupewa nafasi zaidi kutangaza na kudhihirisha Ufalme wa Mungu, hata walipokabiliana na upinzani. Walijua kuwa watu wangempokea Yesu kama wangesikia habari zake na kumwona akitenda kazi. Hakuna ambacho kingeweza kusimama mbele yake kama hayo yangetokea. Mstari wa 31 tunaona jibu la haraka kwenye maombi yao kwa sababu tunapoomba, Mungu husikia.

Tuliambiwa kuwa mambo mawili yalitokea:

- **Muujiza**
  Mahali walipokutanika palitetemeshwa: huu ni muujiza. Ni tendo la Mungu duniani.
- **Jibu wazi kwa maombi**
  Waliomba kwa ujasiri na walipokea hilo kupitia kujazwa na nguvu za Roho Mtakatifu.

Kwa ujumla tunaliona kanisa linalo tuonyesha umuhimu na nguvu ya kuomba kwa pamoja. Sasa tunafahamu kuwa tendo la kuomba pamoja inatuleta kwenye uwepo wa Mungu kwa namna ya tofauti, na yenye nguvu zaidi ya kuomba peke yetu.

?

**Maswali: Kuna faida zipi tunapoomba kwenye Kikundi cha Uzima?**

- Ni baadhi zipi zipo ya faida tunapoomba pamoja kwenye kikundi?
- Ulishawahi kuomba na wengine? Umegundua faida zipi?
- Toa mfano wa nyakati ambazo ni wazo zuri kuomba pamoja.

**Ikiwa unajifunza pomoja na kikundi**
Mwambie kila mtu aandike chini anachofikiri kuwa faida ya kuomba pamoja, na kila mmoja amshirikishe mwenzake majibu ili kila mtu aweze kusikia majibu yaw engine.

Watu wengine wanaweza kushindana kujibu maswali haya na watahitaji muda zaidi au msaada.

Hapa kuna faida wakati tunapoomba pamoja. Ziko nyingi zaidi ambazo utakuwa umezifikiri!

- Tunakuza mkusanyiko wa mahusiano na Mungu na kuyajenga mahusiano yetu binafsi pia.
- Tunajenga imani ya kikundi kila mmoja anavyoona wengine walivyojitoa na kusikia yale ambayo Mungu anawafanyia wengine.
- Maombi yetu yanashirikishwa na kuyaombea pamoja na kila ombi inadhaminiwa kama ya kipekee na maalum.
- Sisi wote tunaomba na kuona miujiza kwa pamoja!

- Tunakuza mkusanyiko wa mahusiano na Mungu na kuyajenga mahusiano yetu binafsi pia.
- Tunajenga imani ya kikundi kila mmoja anavyoona wengine walivyojitoa na kusikia yale ambayo Mungu anawafanyia wengine.
- Maombi yetu yanashirikishwa na kuyaombea pamoja na kila ombi inadhaminiwa kama ya kipekee na maalum.
- Sisi wote tunaomba na kuona miujiza kwa pamoja!

**Kikundi cha Uzima Hadithi**

Ken* anaishi na mke wake na watoto ndani ya soko la kijiji cha Chibondo, kama km 90 kaskazini mwa Lusaka, mji mkuu wa Zambia. Ken anafanya kazi kama mkulima na kutumia muda wake mrefu akiwa mbali na nyumbani kwenye maeneo ya kilimo ya Lunsemfwa. Anaotesha mazao na mboga kutunza familia yake. Pia hutafuta muda kwa kazi ya Mungu na anatoa muda wake kuwasaidia watu kuanzisha Vikundi vya Uzima.

Ken amepanga kuendesha tukio la mafundisho ndani ya Kwekwe kuwasaidia watu kujua namna ya kuanzisha Vikundi vya Uzima. Alipofika, Ken na wale waliokuwa wanamsaidia walisikia habari ya mwanamke mgonjwa ndani ya kijiji. Jina lake ni Lucy* na amekuwepo kitandani kwa muda wa mwezi mmoja, hakuweza kusimama, kula wala kuongea. Kwa kufahamu familia yake ilimtaka Ken na wanakikundi wenzao kumwombea, hilo ndilo tumaini la pekee walilokuwa nalo. Baadaye siku hiyo, kwa vile hawezi kutembea, walimbeba kumpeleka mahali ambapo mafundisho yangefanyika.

Ingelikuwa ni rahisi sana kwa Ken na wanakikundi wengine kumwombea Lucy wenyewe. Waliwahi kufanya mambo ya namna hii huko nyuma kwa hiyo hakuna jambo geni kwao. Hata hivyo, wazo likamjia Ken, kwa nini tusiite jumuia yote kumwombea? Waamini wanakuwa na nguvu wanapokuwa pamoja na watu wote wako sawa na wa muhimu mbele za Mungu. Ken akawaambia washiriki wao wenyewe watamwombea Lucy kama sehemu ya mafundisho kwao. Alisisitiza wazo la kusema kila mtu anaweza kutumika na Mungu na maombi yao yalikuwa ya muhimu kama yake.

Baada ya msisitizo wa Ken na wanakikundi wengine, waliohudhuria mafundisho yale wote walikubali kumwombea Lucy kwa pamoja. Watu toka vijiji tofauti, wa rika tofauti na dini tofauti wote walimwabudu Mungu na wakaweka mikono yao juu ya Lucy wakati wanaomba.

Kwa mshangao mkubwa, Lucy alipokea uponyaji na kuponywa siku hiyo hiyo. Alirudi nyumbani! Mapema siku ya pili, mwanamke huyu huyu aliyekuwa hawezi hata kuamka kitandani na hawezi kutembea aliweza kuja na kujieleza na kutoa shukrani zake nyingi kwa wote waliomwombea. Kipekee, alitaka kumshukuru Ken na kikundi chote kwa tofauti waliouleta kwenye jumuia na kwa uzima yake. Kikundi chote kikamrudishia Mungu utukufu. Walizungumza na Lucy kumfahamisha kuwa ni Mungu ndiye aliyemponya na anataka kufanya mambo ya ajabu katika uzima yake.

**Majina yamebadilishwa kutunza siri za ndani.*

**Maswali: Kikundi cha Uzima Hadithi**

- Unafikiri hadithi hii inatufundisha nini?
- Ken alichukua hatua ipi ya matendo?
- Matendo ya Ken yalileta adhari gani kwa Lucy na wale waliomwombea?
- Ingetokea nini kama Ken angeomba mwenyewe?
- Ingetokea nini kama Ken asingefanya jambo lolote?

**Mafundisho: Tunawezaje Kuomba kwa Pamoja?**
Kuna njia tofauti tunazoweza kuomba pamoja; zingine zinaweza kujumlisha:

- Kuimba kwa pamoja
- Kuomba kutumia vifungu vya Biblia (mfano, unaweza kuomba ukitumia Zaburi)
- Kuomba kutumia Sala ya Bwana kwa kushirikiana, na kuomba kwa kutumia alama
- Wakati mwingi mtu mmoja anaomba na wengine wanakubaliana ama wakati mwingine wote wanaweza kumwomba kwa pamoja
- Omba uvuvio toka kwa Roho wa Mungu kuongoza maombi yako, anaweza kuwakumbusha watu juu ya kifungu cha Biblia au kuwapa neno au picha ambayo Mungu anataka kutumia kwenye kikundi

Labda unayo mawazo mengine zaidi unavyoweza kufikiri ambayo unaweza kuandika chini kwenye kitabu chako cha kumbukumbu.

Unapokutana na wengine kuomba, ukijumlisha na Kikundi cha Uzima, inaweza kuchukua muda watu kuzoea kuomba kwa pamoja hivyo usifanye haraka kwa muda ule mlio nao pamoja. Kila mmoja awe na nafasi ya kuomba ikiwa wanataka, watu wengine wanaweza kuona wasiwasi kuomba kwa sauti mwanzoni. Tunapoomba pamoja hakuna sababu ya kuomba kwa muda mrefu na kuchanganua maombi. Maneno fulani au staili haifanyi maombi ya mtu kuwa bora zaidi ya mtu mwingine. Usiogope wala usikae kimya, hii inawapa watu nafasi ya kuomba wanapotaka na inamsaidia kila mmoja kumsikiliza Roho Mtakatifu nay ale ambayo anataka kusema.

**Kiongozi wa Matendo**
Tunapoomba kwa pamoja ni muhimu kutunza vitu vichache kwenye akili ya kila mtu kutazama kwenye kikundi:

- Wakati mwingine mnaweza kuomba kama kikundi pamoja, wakati mwingine mnaweza kuomba mkiwa wawili ama watatu. Kama mnaombeana mambo ambayo ni ya binafsi zaidi, kumbuka wanaume waombe na wanaume na wanawake waombe na wanawake. Kwa njia hii, kila mtu atajisikia huru zaidi kuomba maombi. Wakwepe watu wanaoenda kuomba kwa pamoja kwa kujitenga.
- Kama unamwombea mtu uponyaji unaweza ukataka kumwekea mkono au sehemu iliyogafilika. Hakikisha hii inakubalika na utake idhini yao. Kama wewe ni mwanamume unayemwombea mwanamke unaweza ukamwambia mwanamke aweke mkono juu yake wakati unaomba na hivyo hivyo kwa jinsia tofauti.
- Mtu unayemwombea anaweza kukueleza mambo ya binafsi juu ya uzima yake. Usionekane kushtuka na usiwahukumu. Ni muhimu sana kutunza siri za watu, usiende na kuwaeleza wanakikundi. Kama kile ulichoambiwa kina kuogopesha, muulize mhusika kama unaweza kumshirikisha mtu mwingine ili huyo mtu aweza kusaidiwa na kupata huduma stahiki.

**Maswali: Tunawezaje Kuomba kwa Pamoja?**
- Unajisikiaje unapoomba na watu wengine?
- Utawakaribishaje watu na kuwatia moyo waweze kuomba kwa pamoja?
- Utahakikishaje kila mtu atajisikia salama mnapoomba kwa pamoja?

"Mwanzoni nilikuwa na wasiwasi kuambia kikundi change kuomba kwa sauti kwa pamoja, sikutaka wasijisikie vizuri. Baadhi yao walikuwa na aibu hapo mwanzo lakini kwa sasa kila mtu anapenda maombi ya pamoja, tunajisikia kuwa pamoja kama kikundi na imani yetu imeongezeka kwa sababu tumeona majibu mengi ya maombi. Kikundi kinakutana kwa pamoja kila wiki kuomba kwa pamoja kwa muda wa Kikundi cha Uzima, wanajisikia vema kuomba na maombi yao ni ya ujasiri!" – **Asisi**

**Omba**

Omba ukitumia Sala ya Bwana sasa, uwe na muda na umwombe Roho Mtakatifu aongoze maombi yako.

**Ikiwa unajifunza pomoja na kikundi**

Mnapoomba pamoja, tumieni mawazo ya pamoja mliyonayo.

**Kufanya Wiki Hii**

Endelea kukutana kama Kikundi cha Uzima sehemu ile ile, kwa siku na muda ule ule.

Wiki hii panga kukutana na wanakikundi wachache wa Kikundi cha Uzima kwa wakati mwingine kuomba kwa pamoja.

Anza kumshukuru Mungu kwa yale ambayo tayari ameshayafanya. Mnaweza kuimba wimbo kwa pamoja.

Mwombe kwa sauti kuombea kijiji chako. Waombee watu wote uliowashuhudia upendo na ujumbe wa Yesu, na waombee waweze kufunguka kusikia injili na Mungu atakupa ujasiri na nafasi ya kushuhudia.

Watie kikundi moyo kumwomba Mungu kama kuna kitu chochote au kuna mtu fulani ambaye anataka umwombee, na kama kuna jambo lolote analotaka ulifanye kama kikundi. Kwa mfano, unaweza kujisikia kuwa Mungu anataka umwombee uponyaji mtu fulani lakini hujisikii kuwa na uhakika. Lazima uchukue hatua, mwamini na uombe.

Tazama kitabu chako cha kazi kutafuta shughuli zingine za kukamilisha wiki hii toka kwenye somo hili.

**Andika Chini**

- Mkiomba kwa pamoja na wanachama wa Kikundi cha Uzima wiki hii? Ulifanya nini?
- Umetambua faida yeyote baada ya kuomba kwa pamoja? Je kikundi kinajisikia kuwa karibu na Mungu na kwa wenzao? Kwa namna gani?

**Wiki hii, panga kuzungumza na mtu wako wa mawasiliano**

- Zungumza nao juu ya Kikundi cha Uzima ulichokianzisha, ukiwashuhudia yale yenye kutia moyo na yale unayoyaona kuwa magumu.

- Waambie baadhi ya vitu unavyoviombea juu yako, kwa marafiki zako na kwa jumuia yako.
- Andaa swali lolote kwa ajili yao juu ya Dignity au kuanzisha Kikundi cha Uzima.

**Shughuli za Ziada**
Hii itakusaidia kufikiri yale uliyoyajifunza, ingiza kwenye matendo na upanue uelewa wako. Huhitajiki kufanya kazi zote za ziada lakini tunakutia moyo kufanya moja ama mbili kwa kila somo. Unaweza ukachagua moja ambayo utaona itakusaidia au unayoipenda zaidi!

**Uchaguzi 1:** Panga kukutana na mtu fulani wiki kuongea nao juu ya maombi. Unaweza kusema Sala ya Bwana kwa pamoja na kuombeana.

**Uchaguzi 2:** Andika orodha ya maombi kwa ajili ya kijiji. Tazama nyuma masomo yaliyopita na uweke kumbukumbu ya vitu ambavyo tayari tumekwisha ombea. Andika chini maombi uliyonayo kwa watu fulani kwenye kijiji au hali. Unavyoomba Mungu anaweza kukuongoza kwenda kumtembelea mtu na kumwombea.

**Uchaguzi 3:** Ombea kazi ya Dignity kwa bara la Sub-Sahara Afrika. Omba kwamba Vikundi vya Uzima vinaanzishwa vijijini kwenye nchi tofauti na kuleta mabadiliko ndani ya vijiji kwa kuwasaidia watu kukuza mahusiano yao na Mungu kwa kuomba kwa pamoja.



# CHOMBO CHA KAZI: Kujifunza Kuto Kukubaliana

Kule Kusini-Mangaribi mwa Zambia kuna kijiji cha Matondo. Wengi wa wanakijiji hapa wanalima ili waweze kuishi, walichozalisha mara nyingi hupelekwa miji ya karibu kwa malori na kuuzwa kwa faida. Kwa mwaka mmoja, kijiji kilipigwa na mvua nzito. Mabubujiko ya nguvu ya maji yalishukia mkoa, kingo za mito zikabomoka na daraja pekee kwenye mji likaporomoka.

Hii ilikuwa ni shida kubwa kwa wanakijiji. Ghafla wakajikuta wametengwa na miji mingine kwenye mkoa, wasiweze kununua mahitaji yao au kuuza mazao. Makanisa mawili yaliyokuwepo yakaamua kuchukua hatua, walisema watajenga daraja iliyoporomoka. Hata hivyo, mara tu walipoanza kulikuwa na tatizo. Vikundi hivyo viwili hawakukubaliana na kitu chochote.

Kanisa moja lilitaka kujenga daraja bila zege, na lingine likaona mbao ndiyo wazo bora zaidi. Moja ilitaka kuajiri wajenzi wa daraja, na lingine likaona wakaazi wanaweza kufanya kazi kwa pamoja kwenye mradi. Hakuna kikundi kichotaka kuingiza fedha zake isipokuwa kama ingejengwa jinsi wanavyotaka.

Kutokubaliana hii ikachukua nafasi zaidi ya daraja. Makanisa hayo mawili yalikuwa tofauti, moja ni ya desturi na nyingine ni karasmatik. Kutokubaliana huku juu ya daraja ikaonyesha namna walivyomwona Mungu na wao wenyewe.

Eneo la mradi ikafikia kusimama kwa haraka na hawakufikia mwisho wa majadiliano yote. Bado mvua ilipoendelea, ikawa wazi kuwa suluhisho lilitakiwa. Ili watu waweze kupata mahitaji yao, kuishi kijijini ikaanza kuonekana ni ngumu. Mwana kijiji mmoja alisombwa na maji alipojaribu kuogelea kuvuka mto. Makanisa yote mawili yakaona ni lazima jambo lifanyike juu ya jambo hilo. Kila mmoja kwa kukata tamaa alihitaji daraja lijengwe, kwa hiyo wakakubaliana kukutana tena. Makanisa yakashindwa kukubaliana na kushindana kwa masaa na kila mmoja alihuzunika kabisa. Baada ya masaa kadhaa, mmoja wa wakulima hapo kijijini aliingilia mkutano. Alichoka na kutokukubaliana kwa makanisa hayo mawili. “Tafadhali acheni mashindano!” aliomba. “Kijiji chetu kinahitaji daraja hili, kwa nini sisi wote tusipige kura?”

Hakuna kikundi kilichofurahia, waliogopa kuwa suluhisho lao lisingepigiwa kura. Bado walijua kuwa lazima jambo lifanyike! Kwa hiyo wakapiga kura na wana kijiji wakaamua namna ya kujenga daraja na makanisa yakaa kufanya kazi kwenye mradi.

Mambo hayakuwa rahisi. Vikundi vile viwili bado ilikuwa hawakubaliani lakini wakaamua kuwa kwa sababu ya faida ya kijiji na watu wengine, waweke tofauti zao kando. Wakati kazi ya kujenga ikiendelea, walianza kuona kuwa hawakuwa na tofauti hata hivyo. Baadaye daraja likakamilika na kila mtu kijijini akshikwa na furaha kubwa. Makanisa yakajifunza kitu ambacho ni cha muhimu sana; wangaliweka tofauti zao kando na kufanya kitu kizuri kwa ajili ya wana kijiji.

Kutokukubaliana ni sehemu ya uzima. Hatutarajii kuishi kwenye uzima bila kukutana na kutokukubaliana au hali zilizo ngumu. Siku zote hakuna suluhisho lililo kamili. Tunapaswa kujifunza kuto kukubaliana vizuri.

Katika kitabu cha Waefeso 4:2-6, Mtume Paulo anaeleza namna ya kushughulikia kupingana na kuto kukubaliana.

> *2Kwa unyenyekevu wote na upole, kwa uvumilivu, mkichukuliana katika upendo; 3na kujitahidi kuuhifadhi umoja wa Roho katika kifungo cha amani. 4Mwili mmoja, na Roho mmoja, kama na mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu. 5Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja. 6Mungu mmoja, naye ni Baba wa wote, aliye juu ya yote na katika yote na ndani ya yote.*

Tunapokutana na mashindano ndani ya Vikundi vya Uzima, tunapaswa kuwa wanyenyekevu, waungwana na wavumilivu. Kutokubaliana kwingi hutokea wakati watu wanapoona hali au imani toka mitazamo tofauti. Kwa mambo mengine kama tukielewa malengo na sababu kwa jambo hilo hatutakuwa na sababu yeyote ya kusababisha mashindano. Ni muhimu sana kuyapa nafasi mawazo ya watu wengine na wanavyojisikia. Tumeelekezwa kuchukuliana kwa upendo. Hii ina maana kuwaachia watu kuongea, kuheshimu mawazo yao, kuonyesha kuwajali, hata kama hukubaliani nao kabisa. Katika hali zingine, inawezekana hata kufanya jambo fulani ambayo unaona ni ya kipumbavu au hakina umuhimu lakini ni muhimu kwa mtu mwingine. Kwa kukutana na hali zilizo ngumu kwa njia hii, tunaileta tabia ya Mungu mahali.

Wazo la wote linasema kama hatukubaliani na mtu juu ya jambo fulani basi, hatumpendi mtu huyo. Hii inaweza kuwa siyo mbali na kweli. Tazama uzima ya Yesu. Hakukubaliana na watu wengi kama Mafarisayo, Warumi na Wayahudi ambo hawakuamini. Bado haikujalisha ni kiasi gani hakukubaliana na mtu au hakupenda matendo yao, bado aliwapenda, bado aliwafia nab ado anawapa nafasi ya kupokea msamaha. Wacha uzima haya yawe mfano.

Tunaagizwa kutafuta amani na umoja kama waamini. Yesu kipekee aliomba juu ya jambo hili alipokuwa kwenye Bustani ya Gethemane akisubiri kusulubishwa. Aliomba kuwa 'tuwe na umoja' kama yeye na baba walivyo umoja na kwamba waamini wote 'watafikia umoja kamili' (Yohana 17:22-23). Mungu anatutaka sisi kama Wakristo kuwa mwili mmoja.

Hii haina maana kuwa wote tutafanana, kusema nenosawa au kufikiri kitu sawa. Kwenye Vikundi vya Uzima siku zote kunakuwepo na mahali kwa hao wanaoomba tofauti, kuabudu tofauti na kuamini vitu tofauti. Kilicho cha muhimu tunashirikiana kanuni sawa ya imani na kutoa mahali kwa hao wasioamini. Katika kitabu cha Waefeso, Mtume Paulo anaainisha jinsi tulivyounganishwa: tunao mwili mmoja, Roho moja, tumaini moja, Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja na Mungu mmoja. Hizi ni imani tunazopaswa kushuhudia kama waamini. Mambo mengine yanaweza kuwa ya mila, desturi na mtazamo binafsi. Mara kadhaa kama Wakristo tunashikwa kwenye kioo, na mambo yasiyokuwa na umuhimu wakati tukiwa na Roho wote. Namna hii ya desturi na tabia kati ya Wakristo ni ya makosa kabisa. Ni kinyume na yale ambayo Mungu ametuagiza kufuata. Tunapaswa kuwa watu wa kutafuta amani badala ya mashindano, umoja badala ya mgawanyiko.

Kitabu cha Warumi 15:7 Mtume Paulo ameandika, *"Kwa hiyo mkaribishane ninyi kwa ninyi, kama naye Kristo alivyotukaribisha, ili Mungu atukuzwe."* Tunampa Mungu utukufu kwa kuwakubali na kuwapenda wale ambao hatukubaliani nao.

**Fikiri juu yake**

Kumbuka kuandika majibu yako kwenye kitabu chako cha kumbukumbu.

- Ni watu gani kwenye kijiji chako ambao unashindana kukubaliana nao?
- Ni maeneo gani na mada zipi ambazo hamkubaliani? Jaribu kufikiri juu ya jambo hili kutokana na mtazamo wa watu wengine. Fikiri mawazo na hisia zao zinakotokea.
- Utafanyaje uweze kukubaliana na mtu huyu? Je mambo gani utafanya kuweka hali ikae sawa?

# 9



# Uwe na Imani

**Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana.**
Waebrania 11:1

**Lengo**
Somo hili litatusaidia sisi kufahamu baadhi ya mifano ya watu waliokuwa na imani katika Biblia na hii ina maana gani kwetu ndani ya vijiji vyetu.

**Mwisho wa somo hili utakuwa na:**

- Jifunze imani ni nini
- Jifunze historia ya watu waliokuwa na imani ndani ya Biblia na ni jinsi gani tunavyoweza kuwa na imani kama wao
- Fahamu kuwa hata kiasi kidogo cha imani inaweza kufanya adhari kubwa

**Tazama Nyuma**
Kila mwanzo wa kila somo tunataka kukutia moyo utazame nyuma kwenye somo lililopita na ufikiri yale uliyoyafanya na yale ambayo Mungu amekufundisha.

- Umejifunza nini toka somo lililopita juu ya maombi na kuwaombea wengine?
- Umemwombea mtu yeyote wiki hii? Iliendeleaje? Ulipata hisia gani? Nini kimetokea?
- Mliomba pamoja kama Kikundi cha Uzima wiki hii? Iliendeleaje? Ulipata hisia gani? Nini kimetokea?

**Vifungu vya Biblia**
Soma kifungu hiki wazi kwa sauti mara kadhaa na fikiri kwa uangalifu juu ya maneno.

> [1]*Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana…* [6]*Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao.*
>
> *Waebrania 11:1 na 6*

**Mafundisho: Imani ni Nini?**
Imani ni nini? Dikshenari ya Kiingereza ya Oxford inasema kuwa imani ni "kuwa na hakika kamili au kumwamini mtu au kitu fulani." Imani ni kuwa na uhakika iliyokamilika au kuwa na imani thabiti katika Mungu.

Hapa kuna mifano ya imani:

- Kuna imani iliyokamilika na kuamini kuwa tumeokoka na tutakuwa na Yesu milele. Tunayo imani kuwa tumeokoka.
- Kuna imani iliyokamilika na kuamini kuwa Mungu atatenda kwa upendo kamili kwetu sisi. Hatatuudumia vibaya. Tunayo imani katika upendo na tabia ya Mungu.
- Kuna imani iliyokamilika na kuamini kuwa tunapotoka kuyafanya mapenzi ya Mungu, atafanya yale ambayo hatuwezi kufanya. Tunayo imani juu ya utoaji wake.
- Kuna imani iliyokamilika na kuamini kuwa Roho Mtakatifu yupo pamoja nasi, kutupa uzima na kutusaidia kuayafanya mapenzi ya Mungu. Tunayo imani wa msaada wa Mungu kupitia roho wake.

Imani haiko juu ya uwezo wetu. Siyo kwamba kujaribu kwa nguvu zote kuamini juu ya kitu fulani. Siyo maelezo kipofu kwamba kitu kisichowezekana kitatokea, huo ni ujinga.

Badala yake, imani ni juu ya Mungu na tabia yake. Imani ni kuamini juu ya Mungu anayetupenda, asiyebadilika na mwaminifu. Tunapojitokeza kwa imani kulingana na mapenzi yake, Mungu hatatuacha kama yatima. Atakuwa hapo. Tunachoamini juu ya tabia ya Mungu hugusa imani yetu, kuwa na uhakika na tabia zetu kwake.

Tunaweza kufikiri juu ya imani na uhakika kwa tabia ya mtu fulani kupitia mfano wa matendo. Waza rafiki kuomba kukopa pesa kwako na kuahidi kurudisha. Inaonekana kuwa namna utakavyomjibu itategemea namna unavyomwamini rafiki yako.

- Kama unamwona rafiki yako kuwa ni mtunzaji wa fedha zake na ni mwaminifu, inaonekana utachagua kuwakopesha pesa zako. Itategemea yale unayoyajua juu ya tabia zao itakupa imani kuwa utarudishiwa fedha zako.
- Kama utaona kuwa rafiki yako siyo mzuri hata kutunza fedha zake na kila mara hawatekelezi yale wanayoahidi kufanya, inaonekana hutakubali kukopesha fedha zako. Inategemea yale unayoyafahamu kuhusu tabia zao hukuwa na imani kuwa utarudishiwa fedha zako.

Tunafahamu kuwa Mungu ni mzuri, mwema, mwenye haki na upendo, hivyo tunapaswa kuamini tabia yake na kuweka imani yetu kwake. Tutamtumikia yeye siku zote tukijua ya kuwa ni mzuri, mwema, mwenye haki na upendo. Tunapokuwa na Mungu na namna alivyo, tutamfuata mazingira yakiwa mazuri ama mabaya.

**Maswali: Imani ni Nini?**

- Imani ni nini?
- Je unamwamini Mungu? Kwa nini na kwanini humwamini?
- Toa mfano wa wakati uliodhihirisha imani yako kwa Mungu au kwa mtu kupitia matendo yako na eleza umejifunza nini juu yake.

**Vifungu vya Biblia**

Waebrania 11 inatuambia juu ya baadhi ya watu toka kwenye Biblia wanaodhihirisha imani. Hii itatusaidia kufahamu imani.

*[1]Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo*
*yasiyoonekana. [2]Maana kwa hiyo wazee wetu walishuhudiwa.*

*[3]Kwa imani twafahamu ya kuwa ulimwengu uliumbwa kwa neno la Mungu, hata vitu vinavyoonekana havikufanywa kwa vitu vilivyo dhahiri.*

*[4]Kwa imani Habili alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora kuliko Kaini; kwa hiyo alishuhudiwa kuwa ana haki; Mungu akazishuhudia sadaka zake, na kwa hiyo, ijapokuwa amekufa, angali akinena.*

*[5]Kwa imani Henoko alihamishwa, asije akaona mauti, wala hakuonekana, kwa sababu*
*Mungu alimhamisha; maana kabla ya kuhamishwa alikuwa ameshuhudiwa kwamba*
*amempendeza Mungu. [6]Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu*
*amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale*
*wamtafutao.*

*[7]Kwa imani Noa akiisha kuonywa na Mungu katika habari za mambo yasiyoonekana bado, kwa jinsi alivyomcha Mungu, aliunda safina, apate kuokoa nyumba yake. Na hivyo akauhukumu makosa ulimwengu, akawa mrithi wa haki ipatikanayo kwa imani.*

*[8]Kwa imani Ibrahimu alipoitwa aliitika, atoke aende mahali pale atakapopapata kuwa urithi;*
*akatoka asijue aendako. [9]Kwa imani alikaa ugenini katika ile nchi ya ahadi, kama katika nchi*
*isiyo yake, akikaa katika hema pamoja na Isaka na Yakobo, warithi pamoja naye wa ahadi*
*ile ile. [10]Maana alikuwa akiutazamia mji wenye misingi, ambao mwenye kuubuni na*
*kuujenga ni Mungu. [11]Kwa imani hata Sara mwenyewe alipokea uwezo wa kuwa na mimba;*
*alipokuwa amepita wakati wake; kwa kuwa alimhesabu yeye aliyeahidi kuwa mwaminifu.*
*[12]Na kwa ajili ya hayo wakazaliwa na mtu mmoja, naye alikuwa kama mfu, watu wengi*
*kama nyota za mbinguni wingi wao, na kama mchanga ulio ufuoni, usioweza kuhesabika.*

*Waebrania 11:1-12*

Hawa watu wote katika Biblia kutoka kwa Kitabu cha Waebrania ni wa Agano la Kale. Mwandishi wa hadithi alikuwa anawaandikia Wayahudi ambao wangewatambua hawa watu wote. Kwa kuwa hatukukua tukijua historia za watu hawa, inabidi tujifunze historia hizi na mfano bora wanaotuonyesha.

Imani ni kuamini na kuwa na uhakika wa yale tusiyoyaona. Pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu. Watu ambao ni wana wa Mungu wanatarajiwa kuishi kwa kufuata mfumo wa sheria kuliko wengine. Kwa mfano Mungu akisema atapeana, basi tunapaswa kuamini hilo na kufanya inavyopasa. Mungu akisema atatulinda, tunapaswa kuamini na kufanya inavyotupasa.

Iwapo tutachukua watu wawili kutoka kwa hadithi tutatambua maana ya imani kwa watu wawili kutoka kwa Agano la Kale la Biblia.

**Mafundisho: Hadithi ya Noa** (inapatikana katika Mwanzo sura ya 6-9)

Waebrania 11:7 inazungumza kuhusu imani ya Noa.

Katika Mwanzo 6:22 inasema, “Ndivyo alivyofanya Noa, sawasawa na vyote alivyomwamuru Mungu.” Mungu alikuwa anaenda kutuma mafuriko na bado Mungu alitaka kuwaokoa wale waliomwamini. Alimwagiza Noa kujenga safina mahali pasipokuwa na maji! Watu walimkejeli Noa na wakadhani alikuwa mwendawazimu. Kisha maji yakaja na kila mmoja isipokuwa Noa na familia yake walikufa. Imani ya Noa kwa Mungu illiokoa uzima yake.

Imani inahitaji matendo. Hii ina maana kuwa imetupasa kufanya kile anachotaka Mungu hata kama hatufahamu kabisa sababu zake.

**Maswali: Hadithi ya Noa**
Soma Mwanzo 6-9 na Waebrania 11:7 na jibu maswali haya kwenye kitabu chako cha kumbukumbu.

- Noa alionyeshaje imani yake ndani ya Mungu na tendo gani alifanya kwa sababu ya imani?
- Kilitokea nini kwa sababu ya imani ya Noa?
- Ni nini ambacho kingetokea kama Noa hakuwa na imani?
- Kwa nini unafikiri Noa alikuwa na imani kwa Mungu na tanajifunza nini mfano wake?

*“Noa alikamilisha imani na u hakika kuwa Mungu alikuwa na mpango mkubwa ambao alitekeleza. Naweza kuwa na imani kama ya Noa kuamini kuwa Mungu akiniambia nifanye jambo silifahamu nitaaminijuu ya mpango wake.”* ***– Agnes***

**Mafundisho: Hadithi ya Ibrahimu** (inapatikana katika Mwanzo sura ya 12 na 17)

Waebrania 11:8-12 inazungumza kuhusu imani ya Ibrahimu na mkewe Sarah.

Ibrahimu aliambiwa na Mungu ya kuwa atapata mtoto wa kiume ijapokuwa alikuwa mkongwe na mkewe alikuwa tasa. Mkewe hakuamini kabisa, alicheka na kucheka tena alipoambiwa. Mungu pia alimwambia ya kwamba uzao wake utazidi na kuwa mwingi kama nyota. Ibrahimu aling’ang’ana kuamini. Alijaribu kuyafanikisha kivyake, alipolala na mjakazi wake. Hata hivyo, aliamini mwishowe. Mungu alimpa Ibrahimu na mkewe mtoto na akatimiza ahadi yake kwao.

Alikuwa na imani ijapokuwa alikufa kabla ya kupokea ahadi nzima. Uzao haukuwa umezidi na kuwa wengi kama nyota za angani. Nakati zingine inatubidi tusubiri kwa muda mrefu kabla Mungu ayajibu maombi yetu au atimize ahadi yake. Uzao wa Ibrahimu leo hii ni watu wote walio na imani katika Mungu wa Izraeli. Mungu alitimiza ahadi yake kwa Ibrahimu.

**Maswali: Hadithi ya Ibrahimu**
Soma kitabu cha Mwanzo 12 na 17 na Waebrania 11:8-12 na jibu maswali haya kwenye kitabu chako cha kumbukumbu.

- Ibrahimu alichukua hatua gani aliposhindwa kumwamini Mungu?
- Ibrahimu alichukua hatua gani alipokuwa na imani na Mungu?
- Kilitokea nini kwa sababu ya imani ya Ibrahimu?
- Kwa nini unafikiri Ibrahimu alikuwa na imani kwa Mungu na sisi tunaweza kujifunza nini kutoka kwa mfano wake?

**Mafundisho: Simama Imara Katika Imani**
Hata ingawa watu walimcheka, Noa siku zote alikuwa na imani na kumwamini Mungu. Uzima yake na uzima ya familia yake yaliokolewa. Alimwona Mungu akitimiza ahadi yake.

Sarah alimcheka Ibrahimu na Ibrahimu hakuwa na imani siku zote, alijaribu kujifanyia mambo mwenyewe yatokee. Mwishoni aliamini na akampokea mtoto. Alifaulu kuona ahadi ya Mungu ya kuwapatia mtoto yeye na Sarah ikitimia, lakini hakufanikiwa kuona ahadi yote ya kuwa na wana kama nyota za mbinguni. Hiyo ingechukua muda mrefu zaidi ya uzima ya Ibrahimu.

Wakati mwingine watu watatucheka.
Wakati mwingine tutajiona kama hatuna imani.
Wakati mwingine hatutaona siku zote yale ambayo Mungu aliahidi.

Lakini kama Noa na Ibrahimu, tunaweza kuwa na imani kama wao kwa sababu tunamtumikia Mungu yule!

**Shughuli: Unahitaji Imani kwa Sababu Gani?**
Tunapoanza kuendesha Kikundi cha Uzima ni muhimu kwamba tunaweka imani yetu kwa Mungu.

Wewe unahitaji nini kuamini na kuwa na imani kwa Mungu kwa ajili ya nini? Kumbuka Mungu hufanya mambo yasiyowezekana! Ndani ya kitabu chako cha kumbukumbu, Orodhesha vitu vya kipekee kwenye uzima wako na kijiji chako, kwa mfano kwa mtu kupokea uponyaji, au mahitaji, au wengine kufikia kumjua Yesu. Andika orodha kwa kadri utakavyotaka!

Je kuna hali ya pekee kwenye jumuia yako unayoona kama kikwazo kwa Kikundi cha Uzima kukubaliwa? Je kuna changamoto ambayo jumuia yako inakabiliana nayo inayoleta ugumu kwa watu wengi?

Je kuna baadhi ya watu wanaokabiliana na magumu na kuteseka kwa namna nyingine?

Imani inahitajika kuombea hali na watu, hasa wakati huoni mambo yanavyo weza kubadilika. Kuishi kwa imani ni kuchukua hatua ya matendo kwenye uzima yetu na jumuia kutegemea na imani kujua Mungu alivyo!

**Ikiwa unajifunza pomoja na kikundi**
Fanyeni shughuli hii kwa pamoja kama kikundi, mkishirikisha mazingira na watu unaotaka kuwaombea. Jitoe kusimama kwa imani pamoja na kuomba kila mara kwa mambo mlioorothesha.

*"Sikuamini kuwa kijiji changu kingeweza kubadilika, nilifikiri siku zote kutakuwa na watu wanaoteseka, wagonjwa, wenye kushindana. Sikuwa na imani ya kumwamini Mungu kubadilisha hayo. Mpaka nilipotambua kuwa imani si juu yangu mimi au kijiji, ni juu ya Mungu nay ale ambayo angeweza kufanya! Anapenda kijiji changu na anataka kuwasaidia wana kijiji. Hivyo nilianza kuombea vitu ambavyo nildhani haviwezekani – na Mungu alijibu! Alimponya mwana kijiji na akafanya njia kwa makanisa kufanya kazi kwa pamoja. Mungu husikiliza kila ombi, anaweza kujibu moja kwa moja lakini naamini anafanya kazi wakati wote." –* ***Mutambo***

**Hadithi: Ndugu Andrea**
Mwana wa mhunzi mmoja, Ndugu Andrea hakumaliza masomo ya Shule ya Upili. Lakini Mungu alimtumia Mholanzi, aliyekuwa na mgongo usio sawa, mwenye elimu kidogo, asiye na mfadhili na bila fedha kufanya mambo ambayo watu wengi walisema hayawezekani. Kutoka Yugoslavia hadi Korea Kaskazini, Ndugu Andrea alipenyeza mataifa yaliyopinga Injili kufikisha Biblia na kuwatia moyo walioamini. Mara nyingi, alihatarisha uzima yake kwa kuyaweka katika hali hatari na matatizo kwa sababu ya wengine.

Mfano mmoja wa jinsi Mungu alivyopeana kwa muujiza wakati Andrea alihitaji kulipia viza yake. Andrea alipopokea mgeni siku moja kabla alihitaji kutuma maombi yake ya viza, alikuwa na uhakika kuwa mgeni atakuja kumpa fedha za kulipia viza yake. Lakini mgeni mwenyewe alikuwa Richard, mtu ambaye Andrea alikuwa amekutana naye katika mitaa ya mabanda Glasko. Richard hakuja kutoa, bali kuomba. Andrea alieleza ya kwamba yeye hakuwa na pesa za kumpa Richard, lakini alipoongea Andrea aliona shilingi sakafuni. Shilingi hii ilikuwa kiasi kile Andrea alihitaji

kulipia viza yake na ingemaanisha kuwa angeendelea kukaa katika chuo cha Biblia. Badala ya kujiwekea shilingi hiyo, Andrea alipeana shilingi hiyo kwa Richard. Andrea alifanya kile alichojua kinafaa, lakini je Mungu angemtimizia haja yake vipi? Dakika chache baadaye, Andrea alipokea barua na ndani yake kulikuwa na shilingi 30! Mungu alimtimizia haja yake katika njia yake, mfumo wa kimiujiza wa kutimiziwa.

Katika miaka iliyofuata, Andrea alijitoa uzima yake kwa mahitaji ya kanisa lililopo katika matifa ya Kikomunisti. [Katika nchi za Kikomunisti, Biblia haikuruhusiwa kuuzwa, kuchapwa au kosomwa. Serikali ilipinga Wakristo na Makanisa, ikiwafunga jela wachungaji na kufanya uzima wanawake na wanaume wa kawaida kuwa magumu.]

Mungu alimpa Andrea gari mpya aina ya Vokswageni Beetle na kwa njia hii Ndugu Andrea aliingiza kwa siri Biblia na rasilimali zingine katika mataifa yaliyozihitaji. Huku akifanya kazi peke yake miaka michache ya awali, Andrea alishughulika pasipo kuchoka kutumikia makanisa yaliyokuwa katika mataifa ya Kikomunisti. Andrea alipomaliza ziara alirudi nchini Uholanzi alikosimulia masaibu yake na kisha kuzuru mojawapo ya mataifa. Kila ziara ilijaa hadithi ya jinsi Mungu alivyopeana kimiujiza na kumwongoza Andrea kukutana na waumini wa kiungu.[11]

**Mafundisho: Kuanza Kidogo**

Kipawa ya imani ni kipwa cha kiroho. Yakobo 1:6 inasema tunapoomba, tuamini bila mashaka. Tunaweza kuomba imani zaidi tukijua kuwa Mungu atatupa!

Yesu alisema tunaitaji tu imani kama punje ya haradali kuweza kuhamisha milima. Alisema hivyo kwa sababu mbegu ya haradali ilikuwa ni mbegu ndogo sana kuliko zingine, bado ikikua inakuwa miongoni mwa mti mkubwa sana! Uliwahi kukamata mbegu kwenye mkono wako? Ni kadogo, ndiyo? Kadogo kiasi cha kuona shida kukiona. Bado ukiotesha, na kukuza na kutunza, inakua na kukua na kukua! Mungu anasema ni kama imani yetu. Ikiwa tutakuwa tu na imani kwa vitu vidogo, basi utiwe moyo na unavyoendelea kumwamini Mungu kwa vitu vidogo imani yako itakuwa. Sasa utaweza kuwa na imani kwa vitu vikubwa.

Mtoto mdogo anaweza kukua na kufikia kuwa mtu mzima mwenye nguvu.
Mdudu mdogo anaweza kufanya maangamizi makubwa kwa mazao.
Tofali dogo linaweza kumaliza kujenga jingo kubwa.

Vitu vidogo vinajalisha na vinaweza kufanya tofauti kubwa!

Mara mti wa mbegu ya haradali unapokuwa mkubwa inazalisha mbegu zake yenyewe na kama zitaoteshwa nazo zitakua na kuwa mti mkubwa! Mungu anaenda kukutumia wewe kupanda mbegu ya imani ndani ya watu wengine na kuwasaidia nao kukua pia. Waza kama umefanya hivyo kwa mtu mmoja na imani yake kukua. Waza kama wewe na yeye mkafanya hivyo kwa watu wengine wawili na wanapokua wanaotesha mbegu kwa wengine. Waza kama jambo hilo likaendelea kufanyika. Hiyo italeta tofauti gani? Watu wengi ndani ya kijiji chako watakuwa na imani kwa Yesu na Mungu atatenda mambo ya kustaajabisha!

**Kikundi cha Uzima Hadithi**

[11]Wortes, David N. (10 February 2012), *Brother Andrew Biography*. Njia ya kufikia 28 April 2020. Inapatikana kwa: https://www.inspirationalchristians.org/evangelists/brother-andrew-biography/

Frank na Godfrey* wote wanaishi Kapwila, mahali kama km 20 kaskazini mwa Nakonde, kulia karibu na mpaka wa Tanzania.

Wote wawili Frank na Godfrey ni wakulima kijijini waliosikia habari za Dignity inavyofanya kazi kupitia kwa rafiki wa Nakonde. Rafiki wao aliwaambia kuwa wanaweza kuahidiwa vitu vya aina mbalimbali na hata mishahara, lakini wakaona shaka.

Kikundi kutoka kwenye jumuia wakamwambia Frank na Godfrey kwenda na kutafuta ukweli kwa kukutana na kikundi cha Dignity kilichokuwa kinatembelea Nakonde. Pamoja na mashaka yao, Frank na Godfrey walikuana na kikundi na walishangazwa kusikia ujumbe waliokuwa wakishuhudia. Siyo juu ya yale ambayo Dignity ingewapa wala hawakutoa ahadi ya mishahara – rafiki yao aliwadanganya. Badala yake wakasikia kwamba hawakuhitaji zawadi kwa rafiki wa maana au mfadhili toka nje; walikuwa nayo wao wenyewe, mahusiano yao, mali zao na mikono yao. Lakini la muhimu zaidi: walikuwa na Mungu. Waliposikiliza Frank na Godfrey wakaanza kuelewa kuwa hii inatosha! Waliporudi kijijini, walikuwa na furaha nyingi kushuhudia kuna mtu aliwaamini na Mungu mwenye kutoa uwezo kupata uzima yao wenyewe.

Frank na Godfrey walirudi nyumbani wakashuhudia waliyoyajifunza kwa wale waliowatuma na pia waliweza kuwaeleza watu wengine walichojifunza kwenye jumuia yao. Walishuhudia imani kuwa kwa wale wanaomjua Mungu kwenye jumuia wanaweza kuungana kwenye maeneo ya kijiji, na kuwafundisha watu kuwa na **imani** na kuanza kufanya kazi kwa pamoja kutafuta suluhisho na uzima yenyewe.

Kwenye kijiji chao kwa sasa kuna Vikundi vya Uzima vitatu wanaojifunza habari za Yesu na kufanya kazi kwa pamoja kwenye jumuia. Mungu ameweka uzima na mabadiliko kwenye moyo wa kijiji chenyewe, kupitia watu wanaoishi hapo.

**Majina yamebadilishwa kutunza siri za ndani*



*"Baada ya kwenda kwenye mkutano wa Dignity nilihisi Mungu ananiambia kuanzisha Kikundi cha Uzima, lakini nilifikiri nahitaji fedha, chakula na nyumba kubwa ya kuwakaribisha watu wote. Niliposoma habi za Noa na kwamba alikuwa na imani ya kumwamini Mungu na kufanya kila jambo Mungu alilomwagiza kufanya – Nilihisi kama Mungu anazungumza na mimi! Nilitaka kufanya yale ambayo Mungu ameniagiza kufanya hata ingawa sikuelewa vizuri. Nimetambua nilihitaji imani na kumwamini Mungu kuanzisha Kikundi cha Uzima, sikuhitaji pesa, chakula au nyumba kubwa!"* – ***Agnes***

**Maswali: Kikundi cha Uzima Hadithi**

- Frank na Godfrey walihitaji nini kufanya tofauti ndani ya kijiji chao?
- Je walihitaji vitu vilivyoonekana kuwa vikubwa (kama mshahara) au walikuwa na imani kuwa Mungu atatumia vitu vile vinavyoonekana kuwa vidogo (kama marafiki)?
- Frank na Godfrey walionyeshaje imani yao katika Mungu na walichukua hatua gani kwa sababu ya imani yao?
- Nini kilichotokea kama matokeo ya matendo ya Frank na Godfrey?
- Unadhani matendo yao yangekuwa na adhari gani kwa imani ya watu wengine?

**Mafundisho: Hitimisho**

Kwenye somo hili tulitazama mifano mingi ya watu wenye imani. Noa na Ibrahamu walikuwa na imani. Ndugu Andrea alikuwa na imani. Frank na Godfrey walikuwa na imani.

Kwa kuwa walikuwa na uhusiano na Mungu, walitambua tabia ya Mungu na kuamini kuwa yeye ni mwaminifu. Walisikia sauti yake, walijua hata waangusha, wamemwona Mungu akifanya mambo ya ajabu kabla na walikuwa na imani kuwa atafanya tena. Wote walichukua hatua kwa yale waliyoyaamini kuhusu Mungu.

Imani ni zawadi kutoka kwa Mungu na zawadi hii ya imani inaweza kukua kila wakati. Tunaanza kumwamini Mungu kwa vitu vidogo na tunapomwona akitekeleza inainua imani yetu kuamini kuwa anaweza kufanya mambo makubwa na makubwa na makubwa. Imani yetu hukua tunapochukua hatua na kumwona Mungu kwenye utendaji.

**Maswali: Hitimisho**

- Nini imekutia moyo kuhusu historia ya hao watu tofauti?
- Unayo imani na uhakika kwa Mungu kwa sababu ya tabia yake? Kwa nini na kwa nini huna?
- Ni imani ya namna gani ungependa kuwa nayo na ni hatua gani utachukua kuanza kutumia imani?

**Omba**

Tazama nyuma kwenye orodha ya hali ya vitu maalum ambazo ungependa kumwona Mungu akileta mabadiliko. Omba kwamba Mungu akupe kipawa cha imani ambayo itakusaidia kuanza kumwamini Mungu kwa imani zaidi ya ile uliyokuwa nayo. Ombea hali zilizopo kwenye orodha yako. Mwombe Mungu atende kwenye hali hizo na kupanda mbegu ya imani ndani ya watu wengine ziweze kukua na kukua na kukua!

**Kufanya Wiki Hii: Mkutane Pamoja Kuomba kwa Ajili ya Imani**

Mwendelee kukutana kama Kikundi cha Uzima, mahali pale pale, na siku hiyo hiyo na muda huo mliokubaliana.

Wiki hii panga kukutana na wanachama wachache wa Kikundi cha Uzima kwa wakati mwingine kujadili somo hili la imani. Washirikishe orodha ya maombi ulioandika toka kwenye somo hili na waulize kama wana kitu cha kuongeza kwenye orodha. Labda kuna watu pekee au hali Fulani kwenye kijiji chako ambayo wewe au Kikundi chako cha Uzima wanayo imani kubadilisha.

Mwombe kwa pamoja ili Mungu awaongezee imani, na kwa kila moja ya hali hizo zilizopo. Kwa mfano, inawezekana kuna watu wameadhirika kwa sababu ya ulevi ndani ya kijiji chako – waombee na uombe kwa imani kuona mambo hayo yanabadilika. Pengine kuna watu wanaohitaji kulishwa ndani ya kijiji chako – waombee na pia uwe na imani ya kuchukua hatua ya kuwalisha.

Tazama ndani ya kitabu chako cha kazi kutafuta kazi za kukamilisha wiki hii kutoka kwenye somo hili.

**Andika Chini**

- Umekutana na wanachama wa Kikundi cha Uzima kuomba kwa ajili ya imani? Je kikundi kimeona mazoezi kuwa ya kusaidia? Kwa nini?
- Umeona majibu yeyote kwa maombi haya?
- Umeona nafasi yeyote ya kuwa sehemu ya majibu ya maombi haya?

**Shughuli za Ziada**

Hii itakusaidia kufikiri yale uliyoyajifunza, ingiza kwenye matendo na upanue uelewa wako. Huhitajiki kufanya kazi zote za ziada lakini tunakutia moyo kufanya moja ama mbili kwa kila somo. Unaweza ukachagua moja ambayo utaona itakusaidia au unayoipenda zaidi!

**Uchaguzi 1:** Angalia kwenye orodha ya maombi, chagua mahitaji mawili ama matatu na uombee kipekee. Ziandike kwenye kipande cha karatasi na ficha hiyo karatasi sehemu fulani salama ambayo unaweza kurudi baada ya mwaka na kuipata. Utatiwa moyo kuona yale ambo Mungu amefanya katika mwaka!

**Uchaguzi 2:** Tafuta mbegu, angalia jinsi ilivyo ndogo na ufikiri itakuwa kuwa nini. Panda mbegu hiyo na tunza, iangalie kila mara inavyoendelea kukua. Tunapo panda kitu fulani tunategemea kitu fulani kitatokea na tunakuwa na imani kuwa mmea utakuwa ndani yake. Kila mara unapoangalia mmea huo, inakukumbusha kuwa tunaweza kuwa na imani katika Mungu kama mbegu ndogo lakini Mungu atatusaidia kukua na kukua katika imani.

**Uchaguzi 3:** Wakati Yoshua alipowaongoza Waisraeli kuvuka mto Yordani, kitabu cha Yoshua 3, aliwachukua watu kumi na wawili kuchukua mawe kutoka mtoni na kuyapanga ili kuweka kumbukumbu. Hii ndiyo iliyokuwa njia ya kukumbuka jinsi Mungu alivyowaleta kupitia mto Yordani na itakuwa kumbukumbu kwa vizazi vingine kwa uaminifu wa Mungu. Ni muhimu kukumbuka nyakati Mungu amejibu maombi yetu. Kumbuka wakati mwingine Mungu amejibu maombi yako, kila mara unapokumbuka chukua moja ya nyakati hizi tafuta jiwe ndogo na weka kando ya dirisha lako ikae hapo. Utatengeneza kifurushi kidogo itakayo kukumbusha uaminifu wa Mungu na kujenga imani yako kwa mambo yajayo.

10



# Muktasari – Nimejifunza Nini?

**Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu.**

Wafilipi 1:6

**Lengo**

Sasa umemaliza ***Safari Kijijini***. Tunataka kukupa muda kidogo kufikiri juu ya yale uliyoyjifunza na ni zipi hatua zako zingine.

**Mwisho wa somo hili utakuwa na:**

- Fikiri juu ya yale yaliyokusaidia na yale ambayo hayajakusaidia hapo nyuma
- Kumbuka umejifunza nini toka ***Safari Kijijini*** na ni kipi hasa kimekuwa cha msaada
- Jifunze umuhimu wa kuvumilia bila kukata tama

**Tazama Nyuma**

Kila mwanzo wa kila somo tunataka kukutia moyo utazame nyuma kwenye somo lililopita na ufikiri yale uliyoyafanya na yale ambayo Mungu amekufundisha.

- Ulijifunza nini kuhusu somo lile lililopita juu ya kuwa na imani?
- Ulikutana na wanachama wako wa kwanza wa Kikundi cha Uzima kutengeneza orodha ya vitu unavyohitaji kuwa na imani navyo? Umeona majibu ya maombi yeyote kwa wiki hii?
- Umeshuhudia yale uliyojifunza kwa mtu yeyote wiki hii?

**Hadithi: Safari**

**Ikiwa unajifunza pomoja na kikundi**

Mwalike mtu wa kujitolea acheze nafasi ya Mulubwa. Mpe vitu vingi abebe kwenye safari yake. Mwalike kila mtu ampe chochote cha kubeba kwenye safari yake. Mwambie ajaribu kutembea akizunguka chumba akivibeba vile vitu vyote mlivyompa!

Mulubwa aliandaa safari yake kuelekea kichakani. Alitumia wiki nzima kupanga mizigo yake. Alipakia na kupakia na kupakia tena. Alitaka kuhakikisha anacho kila anachokihitaji kwa ajili ya safari. Aliamua atapakia nyumba yake yote aondoke nayo!

Aliondoka akiwa na gunia mgongoni mwake na ndoo mbili kwenye mikono yake.

Baada ya siku chache, Mulumbwa hakufika mbali hata hivyo! Kila kitu alichopakia ilikuwa nzito kiasi cha kwamba aliweza tu kutembea polepole.

Lakini bado alikuwa anaokota vitu vingine njiani alivyofikiri vingeweza kumsaidia.

Sasa Mulubwa amebeba gunia mgongoni mwake, kikapu kichwani, ndoo tatu mikononi mwake na akimfuata mbuzi nyuma yake.

Bado aliendelea kukusanya zaidi na zaidi, alitaka kujiandaa kwa chochote ambacho kingeweza kutokea pale kichakani!

Mulubwa sasa amebeba gunia mbili mgongoni kwake, kikapu kichwani, ndoo tatu mikononi mwake, makopo matatu ya asali na maji na mbuzi na kuku wakimfuata nyuma.

Mulubwa sasa anatembea pole, pole san asana!

Aligundua kuwa watu wengi wanampita tu. Anawaona watu na mabegi madogo madogo wakitembea haraka haraka tu.

Baada ya safari fupi anakutana na ujuzi toka kwa wasafiri waliokuwepo huko kichakani kwa muda mrefu. Walilala pamoja usiku na mtu huyo akamwuliza Mulubwa kwa nini amebeba vitu vingi namna hiyo. Mulubwa alimwonyesha huyo mtu vitu vyote alivyoanza navyo safari na vitu vyote alivyookota njiani. Vitu vingine vilifaa kutumika na vingekuwa na msaada. Vitu vingine havikuwa na msaada wowote na Mulubwa hakuwa na sababu ya kuwa navyo! Yule mtu akamwambia alihitaji tu kuwa na vitu vichache kwa safari yake, maana uzito wa mzigo ulimfanya kutembea pole pole. Yule mtu akamwonyesha vitu bora vilivyohitajika kwa matumizi.

Siku chache baadaye Mulubwa akasimama mahali pa kupumzika na akaamua kuviondoa vitu ambavyo vilionekana ni uchafu, asingeweza kuendelea na jinsi alivyokuwa! Sasa alikuwa na uamuzi wa kufanya – Angebakiza vitu vipi kwa ajili yake? Angevitupa vifaa vipi? Na ni vitu gani vipya alivihitaji kwa sababu ya safari yake?

**Mafundisho: Safari Yako**
Uko mwanzo wa safari yako ya kumfuata Mungu na kuona kijiji chako kimebadilika!

Kama safari yeyote, tunabeba begi na kulipakia taratibu vile vitu tunavyovihitaji kwa ajili ya safari. Hatupakii vitu ambavyo hatuvihitaji. Wakati mwingine tunapaswa hata kuangalia kwenye mabebi yetu na kutoa vitu tusivyovihitaji.

Tunaweza kuwa na vitu vya kuumiza hata ndani ya mabegi yetu, au kuwa na elimu ama ujuzi Fulani au wazo ambalo mwishoni wake ni kutukatisha tamaa tu. Pengine tumeshindwa kumwelewa Mungu. Kama Mulubwa, labda ulianza vipindi hii ukiwa na mawazo ambayo yasingeweza kukusaidia namna ya kufanya kazi na Mungu na namna ya kufanya mabadiliko ndani ya kijiji chako. Tunatakiwa kuchukua mawazo haya na ujuzi toka kwenye mabegi yetu maana zitatuchelewesha tukiendelea kubeba.

Pia kuna mawazo na fikra ambazo ni za msaada kwetu kubeba safarini. Zinatusaidia kwenda haraka. Tumeandika Safari kukupa WEWE njia rahisi ya kufanya tofauti KUBWA. Hatuhitaji mawazo wala maelezo magumu. Kwa urahisi tu unapaswa kufuata njia ambayo Mungu mwenyewe ameandaa kwa ajili yako. Haya ni mawazo ambayo tunapaswa kutunza.

Kwa sasa unayo baadhi ya maamuzi ya kufanya. Kutoka kwa yale uliyojifunza katika ***Safari Kijijini***, ni mawazo na fikra gani utachukua kwa safari yako? Ni mawazo na fikra gani utenda kuachana nazo?

*"Nilijihisi kuwa kama yule mtu aliyebeba mabegi mazito. Nilikuwa na shughuli nyingi kanisani na kuwa na presha kufanya kitu hiki na kile kuwa Mkristo na kuishi kama Mkristo. Lakini hadithi hii inanisaidia kufahamu kuwa jambo hili ni rahisi. Nataka kumfuata Mungu na kumuuliza anataka nifanye nini, kwa hiyo nilichukua muda kila siku kumwomba anielekeze anayoyataka mimi kufanya. Siku moja ilikuwa ni kumsaidia jirani, siku nyingine ni kumwombea rafiki yangu aliyekuwa mgonjwa, siku nyingine ni kuwashuhudia watu jinsi nilivyokutana na Yesu." -* ***Asisi***

**Shughuli: Unabeba nini?**
Tumia dakika 20 kujibu maswali haya mawili kwenye kitabu chako cha kumbukumbu.

- Ni mawazo na fikra zipi utabeba kwenye safari yako?
- Ni mawazo na fikra gani unaenda kuziacha?

Unapojibu maswali haya, fikiri kwa uangalifu juu ya vitu vifuatavo:

- Mungu anapenda nini?
- Mungu anatendaje kazi kwenye kijiji chako?
- Unawaonaje watu wengine? Je ni wa muhimu au wamo tu njiani?
- Je jinsi unavyoishi inakurudisha nyuma?
- Kwa namna ulivyolielewa kanisa imekusaidia ama imekurudisha nyuma na kijiji chako?
- Je umevunjwa au umetiwa moyo kwa miradi au mawazo uliyojaribu huko nyuma?
- Je umeumizwa na yale ambayo watu walisema juu yako au kumwumiza mtu mwingine kwa yale uliyoyasema?
- Uliwahi kupata ujuzi wa maumivu kwenye uzima yako na bado unahisi maumivu hayo?

**Ikiwa unajifunza pomoja na kikundi**
Kila mtu aandike chini majibu ya maswali kwenye shughuli hii, halafu shuhudia kwenye vikundi vidogo.

**Mafundisho: Tazama Nyuma**
Hii ni hitimisho kwa kitu cha msingi tulichokijifunza kwenye ***Safari Kijijini.***

**Somo la 1: Miti Mikubwa ya Haki na Somo la 2: Safari ya Dignity**
Watu wa Mungu ni kama **Miti Mikubwa ya Haki**, inaleta kivuli na ni mahali pa kukimbilia kwa wengine. Wewe ni mti mkubwa na unayo nafasi ya muhimu ya kutenda kwenye kijiji chako kuwaunganisha watu na kuwafanya wengine kuwa miti mikubwa! **Watu wa kawaida wanaweza kufanya mambo makubwa kwa ajili ya Yesu!** Unaweza kuanzisha kitu kipya kijijini kwako na kuwasaidia wengine kuishi pamoja.

**Somo la 3: Injili ni Nini? Na Somo la 7 Kushuhudia Upendo na Ujumbe wa Yesu**
Injili ni habari njema kwamba Mungu alitupenda upeo kiasi cha kumtuma Mwanaye wa pekee kuchukua adhabu yetu kwa kutompenda Mungu. Tunaweza kuchagua kupokea msamaha huu na kuwa mbali na adhabu, kukabidhi uzima yetu kwa Mungu na kuishi jinsi anavyopenda kuanzia sasa. Tunapopitisha uamuzi tunapewa haki na Mungu na tunaweza kwenda kijijini kwetu na jumuia na dunia na kuyaweka mambo sawa pia! **Tunaweza kushuhudia ujumbe, kweli na upendo**

**wa injili kwa wengine kufuatia maneno yetu na matendo. Hii itawasaidia wengine kupata uzima katika Yesu,** hii itabadilisha jumuia na kuwasaidia wengine zaidi kusikia injili na kukutana na Yesu.

**Somo la 4: Uzima ni Kupitia Familia na Somo la 5: Kila mtu Anayo Sehemu**
Mungu anatualika kwenye familia yake! Familia zinafanya kazi pamoja, wakifanya kazi kwenye migawanyo yao, wakitazama yale yenye kuwaunganisha wao na kuwakaribisha watu kwenye familia. **Kila mtu analo jambo la kufanya kwenye familia**, kila mmoja analo jambo la kufanya la kuwanufaisha wengine na unaweza kuwa ni mtu wa kuwasaidia wengine kutambua hili. **Mungu amemwita kila mtu kuunganika kuwa familia ya Mungu** kufikia na kupenda kijiji chao kwa pamoja.

**Somo la 6: Kuendesha Vikundi Vidogo Vikubwa**
Vikundi vya Uzima ni vya muhimu sana kwa Mungu kufanya kazi kwenye kijiji, inawaleta watu pamoja na kuifanya injili kuwa hai! Mkutano mdogo wa kikundi katika kijiji chako ni kifani ya Biblia: **Kikundi cha Uzima, ambayo mtu yeyote anaweza kuwa ni sehemu yake, kuwa pamoja, kujifunza, kukaribishana, kuwasaidia wengine na kuingiza imani yao kwenye matendo!**

**Somo la 8: Kuwaombea Watu**
Maombi yanabubujika tunapokuwa na uhusiano na Mungu. Maombi ni njia ya kutusaidia kusikiliza, kutenda na kutembea ndani ya Roho wa Mungu. **Tunapoomba pamoja na wengine tunajenga imani ya kila mmoja**, tunamsikiliza Mungu kwa kila mmoja wetu na kwa jumuia, na tunaona jinsi Roho wa Mungu anavyotembea ndani ya kijiji chetu.

**Somo la 9: Kuwa na Imani**
Imani ni kuamini kamili na kuwa na uhakika ndani ya Mungu. Tunaweza kuwa na imani kwa sababu tunayo mahusiano na Mungu, tujua tabia yake na tunafahamu hatatuangusha. **Kikundi cha Uzima huwasaidia watu kuweka imani zao kwenye matendo!**



*"Kitu ambacho kimesimama hasa kwangu kutoka Safari Kijijini ni pale Mungu anaponiambia niwe mti mkubwa na kuwafanya wengine kuwa miti mikubwa! Sikuwahi kufikiri kama ningeweza kuanzisha kitu kipya au kufanya kitu kikubwa, lakini hii imenipa uhakika kufanya! Na kwa sasa nawafundisha wengine kuwa miti mikubwa na kuanza vitu vipya kwenye vijiji vingine ili tuweze kueneza upendo na ujumbe wa Yesu kila mahali!"*
*– **Mutambo***



**Shughuli: Ni mawazo gani toka *Safari Kijijini* utaenda kubeba kwenye safari yako**
Tumia dakika 20 kujibu maswali hapo chini ndani ya kitabu chako cha kumbukumbu. Tazama kila Somo tena ndani ya kitabu hiki kukusaidia kukumbuka.

- Ni somo lipi hasa umelishika? Kwa nini?
- Somo lipi hasa limekustaajabisha? Kwa nini?
- Ni somo lipi ni rahisi kuingiza kwenye matendo ndani ya kijiji chako? Kwa nini?
- Ni somo lipi lililo gumu kuingiza kwenye matendo ndani ya kijiji chako? Kwa nini?
- Ni somo lipi unafikiri linaweza kufanya badiliko kubwa kwenye kijiji? Kwa nini?
- Ni vitu gani vya muhimu umejifunza katika ***Safari Kijijini*** ambayo hungependa kusahau? Kwa nini?

**Ikiwa unajifunza pomoja na kikundi**
Kila mtu aandike chini majibu ya maswali kwenye shughuli hii, halafu shuhudia kwenye vikundi vidogo.

**Mafundisho: Usikubali Kushindwa!**
Katika kuanza safari mpya tunakuwa tumejazwa na msisimko, kutazamia jambo kutokea na imani. Kuna masaa mengi mbele ambayo haitaaminika – kuona mahusiano yakirejeshwa, kuwaona watu wakija kwa Yesu, kuwaona watu wagonjwa wakiponywa, kuwasaidia hao wanaoteseka, kujenga umoja baina ya makanisa, kuona kijiji kuwa ni jumuia yenye upendo. Mungu anaenda kufanya mambo ya ajabu kupiti wewe na Kikundi chako cha Uzima!

Hata hivyo, kwa kila safari yeyote, mara zote siyo rahisi na kunakuwepo na changamoto mbeleni. Nyakati hizo utahitaji uvumilivu kuendelea mbele.

Kwenye kifungu cha Biblia hapo chini Mtume Paulo analiandikia kanisa la Wathesalonike na kuwatia moyo kamwe kutokata tama na kubaki katika imani, upendo na tumaini.

> *Wala hatuachi kuikumbuka kazi yenu ya imani, na taabu yenu ya upendo, na saburi yenu ya tumaini lililo katika Bwana wetu Yesu Kristo, mbele za Mungu Baba yetu.*
>
> *1 Wathesalonike 1:3*

Tunaweza kuvumilia na kuwa na subira kwa sababu tunalo tumaini ndani ya Bwana Yesu Kristo. Siyo kila kitu kinatutegemea sisi. Kuvumilia maana yake kamwe usikate tama na songa mbele bila kujali nini kitatokea.

Kutakuwa na nyakati ngumu kumfuata Mungu na majaribu yatakuwa ya kukatisha tamaa, lakini Mungu anatuagiza kusonga mbele, atatutia nguvu katika imani na tutaona mambo ya ajabu!

Hapa kuna mambo matatu ya kukumbuka kutusaidia kuvumilia:
**1. Mungu atamaliza kazi aliyeianzisha**

> *[3]Namshukuru Mungu wangu kila niwakumbukapo, [4]sikuzote kila niwaombeapo ninyi nyote nikisema sala zangu kwa furaha, [5]kwa sababu ya ushirika wenu katika kuieneza Injili, tangu siku ile ya kwanza hata leo hivi. [6]Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu.*
>
> *Wafilipi 1:3-6*

Mungu ameanzisha kitu Fulani kipya ndani ya uzima yako, ya kuendelea ***Safari Kijijini*** Mungu atakuwa ameongea na wewe juu ya kitu kipya anachotaka wewe ufanye. Aliahidi kukamilisha kazi aliyoianzisha na utakuwa sehemu ya kazi hiyo. Mungu kamwe hakati tama na sisi na kwa watu wake!

**2. Kamwe msikate tama kukutana**

> *[23]Na mlishike sana ungamo la tumaini letu, lisigeuke; maana yeye aliyeahidi ni mwaminifu;*
> *[24]tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri; [25]wala tusiache*
> *kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine; bali tuonyane; na kuzidi kufanya hivyo,*
> *kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia.*
>
> *Waebrania 10:23-25*

Tulivyojifunza kwenye vipindi hii, kukutana pamoja na kuomba pamoja ni muhimu sana na ina nguvu ya kubadilisha jumuia! Shikilia tumaini ulilonalo ndani ya Yesu Kristo, mtiane moyo na kamwe usikate tama kukutana pamoja.
Kuna mithali isemayo: *'Ikiwa unataka kufunga, nenda mwenyewe. Ukitaka kwenda mbali, mwende pamoja.'*[12]

Ili kukabiliana na hali ngumu, tunawahitaji watu watuzunguke kutukumbusha uaminifu wa Mungu na kututia moyo kusonga mbele haijalishi kuna nini.

**3. Usiache kutenda mema**

> *Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna kwa wakati wake, tusipozimia roho.*
>
> *Wagalatia 6:9*

Ni rahisi kukata tamaa tunapofanya mambo mazuri bila kuona matokeo au kufikiri watu hawatudhamini. Lakini Mungu aliahidi kuwa kama hatutakata tamaa tutavuna kwa wakati wake. Unachofanya kwa imani na upendo kwa wengine, usiache kufanya kwa sababu inaleta tofauti hata ikiwa hatuoni! Mungu anaona kile unachokifanya. Kutakuwepo na dhawabu kwa wale wanomtumika Mungu, Siyo dhawabu ya fedha ila ni dhawabu ya Ufalme wa Mungu unaokuja.

Mwisho, ufunguo wa kuvumilia ni kudumu kumtazama Yesu. Yesu alikabiliana na majaribu na mambo magumu na upinzani hata msalabani kwa sababu ya furaha iliyokuwa mbele yake. Tunapaswa kumtazama huyu aliyefanya hayo yote na kushinda ili kwamba katika Yesu tuweze kushinda pia.

Tumaini tulilonalo katika Bwana Yesu Kristo ni kwamba chochote kitakachotokea katika uzima haya, yuko pamoja nasi na tutakuwa pamoja naye kwa ajili ya uzima wa milele.

**Maswali: Usikubali Kushindwa!**

- Nini imekutia moyo wakati wa hali ngumu kabla?
- Ni nani unayemfahamu mtia moyo mzuri? Nini kinawafanya kuwa watia moyo wazuri?
- Ni watu gani waliokuzunguka ambao utawaambia wakutie moyo wakati unapoendelea kuongoza Kikundi cha Uzima? (Hii itakuwa ni watu ambao uko nao kwenye Kikundi cha Uzima)

**Kikundi cha Uzima Hadithi**

Dignity imekuwa ikifanya kazi na vijiji kule Siavonga kuanzia Julai 2012. Vikundi vichache vya Uzima vilianzishwa lakini havijakua wala kuanzisha Vikundi vingine vya Uzima. Kikundi kimebidi kuvumilia kwenye maeneo hayo na kuamini kuwa Mungu atawasaidia. Walipotaka kukata tamaa,

[12] Haijulikani, Haijatolewa tarehe, *PassItOn* Njia ya kufikia 7 October 2020. Inapatikana kwa: https://www.passiton.com/inspirational-quotes/7293-if-you-want-to-go-fast-go-alone-if-you-want

walisonga mbele. Kikundi kikaamua kuwa watawatembelea wanajumuia kila mara na kuwatafuta watu ambao Mungu amewaweka hapo kuongoza Vikundi vya Uzima kuleta mabadiliko kwenye maeneo yao. Miti mikubwa ya Mungu! Kuanzia mwaka 2018 mwezi wa nane kikundi kiliwapata watu ambao walikuwa tayari kujitolea kuanzisha Vikundi vya Uzima. Kuanzia hapo Vikundi vya Uzima vilianzishwa. Mmoja wa kikundi alisema hivi: *"Uvumilivu wetu hapa Siavonga umeshinda upinzani tuliokabiliana nao."*

**Omba**

Omba kwa ajili ya uvumilivu ili usikate tamaa wakati nyakati ni ngumu. Omba kwamba Kikundi chako cha Uzima havitakata tamaa kukutana pamoja na kutenda mema. Mshukuru Mungu kwa mambo ambayo umejifunza kukusaidia kushuhudia upendo na ujumbe wa Yesu kwa wengine.

**Kufanya Wiki Hii**

Mwendelee kukutana kama Kikundi cha Uzima sehemu, siku na muda mliokubaliana.

Wiki hii, kabla au baada ya mkutano wa Kikundi cha Uzima, muwe na muda wakati mwingine mkisherekea pamoja. Mkieleza kuwa mmemaliza *Safari Kijijini*. Hii ni sherehe yenye kustahili! Mmeanza pia kukutana kwa pamoja kama Kikundi cha Uzima. Hii ni sherehe yenye kustahili! Mchukue muda wakati mwingine kukumbuka mambo yale yote Mungu aliowafundisha na maombi aliyoyajibu wakati mnapokutana pamoja.

Tafuta njia ya kumsifu kwa pamoja. Mnaweza kuimba au kuomba, unaweza kushuhudia historia yako na wengine, unaweza kutoa fedha kidogo ama muda kumsaidia mtu mwingine kama njia ya kumrudishia Mungu sifa.

Mwombee kila mtu ambaye yuko kwenye Kikundi chako cha Uzima. Mwombe Mungu awape uzima mapya, wajenge wawe miti mikubwa ambayo itaeneza upendo na ujumbe wa Yesu kwa wengine. Omba kwamba Kikundi cha Uzima watajifunza pamoja, kutiana moyo na kufanya kazi kwa pamoja kuleta tofauti kwenye kijiji chako.

Tazama kitabu chako cha kazi tafuta shughuli zingine za kukamilisha wiki hii kutoka kwenye somo hili.

**Andika Chini**

- Je mmekuwa na muda wa kusherekea na Kikundi chako cha Uzima na kumshukuru Mungu? Mlisherekea namna gani?
- Umejisikiaje kukumbuka yale ambayo Mungu amefanya kwenye vipindi hii?
- Je unafurahia mambo ya baadaye ya Kikundi cha Uzima?

**Wiki hii, panga kuzungumza na mtu wako wa mawasiliano**

- Waambie kuwa umemaliza ***Safari Kijijini*** na masomo yale yaliyokuwa ya muhimu kwako.
- Wajulishe jinsi Kikundi cha Uzima ulichokianzisha kinavyoendelea. Kama unakabiliwa na changamoto yeyote unaweza kumshirikisha mtu wako wa mawasiliano. Wataweza kukutia moyo.
- Andaa swali lolote ulilonalo juu yao kuhusu Dignity au kuanzisha Kikundi cha Uzima.
- Kama unataka kuendelea na Safari hii na kujifunza ***Safari ya Maeneo*** ni muhimu kuzungumza na mtu wako wa mawasiliano juu ya jambo hili. Itakuwa ni vizuri kuwa na

muda kidogo kutazama yote uliyojifunza na ujizoeshe kuongoza Kikundi cha Uzima kabla ya kuanza vipindi nyingine. Hata hivyo, itakuwa ni vizuri kupanga ni lini utaanza ***Safari ya Maeneo***. Hii itakupa mtazamo.

**Shughuli za Ziada**

Hii itakusaidia kufikiri yale uliyoyajifunza, ingiza kwenye matendo na upanue uelewa wako. Huhitajiki kufanya kazi zote za ziada lakini tunakutia moyo kufanya moja ama mbili kwa kila somo. Unaweza ukachagua moja ambayo utaona itakusaidia au unayoipenda zaidi!

**Uchaguzi 1:** Tazama nyuma Somo la 1 na 2 na shughuli ulizofanya ambazo zimesaidia kufikiri hali ilyopo kwa sasa hapo kijijini kwako. Andika chini mabadiliko uliyoyaona hadi sasa.

- Kuna mtu aliyekuwa anateseka amesaidiwa?
- Kuna mtu amefanyika Mkristo?
- Watu toka makanis tofauti wameanza kufanya kazi pamoja?
- Je watu wameanza kusaidiana? Wanafanyaje jambo hili?
- Je watu wameanza kutumia vipawa vyao ndani ya Kikundi cha Uzima na ndani ya kijiji?

Tungependa kusikia hadithi zako na kusherekea pamoja nawe, wacha mtu wako wa mawasiliano kufahamu majibu yako kwa maswali yaliopo hapo juu.

**Uchaguzi 2:** Andika hadithi fupi ya mtu anayekabiliana na change moto na anonekana kukata tamaa. Kwenye hadithi yako, andika jinsi Mungu anavyowatia moyo, pengine kupitia mtu mwingine, na uwasaidie kuvumilia na kusonga mbele.

**Uchaguzi 3:** Mpe mtu mwingine kitabu hiki ambaye unadhani Mungu anamwita kushuhudia upendo na ujumbe wake kwenye jumuia yao. Jitoe kuwa mtu wao wa mawasiliano, rafiki kwenye Safari. Unaweza kuwasaidia waanze safari ya ajabu na Mungu!

**Pongezi!**

Utakuwa sasa umemaliza ***Safari Kijijini***! Tunatumaini utakuwa umevuviwa na kupata changamoto kwa yale uliyojifunza. Tunaomba kuwa Mungu akutumie kuleta mabadiliko ndani ya kijiji chako na kwenye uzima ya wanakijiji.

Unaweza kumkabidhi mtu mwingine wa kijiji kingine kitabu hiki ili nao waweze kuanzisha Kikundi cha Uzima.

Tunza mahusiano na mtu wako wa mawasiliano na wajulishe yale uliyoyafanya mpaka sasa. Kama huna mtu wa mawasiliano unaweza kutuma tovuti kwa **hello@dignityonline.org.uk** au wasiliana kwa WhatsApp no **+447340573937.**

Mpaka sasa ni muhimu kuingiza haya kwenye mazoezi yote uliyojifunza kwenye kitabu hiki na uwe

unakiendesha Kikundi cha Uzima. Kabla ya kuendelea kwenye kitabu kingine, tunataka kukusaidia kwa vitendo kuanzisha kazi ya Mungu badala ya kujifunza tu. Sasa ni wakati wa kuwa na muda kuwafundisha hao walioko kwenye Kikundi chako cha Uzima ili waweze kufanyika miti mikubwa na washuhudie upendo na Ujumbe wa Yesu ndani ya Kijiji!

Kama umefurahia ***Safari Kijijini*** na unataka kuendelea na safari yako, basi unaweza kumuuliza huyo mtu wako wa mawasiliano juu ya vipindi nyingine. ***Safari ya Maeneo*** inakufanya kukua na kupanua kazi ya Kikundi cha Uzima, ukianzisha Vikundi vingine vya Uzima na kusaidia Vikundi vya Uzima hivi kuongezeka.

# Orodha za Picha

| | |
|---|---|
| Jalada la Mbele | Imepigwa picha na Concha Mayo tarehe Unsplash |
| Somo la 1 | Mche wa Ndizi - Imepigwa picha na Jametlene Reskp tarehe Unsplash |
| Somo la 1 | Mti wa Banyani - Imepigwa picha na Brandon Green tarehe Unsplash |
| Somo la 2 | Imepigwa picha na Jtarehe Tyson tarehe Unsplash |
| Chombo Cha Kazi: Tembea na Yesu | Imepigwa picha na Hu Chen tarehe Unsplash |
| Somo la 3 | Imepigwa picha na Loren Joseph tarehe Unsplash |
| Somo la 4 | Imepigwa picha na Roman Nguyen tarehe Unsplash |
| Chombo Cha Kazi: Kuwatayarisha Watu wa Mungu | Imepigwa picha na Ratanjot Singh tarehe Unsplash |
| Somo la 5 | Imepigwa picha na Nick Fewings tarehe Unsplash |
| Somo la 6 | Imepigwa picha na Denys Argyriou tarehe Unsplash |
| Chombo Cha Kazi: Kuwa Mchungaji | Imepigwa picha na Nick Fewings tarehe Unsplash |
| Somo la 7 | Imepigwa picha na Trevor Cole tarehe Unsplash |
| Somo la 8 | Imepigwa picha na Trevor Cole tarehe Unsplash |
| Chombo Cha Kazi: Kujifunza Kuto Kukubaliana | Imepigwa picha na Sheir Hooley tarehe Unsplash |
| Somo la 9 | Imepigwa picha na Zoltan Tasi tarehe Unsplash |
| Somo la 10 | Imepigwa picha na Maxime Agnell tarehe Unsplash |
| Jalada la Mbele | Imepigwa picha na Free-Photos tarehe Pixabay |

# - SAFARI -

Mitume ni 'wale waliotumwa' wa kanisa la kwanza. Paulo na mitume wengine walichukua safari kubwa ya imani. Walipata njia ya kuwaeleza watu habari za ujumbe wa Yesu na kuchukua muda kuonyesha upendo na nguvu za Yesu kwenye jumuia na vijiji vingi. Hapo mwanzo waliwafundisha watu kuishi kwa kweli ya Yesu, wakisambaza ujumbe na matendo ya upendo wa Yesu kwao wenyewe. Haikuwahusu mitume wenyewe, iliwahusu watu wote.

Hapa ndipo unapohusika. Dignity imeanzisha ***Safari***, kozi ya kukusaidia kufuata hatua za wafuasi wa kwanza wa Yesu. Tunataka wewe ujifunze namna ya kuchukua hatua hizo wewe mwenyewe.

Kujifunza ***Safari*** itakupa wewe nafasi ya kujifunza kufanya kazi na Mungu, kuanzia kwenye kijiji chako au jumuia. Huhitaji kuhudhuria shule. Utajifunza mafundisho mahali pale pale ulipo, hata na marafiki wanaokuzunguka. Wakati kozi inapoendelea utawashirikisha watu ujumbe na upendo wa Yesu kila siku kwa wanakijiji na jumuia inayokuzunguka.

***Safari*** ni mtiririko wa mavipindi manne. Katika kila vipindi utajifunza namna ya kushiriki upendo na ujumbe wa Yesu kwa kuanzisha Vikundi vya Uzima au kuwasaidia wengine kufanya hivyo. Utaenda kwenye somo linalofuata wakati kazi ya matendo imekamilika. Tunataka kukuwezesha wewe kuanzisha kazi kwa matendo badala ya kujifunza tu neno la Mungu.

***Safari Kijijini*** inawasaidia watu binafsi kutambua hali iliopo sasa kwenye vijiji vyao na namna Kikundi cha Uzima inavyokuleta upendo wa Yesu na kujenga umoja. Watu binafsi watakuwa wameanzisha Kikundi cha Uzima mwisho wa vipindi hili.

Wasiliana nasi kwa hello@dignityonline.org.uk au +**447340573937**.
Kwa mtiririko wa vitabu vyetu na bei tembelea mtandao wetu:
**www.dignityonline.org.uk/publications**

Swahili Toleo la Kwanza

© Dignity. Dignity chama cha kusaidia kilichosajiliwa no. 1122656.
Dignity (Worldwide) ni kampuni iliyodhibitiwa na dhamana, iliyosajiliwa Uingereza na Wales no 6394480.

DIGNITY
www.dignityonline.org.uk